

**MAKOSA YA KISARUFI KATIKA VYOMBO VYA HABARI VYA
TANZANIA: UCHUNGUZI WA TBC1, ITV NA STAR TV**


ALCHERAUS RWEGASILA MUSHUMBWA

**TASNIFU ILIYOWASILISHWA IKIWA NI SEHEMU YA KUTIMIZA MASHARTI
YA KUTUNUKIWA SHAHADA YA UZAMILI YA KISWAHILI (ISIMU)
KATIKA IDARA YA LUGHA NA TAALUMA ZA FASIHI YA
CHUO KIKUU HURIA CHA TANZANIA**

2022

UTHIBITISHO

Aliyetia saini hapo chini anathibitisha kwamba, amesoma tasnifu hii yenye anuani “**Makosa ya Kisarufi katika Vyombo vya Habari vya Tanzania: Uchunguzi wa TBC1, ITV na STAR TV**” na kupendekeza ikubaliwe na Chuo Kikuu Huria cha Tanzania kwa ajili ya kutunukiwa Shahada ya Uzamili katika Kiswahili (Isimu) ya Chuo Kikuu Huria Cha Tanzania.



Dr. Salma O. Hamad.

(Msimamizi)

Tarehe.....

HAKIMILIKI

Haki zote zimehifadhiwa. Hairuhusiwi kuiga, kunakili, kuzalisha au kusambaza sehemu yoyote ya tasnifu hii bila kibali cha maandishi kutoka kwa mwandishi au Chuo Kikuu Huria cha Tanzania kwa niaba, isipokuwa kwa shughuli halali, kama vile kwa ajili ya utafiti, kujisomea au kufanya marejeo ya kitaaluma.

TAMKO

Mimi, **Alcheraus Rwegasila Mushumbwa**, nathibitisha kuwa tasnifu hii ni kazi yangu halisi na haijawahi kuwasilishwa katika chuo kikuu kingine chochote kwa ajili ya kutunukiwa shahada kama hii au nyingine yoyote.



.....
Saini

.....
Tarehe

TABARUKU

Kazi hii naitabaruku kwa Mwendazake, **Dotto Charles Biseko** (PG201800620), mwanafunzi mwenzetu tuliyeanza pamoja safari ya kuisaka digrii ya Umahiri katika Kiswahili ya Chuo Kikuu Huria cha Tanzani. Lakini, kwa mapenzi ya Mola, mwenzetu alitangulia mbele ya haki kabla ya kumaliza safari tuliyoianzisha. Naamini huko aliko atakuwa na faraja kuona wenzake aliotuacha katikati ya safari tumefikia kilele cha safari. Apumzike kwa Amani huko aliko.

SHUKURANI

Kwanza kabisa, namshukuru Mola kwa kuniongoza vema katika safari yangu ya masomo tangu darasa I hadi Sahada ya Umahiri. Bila yeze nisingefua dafu.

Pili, nawashukuru wazazi wangu pamoja na ndugu zangu kwa kushirikiana nami katika kunitia moyo wakati wa masomo yangu. Msaada na kunitia moyo kwao pindi nilipokaribia kukata tamaa kulinisaidia kupambana hadi kufikia hatua hii.

Tatu, kwa umuhimu wa pekee namshukuru sana msimamizi wangu, Dkt. Salma Omar Hamad kwa kukubali kunisimamia katika utafiti huu, kuniongoza, kunielekeza na kunishauri ili kufanya kazi bora, ambayo matunda yake ni tasnifu hii. Hakika, bila kuchoka na kwa upendo wote amekuwa msaada mkubwa kwangu katika kutimiza utafiti huu. Mungu azidi kumbariki na kumjalia moyo huohuo wa usaidizi kwa wanafunzi wengine.

Nne, nawashukuru sana wahadhiri wa Chuo Kikuu Huria cha Tanzania walionifundisha kozi za umahiri. Wakiongozwa na Mzee Bakari Kombo, Dkt. Zelda Elisifa, Dkt. Salma Omar, Dkt. Hadija Jilala na Dkt. Nasra Habibu. Mihadhara pamoja na ushauri wao vilinijenga vema katika taaluma ya isimu ya Kiswahili.

Tano, nawashukuru wanafunzi wenzangu tuliokuwa pamoja katika darasa la isimu ya Kiswahili (2018-2020). Nao ni Lubadanja Enocy, Monica Mwacha, Joromba Sophia, Dotto Biseko (marehemu) na Oliver August. Ushirikiano wao umenisaidia sana kuweza kufikia hatua hii. Nawashukuru sana.

Mwisho, japo si kwa umuhimu, namshukuru Bw. Ndibalema Khatibu, kwa msaada wake, hasa wa kusaidia kupanga kazi hii hadi kuonekana katika umbo hili la kitasnifu. Hakika, nikiri kuwa bila yeze kazi hii ingelikuwa ngumu sana kwangu.

IKISIRI

Utafiti huu ulichunguza makosa ya kisarufi kwenye vyombo vya habari vya Tanzania. Umakini uliwekwa kwenye channeli za TBC1, ITV na STAR TV. Utafiti uliongozwa na malengo matatu: Kuchunguza aina za makosa ya kisarufi katika vyombo vya habari; sababu za kufanyika kwa makosa ya kisarufi; na, hatua za utatuzi wa makosa hayo. Ili kutimiza malengo hayo, data zilikusanywa kutoka uwandani na mactabani kwa kutumia mbinu za usomaji wa matini, usikilizaji na utazamaji wa taarifa za habari, na hojaji. Aidha, nadharia mbili ziliongoza ukusanyaji na uchambuzi wa data za utafiti huu. Nadharia hizo ni Uchanganuzi wa Habari Kisarufi ya van Dijk (1988) na nadharia ya Uchanganuzi Makosa ya Corder (1976). Mkabala wa kitaamuli ulitumika katika kuchambua data na kuwasilisha matokeo ya utafiti. Data zilichanganuliwa na kufafanuliwa kwa maelezo na mifano ya kutosha. Matokeo ya utafiti yameonesha kuwa kuna makosa mbalimbali ya kisarufi katika vyombo vya habari vya Tanzania kama makosa ya kimsamiati, kimatumshi, kimaumbo, kimuundo na kisemantiki. Pia, utafiti ulibaini kuwa kuna sababu za kufanya makosa ya kisarufi kwenye vyombo vya habari ambazo ni kukosa umahiri wa lugha (Kiswahili), athari ya lugha ya kwanza, kasumba, kutomudu sarufi ya Kiswahili, ufahamu wa lugha zaidi ya moja na ukosefu wa taaluma ya lugha kwa wanahabari. Vilevile, hatua za kuchukua ili kuepuka makosa zilizopendekezwa ni ufundishaji wa taaluma ya lugha kwa wanahabari, utoaji wa semina za matumizi sahihi ya lugha, vyombo vya habari kuajiri au kutumia wataalamu wa lugha, kutungwa kwa sheria za matumizi ya lugha na kufanya uhariri kwa kina kabla ya kutoa habari. Kutokana na utafiti huu, kuna haja ya tafiti nyingine kuendelea kufanyika kuhusu makosa mengine ya lugha yanayofanyika katika vyombo vya habari pamoja na athari zake.

Maneno Makuu: *Kimatumshi, Kimaumbo na Kisintakisia*

YALIYOMO

UTHIBITISHO	ii
HAKIMILIKI.....	iii
TAMKO.....	iv
TABARUKU	v
SHUKURANI.....	vi
IKISIRI..	vii
YALIYOMO.....	viii
ORODHA YA MAJEDWALI	xiii
VIFUPISHO NA ALAMA	xiv
UFAFANUZI WA DHANA.....	xv
SURA YA KWANZA: UTANGULIZI	1
1.1 Utangulizi.....	1
1.2 Usuli wa Mada	1
1.2.1 Televisheni ya TBC1	4
1.2.2 Televisheni ya ITV.....	5
1.2.3 Televisheni ya STAR TV.....	6
1.3 Tatizo la Utafiti	6
1.4 Malengo ya Utafiti	7
1.4.1 Lengo Kuu la Utafiti	7
1.4.2 Malengo Mahususi.....	7
1.5 Maswali ya Utafiti.....	8
1.6 Umuhimu wa Utafiti	8

1.7	Mawanda na Mipaka ya Utafiti.....	9
1.8	Muhtasari wa Sura	10

SURA YA PILI: MAPITIO YA KAZI TANGULIZI NA KIUNZI CHA

NADHARIA.....	11
----------------------	-----------

2.1	Utangulizi.....	11
2.1.1	Dhana ya Makosa ya Lugha na Makosa ya Kisarufi	11
2.1.2	Makosa ya Lugha na Makosa ya Kisarufi kwa Watumiaji wa Lugha	13
2.2	Makosa ya Lugha na Makosa ya Kisarufi kwenye Vyombo vyा Habari.....	17
2.2.1	Makosa ya Lugha na Makosa ya Kisarufi kwenye Vyombo vyा Habari Vinavyotumia Lugha Zingine	18
2.2.2	Makosa ya Lugha katika Vyombo vyा Habari Vinavyotumia Kiswahili	24
2.3	Pengo la Utafiti	28
2.4	Kiunzi cha Nadharia.....	30
2.4.1	Kiunzi cha UHK	30
2.4.2	Kiunzi cha Nadharia ya UM	34
2.5	Muhtasari wa Sura	36

SURA YA TATU: MBINU ZA UTAFITI.....	37
--	-----------

3.1	Utangulizi.....	37
3.2	Eneo la Utafiti	37
3.3	Wango la Utafiti/ Watafitiwa.....	38
3.4	Sampuli na Usampulishaji	38
3.4.1	Sampuli ya Utafiti	38
3.4.2	Usampulishaji	41

3.5	Mbinu za Ukusanyaaji wa Data	44
3.5.1	Usomaji wa Matini.....	44
3.5.2	Utazamaji na Usikilizaji.....	45
3.5.3	Hojaji.....	45
3.6	Uchambuzi wa Data na Uwasilishaji wa Matokeo	46
3.7	Muhtasari wa Sura	48
SURA YA NNE: UWASILISHAJI NA UCHAMBUZI WA DATA		49
4.1	Utangulizi.....	49
4.2	Makosa ya Kisarufi katika Habari za TBC1, ITV na STAR TV	49
4.2.1	Makosa ya Kimsamiati	50
4.2.1.1	Matumizi ya Neno la Kiingereza	50
4.2.1.2	Matumizi ya Neno Lisilostahili	53
4.2.1.3	Kuandika Neno Isivyo	55
4.2.1.4	Udondoshaji wa Neno	58
4.2.1.5	Uchopekaji wa Neno Lisilohitajika.....	60
4.2.1.6	Kosa la Kutumia Maneno Yasiyo Sanifu.....	61
4.2.2	Makosa ya Kimatamshi.....	62
4.2.3	Makosa ya Kimaumbo	67
4.2.3.1	Kosa la Umoja na Wingi.....	68
4.2.3.2	Kosa la Uchopekaji wa Kipashio Kisichostahili.....	69
4.2.3.3	Kosa la Udondoshaji wa Kipashio	72
4.2.4	Makosa ya Kimuundo	73
4.2.4.1	Kosa la Upatanisho wa Kisarufi.....	74

4.2.4.2	Kosa la Mpangilio Usio Sahihi	77
4.2.4.3	Kosa la Urudiaji wa Maneno	78
4.2.5	Makosa ya Kisemantiki.....	80
4.2.5.1	Kosa la Utata.....	81
4.2.5.2	Kosa la Kukosa Mantiki.....	82
4.2.5.3	Kosa la Kutokueleweka kwa Kilichoelezwa.....	84
4.2.6	Mjadala	85
4.3	Sababu za Makosa ya Kisarufi katika Habari za TBC1, ITV na STAR TV	91
4.3.1	Kukosa Umahiri wa Lugha	91
4.3.2	Athari ya Lugha ya Kwanza/Mama	94
4.3.3	Kasumba	96
4.3.4	Kutomudu Sarufi ya Kiswahili	98
4.3.5	Ufahamu wa Lugha zaidi ya Moja.....	100
4.3.6	Ukosefu wa Taaluma ya Lugha kwa baadhi ya Wanahabari.....	101
4.4	Hatua za Kuchukuliwa ili Kuepuka Makosa ya Kisarufi katika Habari za TBC1, ITV na STAR TV	103
4.4.1	Ufundishaji wa Taaluma ya Lugha (Sarufi) ya Kiswahili kwa Wanahabari	103
4.4.2	Utoaji wa Semina za Matumizi Sahihi ya Lugha.....	106
4.4.3	Kuajiri au Kutumia Wataalamu wa Lugha katika Vyombo vya Habari	108
4.4.4	Kutungwa kwa Sheria Zinazolinda Matumizi Sahihi ya Lugha	110
4.4.5	Kufanyika kwa Uhariri wa Kina	111
4.5	Muhtasari wa Sura	112

SURA YA TANO: MUHTASARI, HITIMISHO NA MAPEDEKEZO	113
5.1 Utangulizi.....	113
5.2 Muhtasari wa Jumla	113
5.3 Muhtasari wa Matokeo	115
5.4 Hitimisho.....	117
5.5 Mapendekezo	118
5.5.1 Mapendekezo ya Kuepuka Makosa	118
5.5.2 Mapendekezo ya Tafiti Zingine juu ya Mada hii	120
MAREJELEO	122
VIAMBATISHO	132

ORODHA YA MAJEDWALI

Jedwali 3.1:	Wango la Chaneli na Sampuli yake	39
Jedwali 3.2:	Idadi ya Matini za Habari.....	39
Jedwali 3.3:	Idadi ya Watafitiwa (Hadhira na Wanahabari)	40
Jedwali 4.2.1.1:	Kosa la Matumizi ya Neno la Kiingereza	51
Jedwali 4.2.1.2:	Kosa la Kutumia Neno Lisilostahili.....	54
Jedwali 4.2.1.3.1:	Kosa la Kuunganisha Maneno	56
Jedwali 4.2.1.3.2:	Kosa la Kutenganisha Neno	58
Jedwali 4.2.1.4:	Kosa la Udondoshaji wa Neno.....	59
Jedwali 4.2.2.1:	Taratibu za Utamkaji wa Konsonanti za Kiswahili kwa Sifa za Mahali na Jinsi ya Utamkaji	63
Jadwali 4.2.2.2:	Taratibu za Utamkaji wa Irabu za Kiswahili	63
Jedwali 4.2.2.3:	Makosa ya Kimatamshi.....	65
Jedwali 4.2.3.1:	Kosa la Umoja na Wingi.....	68
Jedwali 4.2.3.2:	Kosa la Uchopekaji wa Kipashio Kisichostahili.....	70
Jedwali 4.2.3.3:	Kosa la Udondoshaji wa Kipashio	72
Jedwali 4.2.4.1:	Kosa la Upatanisho wa Kisarufi.....	75
Jedwali 4.2.4.2:	Kosa la Mpangilio Usio Sahihi	77
Jedwali 4.2.4.3:	Kosa la Urudiaji wa Maneno	79
Jedwali 4.2.5.1:	Kosa la Utata.....	81
Jedwali 4.2.5.2:	Kosa la Kukosa Mantiki.....	83
Jedwali 4.2.5.3	Kosa la Kutokueleweka kwa Kilichoelezwa.....	84

VIFUPISHO NA ALAMA

BAKITA:	Baraza la Kiswahili la Taifa
BBC:	British Broadcasting Corporation
DW:	Deutsche Welle
EATV:	East Africa Television
FM:	Frequency Modulation
ITV:	Independent Television
KBC:	Kenya Broadcasting Corporation
K/Laini, K/Gumu	Kaakaa Laini, Kaakaa Gumu
MOMT:	Media Ownership Monitor Tanzania
MS:	Msailiwa
NUHU/M:	Nadharia ya Uchanganuzi wa Habari kama Usemi/Matini
STAR TV:	Star Television
TATAKI:	Taasisi ya Taaluma za Kiswahili
TUKI:	Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili
TBC:	Tanzania Broadcasting Corporation
TM:	Tafsiri ya Mtafiti
UHK:	Uchanganuzi wa Habari Kisarufi
UM:	Uchanganuzi Makosa
+	Ungana
→	Ilipaswa kuwa/imekuwa
—	Kipashio kilichodondoshwa
{ }	Mipaka ya mofu/ kiambishi
()	Mabano

//	Mipaka ya kimatamshi ya sauti au neno
\$	Mpaka wa silabi
§	Kipengele au sehemu

UFAFANUZI WA DHANA

- Blogu:** Ukurasa wa tovuti unaomilikiwa na mtu binafsi/taasisi wenyewe taarifa au mawazo au mada maalumu ambapo taarifa mpya huingizwa mara kwa mara.
- Chaneli:** Kituo kimojawapo kati ya vituo vingi vya shirika moja la televisheni.
- Lugha:** Lugha asilia ya binadamu itumiayo maneno na ishara (maandishi na mazungumzo).
- Makosa ya kisarufi:** Makosa yanayokiuka kanuni za kisarufi za lugha husika.
- Makosa ya lugha:** Matendo ya kuwasiliana kwa lugha yanayokiuka utaratibu maalumu wa lugha husika.
- Matini:** Habari iliyowasilishwa kwa mdomo au maandishi.
- Mkabala wa kitaamuli:** Mkabala wa utafiti unaotumika kuchambua, kuchanganua na kuwasilisha data bila kuhusisha takwimu.
- Redio:** Chombo kinachotoa matangazo yake kwa mazungumzo tu.
- Sarufi:** Sheria, kanuni au taratibu zinazotawala matumizi ya lugha husika katika viwango vya matamshi, maumbo, miundo na maana.
- Sinhala:** Mojawapo ya lugha zinazopatikana na kuzungumzwa nchini Sirilanka.

- Televisheni:** Chombo kinachonasa picha, sauti na maandishi kutoka kituo cha kurushia matangazo na kuvionesha pamoja na kutoa sauti iliyonaswa.
- Vyombo vyahabari:** Vyombo vinavyojishughulisha na utoaji wa matangazo na habari kwa umma kama redio, televisheni, blogu, magazeti n.k.
- Umahiri:** Kutumia lugha kwa ufasaha au sahihi.
- Umilisi:** Ujuzi wa kanuni zinazotawala lugha fulani.
- Utendaji:** Usemaji wa lugha dhahiri wa mtu binafsi.
- Wango:** Jumla ya watu au vitu vyote vinavyofaa kutafitiwa.

SURA YA KWANZA

UTANGULIZI

1.1 Utangulizi

Utafiti uliozaa tasnifu hii ulichunguza makosa ya kisarufi katika vyombo nya habari nya Tanzania kwa kumakinikia TBC1, ITV na STAR TV. Sura hii inafafanua taarifa za awali za utafiti ambazo ni usuli wa mada na vyombo nya habari vilivyotafitiwa, tatizo la utafiti, malengo ya utafiti, maswali ya utafiti, umuhimu wa utafiti, mawanda na mipaka ya utafiti, na muhtasari wa sura.

1.2 Usuli wa Mada

Mojawapo ya mambo muhimu yanayofanya maisha ya binadamu kuwa na maana ni mawasiliano. Mawasiliano ni kupeana taarifa au kupashana habari baina ya watu wawili au zaidi kwa kutumia njia mbalimbali (TUKI, 1990; Massamba 2007; Bukagile, 2007; Kadeghe, 2012; TATAKI, 2013; BAKITA, 2015). Mawasiliano ya binadamu hufanywa kwa namna mbalimbali kulingana na ubunifu wa wawasilianaji. Namna kuu mbili zinazotumika kwa kiwango kikubwa ni ishara na lugha. Mawasiliano ya binadamu hutawaliwa na lugha kwa kiasi kikubwa. Lugha hiyo huitwa lugha asilia ambayo, kwa mujibu wa wanaisimu, ni mfumo au utaratibu wa mpangilio maalumu wa sauti nasibu za binadamu ziambatanazo na ishara zenye maana zilizokubaliwa na jamii fulani ya watu ili zitumike katika mawasiliano baina yao (Massamba, 2007: 64; Matinde, 2012; Wanjala na Kavoi, 2013). Kwa msingi huo, lugha ni chombo kikuu cha mawasiliano ya binadamu, ambacho hutumika kupashana habari miongoni mwa watu. Ijapokuwa lugha ni nyenzo muhimu katika mawasiliano ya binadamu, bado matumizi yake yanakumbwa na makosa mbalimbali

yanayofaywa na wawasilianaji. Makosa hayo ndiyo yaliyochunguzwa kwenye vyombo vyahabari na kuazaa tasnifu hii.

Makosa katika matumizi ya lugha ya binadamu ni jambo ambalo ni gumu kuepukika au kuzuulika kabisa. Hii ni kwa sababu watumiaji wa lugha hufanya makosa ya kila aina, na ya mara kwa mara katika mawasiliano ya kimazungumzo au kimaandishi. Makosa hayo huwa na sababu zake kulingana na mazingira yanayotinga mwasilianaji au lugha yenye. Tunaweza kuhusisha sababu za makosa ya lugha na mtazamo wa Chomsky (1965). Kwa mujibu wa Chomsky, lugha ni tukio la kiakili/kisaikolojia. Hivyo, lugha humiliwa akilini mwa mzungumzaji-msikilizaji wa jamiilugha fulani, ambaye anaifahamu vizuri lugha ya jamii yake pasi kuathiriwa na upotofu wa hali za kisarufi kama mkwamo wa kumbukumbu, upunguani, kukosa makini na kubadili nia, na makosa ya kudhihirisha maarifa yake ya lugha kwenye utendaji halisi (Chomsky, 1965:3-4). Kwa maelezo ya Chomsky, ni wazi kwamba maarifa ya mtumiaji wa lugha huweza kuathiriwa na sababu mbalimbali kiasi cha kuleta upotofu wa kile ambacho msemaji na msikiliza walilenga, na hivyo kusababisha makosa. Chomsky anaendelea kufafanua kwamba binadamu hutumia vitengo vikuu viwili vyahabari ni umilisi/maarifa na utendaji. Umilisi ni ujuzi au welewa wa kanuni zinazotawala lugha husika unaohodhiwa akilini mwa msemaji/msikilizaji wa jamiilugha fulani na kila msemaji asilia wa lugha yake huwa nao. Utendaji ni matumizi halisi (usemaji au uandishi) ya lugha katika muktadha mahususi (Chomsky, 1965: 4). Ujuzi wa lugha unaomilikiwa na msemaji huweza, wakati mwingine, kutoakisiwa na utendaji katika uhalisia kwa sababu, kwa mujibu wa Chomsky, utendaji huathiriwa na mambo kadhaa kama kasoro za matamshi, masuala

ya kihisia (hasira, woga, furaha), uchovu, ulevi, ulemavu, athari za mazingira, maradhi na matumizi ya kanuni za lugha (Chomsky, 1965:3; Habwe na Karanja, 2004; Matinde, 2012:226; Ligembe, 2017).

Kwa upande mwagine, makosa ya lugha yanahusishwa na ujifunzaji wa lugha (hasa ya pili) (Corder, 1967; Touchie, 1986; Jing, Xiaodong & Yu, 2016; Jin, 2019) na ujuzi/umahiri. Kulingana na Greene (2003) na Hargie (2006), ujuzi au umahiri huchangia makosa katika mawasiliano ya lugha. Ujuzi/umahiri ni chanzo cha makosa pale ambapo mwasilianaji ambaye hana ujuzi/umahiri hufanya makosa mengi kuliko mwenye ujuzi/umahiri. Hivyo, mzungumzaji mwenye ujuzi atafanya makosa machache kuliko mzungumzaji asiyé na ujuzi. Maoni ya wataalamu hao yanathibitisha kwamba katika mawasiliano ya lugha, makosa hujitokeza, na kwa maelezo yao, makosa hayo husababishwa na kiwango cha ujuzi wa mtumiaji wa lugha. Hivyo, utafiti huu ulichunguza makosa ya lugha na sababu zake katika vyombo vyá habari ukimakinikia yale ya kisarufi.

Kama ambavyo aya zilizotangulia zinavyoeleza, ni wazi kwamba suala la makosa ya lugha ni jambo ambalo linachukua nafasi katika mawasiliano ya lugha za binadamu kila mara. Madai haya yamewahi kuthibitishwa na mwanaisimu Fry (1969) anaposema “kila wakati upitao, mamilioni ya maneno hutamkwa kutoka kwa msemaji hadi msikilizaji katika muktadha maalumu wa ulimwengu. Katika mawasiliano ya namna hiyo, makosa kadhaa ya maneno hutokea ama kwa upande wa msemaji au msikilizaji.” Maelezo ya Fry yanaendelea kuthibitishwa na tafiti mbalimbali zinazoonesha uwapo wa makosa katika lugha mbalimbali kama vile Kiingereza, Kifaransa, Kichina, Kijerumaní, Kiarabu na Kiswahili (Zhang, Zhou,

Huang & Pan, 2000; DeCapua, 2008; Huang, Wu & Chang, 2007; Idarus, 2010; Tarawneh & Almomani, 2013; Frost, 2016). Hata hivyo, tafiti na maandiko mengi yaliyoshughulikia makosa ya lugha yamejikita kuchunguza kwa kina makosa yanayofanywa na wanaojifunza lugha ya kwanza au ya pili kwa kiwango kikubwa. Tafiti za makosa ya lugha kwa wajuzi wa lugha hasa wale ambao lugha yao ni ya asili, hazijafanyika vya kutosha na kutokana na upeo wa mtafiti amepata andiko moja la (Idarus, 2010) lihusulo makosa yanayofanywa mara kwa mara na watumiaji wa Kiswahili, pamoja na andiko la Frost (2016) lililozungumzia tu makosa 20 yaliyozoleka kwa watumiaji wa Kiingereza wakiwamo wazawa wa lugha hiyo. Hivyo, utafiti huu ulichunguza makosa ya kisarufi katika vyombo vya habari vya Kiswahili vya Tanzania, yanayofanywa na wanahabari wazawa wa lugha ya Kiswahili. Umakini uliwekwa kwenye televisheni za TBC1, ITV na STAR TV.

1.2.1 Televisheni ya TBC1

TBC1 ni mojawapo ya channeli za televisheni ya taifa iliyo chini ya Shirika la Utangazaji Tanzania. Shirika hili humilikiwa na serikali ya Tanzania kwa asilimia 100 (Sturmer, 1998; Media Ownership Monitor Tanzania [MOMT], 2018). TBC kama chombo cha utangazaji kabla ya kupitia mabadiliko na vipindi mbalimbali lilianzishwa mnamo mwaka 1957 kama kituo cha redio (Sturmer, 1998:80). Kipindi hicho Tanganyika ikiwa chini ya utawala wa Mwingereza. Hata hivyo, mara baada ya uhuru serikali ilianzisha mchakato wa utaifishaji wa baadhi ya mali zilizokuwa chini ya serikali ya mkoloni na watu binafsi. Kwa mujibu wa Sturmer (1998:112-115), juhudzi za utaifishaji wa TBC zilianza rasmi kujadiliwa bungeni na hatimaye mnano tarehe 1 Julai, 1965, TBC ilitaifishwa rasmi na kuwa chombo cha habari

kinachomilikiwa na serikali baada ya mswada wa utaifishaji kupitishwa na kuwa sheria rasmi. Utaifishaji huo uliifanya TBC kubadilishwa jina na kuitwa Radio Tanzania Dar es Salaam (RTD) chini ya Wizara ya Habari, Utangazaji na Utalii.

Hata hivyo, mchakato wa kukifanya chombo hiki kuwa na hadhi ya shirika, kutoka kwene hadhi ya kituo cha utangazaji ultimia mwaka 1992 ambapo sheria ya Mashirika ya Umma ilitungwa na kulitambua TBC kama shirika la umma linalotoa huduma ya utangazaji kwa umma kwa njia ya redio na televisheni (MOMT, 2018: 88). Kama shirika la habari, TBC linamiliki idhaa za redio za TBC Taifa, TBC FM na TBC International; channeli za televisheni za TBC1 TBC2 na Safari Chennel. Shirika hili hutoa matangazo yake kwa lugha ya Kiswahili kwa asilimia kubwa isipokuwa idhaa ya TBC International. Kwa kuwa ni shirika la umma, asilimia 75 ya vipindi vyake vinatakiwa viwe vya habari na elimu, na asilimia 25 tu viwe vya burudani. Kwa hiyo, malengo makuu ya TBC ni kuelimisha na kupasha habari kuhusu masuala ya kitaifa na kimataifa (MOMT, 2018:88). Hivyo, mtafiti alichunguza habari zinazotolewa na channeli ya TBC1 tu.

1.2.2 Televisheni ya ITV

ITV ni televisheni iliyo chini ya kampuni ya IPP Media Limited (MOMT, 2018:75) na hupatikana Tanzania bara. ITV ilianza shughuli zake mwaka 1994 (Sturmer, 1998:194) ikiwa na kituo kimoja cha televisheni (ITV) na kimoja cha redio (Radio One). ITV hutoa matangazo yake Tanzania. Kituo hiki kinamilikiwa na kampuni binfsi ya IPP Media iliyo chini ya familia ya Dkt. Reginald Abraham Mengi. Televisheni hii hutoa matangazo yake kwa saa 24 za siku na hutangaza vipindi vyake kwa lugha ya Kiswahili.

1.2.3 Televisheni ya STAR TV

STAR TV ni kituo cha televisheni cha binafsi kilichopo Mwanza, Tanzania bara, na kinamilikiwa na kampuni ya Sahara Media Group. Kulingana na MOMT (2018: 92), kituo hiki kilianzishwa mwaka 2000 na hivi sasa kina watazamaji wengi hasa katika Kanda ya Ziwa na Nyanda za Juu Kusini. Kituo hiki chenye vipindi hasa nya habari na matukio, pia hutangaza burudani, maigizo na michezo kwa lugha ya Kiswahili.

1.3 Tatizo la Utafiti

Pamoja na juhudzi za wataalamu mbalimbali wa lugha kuhoji na kushauri uepukaji wa makosa ya lugha ili kutumia Kiswahili fasaha kwenye vyombo nya habari nya Tanzania, bado tunazidi kushuhudia makosa mbalimbali ya lugha kwenye vyombo nya habari nya Tanzania. Kwa mujibu wa wataalamu mbalimbali wa lugha, kuna makosa ya lugha kwenye vyombo nya habari nya Tanzania vinavyotumia Kiswahili katika matangazo na utoaji wa habari (Maina, 2013; Sewangi, 2017; Sigalla, 2019). Makosa hayo hudaiwa kuwa ni ya mara kwa mara (Maina, 2014; Sewangi, 2017). Kwa maoni ya watafiti, asilimia kubwa ya wanahabari hasa wa karne ya 21, hutumia lugha isiyo sahihi au sanifu katika kuhabarisha umma. Hali hiyo imekuwa sababu ya makosa kadha wa kadha kufanyika katika vyombo nya habari na kusababisha uharibifu wa Kiswahili na kusambaza lugha isiyo fasaha kwa hadhira ambayo huamini yanayosemwa na vyombo hivyo (Massamba, 1995; Ponella, 1995; Simba, 1995; Shoo, 2004; Maina, 2013, 2014 na Sewangi, 2017). Maandiko ya wataalamu hao yanasisitiza kuwa kufanya makosa ya lugha katika vyombo nya habari bila kudhibitiwa, ni kuendeleza utamaduni wa kubananga lugha unaoweza kuzaa mtindo wa lugha isiyo fasaha na kuenea ukichukuliwa na hadhira kuwa ni lugha sahihi.

Hali hii inadhihirisha kuwa makosa ya lugha katika vyombo vya habari vya Tanzania vinavyotumika Kiswahili, ni tatizo ambalo linaendelea kuwapo na halijatatuliwa. Tatizo hili linahitaji kuendelea kufanyiwa tafiti kwa ajili ya kulitafutia ufumbuzi zaidi. Kwa hivyo basi, utafiti huu ulilenga kuwa sehemu ya ufumbuzi wa tatizo hili kwa kuchunguza makosa ya kisarufi yanayofanyika kwenye vyombo vya habari vya Tanzania ili kuyatafutia utatuzi utakaoendeleza juhudini zilizokwishaanzishwa za kuhimiza matumizi ya Kiswahili fasaha kwenye vyombo vya habari na hadhira yake.

1.4 Malengo ya Utafiti

Utafiti uliongozwa na lengo kuu moja na malengo mahususi yafuatayo:

1.4.1 Lengo Kuu la Utafiti

Utafiti uliongozwa na lengo kuu moja ambalo ni kuchunguza makosa ya kisarufi katika vyombo vya habari vya TBC1, ITV na STAR TV ili kuyatafutia masuluuhisho yatakayosaidia kuepuka makosa hayo kwa ajili kutumia na kueneza Kiswahili fasaha.

1.4.2 Malengo Mahususi

Ili kutimiza lengo kuu, malengo mahususi matatu yaliongoza utafiti huu, nayo ni:

- i) Kubainisha makosa ya kisarufi yanayofanywa katika habari za TBC1, ITV na STAR TV.
- ii) Kubainisha sababu za makosa ya kisarufi yanayofanywa katika habari za TBC1, ITV na STAR TV.
- iii) Kupendekeza hatua za kuchukuliwa ili kuepuka makosa ya kisarufi katika habari za TBC1, ITV na STAR TV.

1.5 Maswali ya Utafiti

Ili kuweza kutimiza malengo, utafiti aliongozwa na maswali yafuatayo:

- i) Ni makosa ya kisarufi yapi yanayofanywa katika habari za TBC1, ITV na START TV?
- ii) Ni sababu zipi zinazosababisha kufanyika kwa makosa ya kisarufi katika habari za TBC1, ITV na STAR TV?
- iii) Ni hatua zipi zinapaswa kuchukuliwa ili kuepuka kufanya makosa ya kisarufi katika habari za TBC1, ITV na STAR TV?

1.6 Umuhimu wa Utafiti

Utafiti wowote wa kitaaluma hutegemewa kuwa na mchango fulani katika jamii pindi ukamilikapo. Kama tafiti nyingine za lugha, utafiti huu una umuhimu katika uwanja wa sarufi hasa kwa kuonesha makosa ya kisarufi, sababu na hatua za kuchukuliwa kuepuka makosa hayo katika vyombo vyahabari wakati wa kutoa habari kwa umma. Kwa kufanya hivyo, wanaisimu na watumiaji wa Kiswahili watakuwa na maarifa juu ya makosa ya kisarufi yanayofanywa kwenye vyombo vyahabari vya Tanzania. Pia, utafiti umeziba pengo la kimaarifa lililokuwapo kwenye tafiti za makosa ya lugha. Hii ni kwa sababu tafiti nyingi zilijikita kuchunguza makosa ya lugha yanayofanywa na wanafunzi wa lugha ya pili na ya kwanza, huku zikupuuza makosa yanayofanywa na wazungumzaji wa lugha ambao ni wazawa wa lugha husika na wana ujuzi wa lugha yao. Aidha, utafiti utasaidia katika kuimarishe na kuinua kiwango cha ujuzi wa lugha kwa watumiaji wa Kiswahili kupitia vyombo vyahabari. Umuhimu huo umedhihirika kwenye marekebisho (ukosoaji) ya makosa

yaliyobainishwa pamoja na mapendekezo ya kuepuka makosa hayo katika sura ya 4 ya tasnifu hii.

1.7 Mawanda na Mipaka ya Utafiti

Utafiti ulishughulikia makosa ya lugha yanayofanywa na watumiaji wa Kiswahili katika vyombo vya habari nchini Tanzania hasa TBC1, ITV na STAR TV. Watumiaji wa lugha hufanya makosa mbalimbali wakati wa kuwasiliana kwa kutumia lugha zao. Miongoni mwa makosa hayo ni yale ya kisarufi. Makosa hayo hufanywa na watu wa rika na hadhi zote. Kwa hivyo, utafiti ulijikita kuchunguza makosa ya kisarufi kwenye vipengele vya msamati, matamshi, muundo na maana/mantiki katika lugha ya Kiswahili, yanayofanywa na wanahabari wazungumzao Kiswahili kama lugha yao na itumikayo kwenye channeli teule. Kwa upande wa malengo yaliyotimizwa yalikuwa ni kubainisha makosa ya kisarufi, sababu zake na hatua zinazopaswa kuchukuliwa ili kuepuka makosa hayo katika vyombo vya habari. Hata hivyo, utafiti huu haukushughulikia makosa ya lugha ambayo si ya kisarufi kwa kuwa sarufi ina mchango mkubwa sana katika kujenga ufasaha wa lugha kwa watumiaji wa lugha husika ambapo makosa mengine ya lugha yanaweza kuepukika ikiwa mtumiaji wa lugha anamudu sarufi. Aidha, utafiti haukushughulika na wanahabari ambao Kiswahili si lugha yao ya mawasiliano ya kila mara au wanaojifunza lugha hii kwa sababu, kwa upande wa wajifunzaji wa lugha ya pili/kigeni, tafiti nyingi zimekwishafanyika na kueleza kwa kina makosa yanayofanywa na wajifunzaji hao, sababu zake na mapendekezo ya kutatua makosa hayo.

1.8 Muhtasari wa Sura

Sura hii imefafanua taarifa za awali za tasnifu. Vipengele vilivyofafanuliwa ni usuli wa tatizo ambao umetoa sura ya jumla ya jambo linalochunguzwa na maelezo kuhusu vyombo vyaa habari vinayotafitiwa; tatizo la utafiti limefanuliwa ili kuonesha jinsi lilivyo; malengo ya utafiti na maswali yaliyoongoza utafiti yamewekwa bayana; umuhimu wa utafiti pamoja na mawanda yake vimeelezwa kwenye sura hii.

SURA YA PILI

MAPITIO YA KAZI TANGULIZI NA KIUNZI CHA NADHARIA

2.1 Utangulizi

Sura hii imeshughulikia kazi mbalimbali za kitafiti zinazohusu mada iliyotafitiwa. Hapa zimeelezwa baadhi ya tasnifu, makala, vitabu na nyaraka mbalimbali ambazo zimeandika juu ya mada ya utafiti. Yaliyofafanuliwa katika sura hii ni maandiko ambayo mtafiti aliyasoma ili kumpa maarifa zaidi juu ya mada. Pia, sura hii imefafanua nadharia zilizoongoza utafiti na hatimaye sura imeonesha pengo la maarifa lililohitajika kuzibwa.

2.1.1 Dhana ya Makosa ya Lughya na Makosa ya Kisarufi

Dhana ya makosa ya lugha imeshughulikiwa na wanaisimu mbalimbali kwa kutumia vigezo mbalimbali. Hata hiyo, kwa kiasi kikubwa wote wanaelekea kukubaliana kwenye fasili zao. Kwa mujibu wa Cummingsworth (1987), makosa ya lugha ni ukiukwaji wa kaida za lugha fulani ambao hutokea kiutaratibu maalumu. Aidha, Gass na Selinker (2008) wanaamini kwamba makosa ya lugha ni jambo la kimfumo kwani, hutokea mara kwa mara na huwa hayatambuliwi na msemaji (mjifunzaji au mzungumzaji wa kawaida) kama ni makosa. Mawazo ya wataalamu hao yanaungwa mkono na Feltsen (2009) anaposhadidia kwamba kosa katika lugha ni ukosefu wa umilisi wa lugha na ni jambo ambalo mtu hutakiwa kujifunza na kuelewa taratibu na hatimaye kulirekebisha. Fasili hizo zilimpatia mtafiti mwanga wa fasili iliyomwongoza kwenye utafiti kwamba, makosa ya lugha ni matendo ya kuwasiliana kwa kutumia lugha, ambayo yako kinyume na utaratibu maalumu wa lugha husika. Utaratibu huo hutokana na kaida za lugha zilizowekwa na kukubalika mionganoni mwa

wanajamiilugha husika. Hivyo, matendo hayo yanadhihirisha umilisi hafifu wa mtumiaji wa lugha anayehusika.

Kwa upande mwingine, makosa ya kisarufi hujikita katika sarufi ya lugha inayohusika. Sarufi kwa upande wake, ni taaluma inayochunguza na kuchambua kanuni, sheria au taratibu zinazotawala matumizi ya lugha husika katika viwango vyote vya matamshi, maumbo, miundo na maana (TUKI, 1990:29; Massamba, Kihore na Hokororo, 1999; Saluhaya, 2016). Kwa maana hiyo, makosa ya kisarufi huhusu sarufi ya lugha fulani. Pia, haya ni sehemu ya makosa ya lugha japokuwa si kila kosa la lugha ni la kisarufi. Kulingana na Saluhaya (2016:120), makosa ya lugha hujumuisha makosa ya kimamatamshi, kimsamiati, kimuundo na kimaana. Saluhaya (keshatajwa) anasisitiza kwamba vipengele hivyo vikitumiwa vibaya husababisha makosa ya kisarufi. Kwa maelezo haya tunaweza kusema kuwa kulingana na Saluhaya, makosa ya kisarufi ni matumizi mabaya ya vipengele vya kisarufi: matamshi, msamiati, muundo na maana. Fasili hiyo inakubaliwa na Mushumbwa (2018) anapofafanua kuwa makosa ya kisarufi ni ile hali ya mtu kuzungumza au kuandika kwa kukiuka kaida na taratibu za kisarufi za lugha fulani. Makosa ya kisarufi katika Kiswahili, ni uzungumzaji na uandikaji wa Kiswahili unaokiuka taratibu za sarufi ya Kiswahili, unaofanywa na baadhi ya wazungumzaji wa lugha ya Kiswahili. Aidha, haya ni makosa yanayofanywa kwa kujua au kutokujua katika kuwasiliana kwa njia ya maandishi au mazungumzo (Mushumbwa, 2018:13). Katika utafiti huu, mtafiti aliafikiana na fasili hizi na zilimwongoza wakati wa uchunguzi wa matini za habari za vyombo vilivyotafitiwa.

2.1.2 Makosa ya Lughya na Makosa ya Kisarufi kwa Watumiaji wa Lughya

Kama ilivvyeolezwa kwenye §1.2 kwamba katika mawasiliano ya binadamu makosa ya lughya hayakosi na ni vigumu kuepukika, watafiti wa isimu na lughya wamefanyia kazi jambo hili wakaibuka na maoni/mapendekezo kadhaa. Kipengele hiki kinafafanua tafiti na maandiko ya kitaaluma yaliyoeleza kuwapo kwa makosa ya kisarufi kwa watumiaji wa lughya.

Katika andiko lake maarufu la *Aspects of the Theory of Syntax* (1965), Chomsky anajaribu kutofautisha dhana za umilisi na utendaji katika lughya. Katika maeleo yake anakiri kwamba umilisi wa lughya (kanuni) anaomiliki msemaji wa lughya asilia huweza kuathiriwa na sababu kadhaa kama kasoro za ala za matamshi, uchovu, upunguani, hisia (hasira na furaha), ulevi, matumizi ya kanuni za lughya n.k. Athari hizo humfanya msemaji wa lughya kutokuwasilisha vema umilisi uliomo ubongoni mwake na hivyo kusababisha dosari katika mazungumzo. Mathalani, mtu mwenye hasira au furaha anaweza kutamka maneno kwa kigugumizi au maneno ambayo hakudhamiria kutamka na hivyo kufanya mawasiliano yalete kizingiti cha kuelewana na msikilizaji wake. Vivyo hivyo, katika kujaribu kufuata vema kanuni za lughya yake, msemaji anaweza kukosea na kutoa sentensi au tungo ambayo haikubaliki katika muktadha wa jamii yake, akawa amefanya kosa la kisarufi. Mawazo ya Chomsky kwa upande fulani yanaungwa mkono na Corder (1967: 166) anapokiri kwa kusema kuwa:

Sote twajua kwamba katika hali ya mazungumzo ya kawaida ya mtu mzima katika lughya zetu asilia tunaendelea kufanya makosa ya namna moja au nyingine. Makosa hayo yawenza kusababishwa na kukosa kumbukumbu, uchovu, hali ya mwili kutokuwa sawa, changamoto za kisaikolojia kama kuwa na hisia kali n.k. Hata hivyo, makosa hayo huwa si makosa ya kukosa umilisi wa lughya bali ni

makosa ya kiutendaji na pale ambapo tunapoyabaini tunaweza kuyarekebisha (T.M).

Maelezo ya Corder yanaafikiana na maoni ya Chomsky ila Corder anakwenda mbali zaidi akisisitiza kwamba makosa ya kiutendaji si makosa ya kiumilisi; hivyo, yanaweza kurekebishwa na msemaji mwenyewe pale yanapogunduliwa. Ikumbukwe kuwa, Corder (ameshatajwa) anatoa kauli hii akiwa anayatazama makosa ya lugha ya mzungumzaji anayejifunza lugha ya pili. Hata hivyo, ijapokuwa makosa yanayosababishwa na sababu zilizotajwa na Chomsky (1965:3-15) na Corder (1967:166) yanaweza kuchukuliwa kuwa si makosa ya kiumilisi na hayapaswi kupewa kipaumbele kwani si ya kiisimu; lakini, bado yana athari katika mawasiliano kwa kuwa yanaweza kusababisha mkwamo wa kimawasiliano na pasiwepo welewano baina ya msemaji na msikilizaji. Pamoja na hayo, maelezo ya wanaisimu hawa yalitoa mwanga kwa mtafiti kuweza kutofautisha makosa ambayo mtumiaji wa lugha anaweza kuyafanya akiwa katika hali yake ya kawaida na akiwa katika hali ambayo si ya kawaida. Utafiti huu ulichunguza makosa ya kisarufi ambayo wanahabari huyafanya wanapokuwa wanatangaza na kutoa habari kwenye vyombo vyao.

Fry (1969:69) akishughulikia ithibati za makosa ya uzungumzaji wa lugha, anakiri kwamba katika mawasiliano ya mdomo, makosa kadhaa hutokea kwa upande wa msemaji au msikilizaji. Pamoja na kutokea kwa makosa hayo, Fry (ameshatajwa) anafafanua kwamba inatokea, japo sio mara kwa mara, msemaji hutamka sauti au maneno mengine ambayo ni tofauti na alivyodhamiria kutamka. Au msikilizaji naye, huweza kuchukua jambo lingine tofauti na yale ambayo msemaji wake alimaanisha. Hali hii itokeapo, makosa hurekebishwa haraka; yale ambayo hufanywa na msemaji

hurekebishwa na msemaji mwenyewe, na yale ambayo ni ya msikilizaji hurekebishwa na msikilizaji au anaposhindwa kufanya hivyo basi ujumbe wa jumla wa msemaji humfanya msikilizaji arekebishe makosa yake hayo. Fry (1969: 71-73) anakwenda mbali zaidi na kutaja kwamba makosa ya uzungumzaji ni ya fonimu, mofimu na maneno. Makosa hayo hutokana na utamkaji vibaya wa sauti, ambao pia huathiri maumbo, na uteuzi mbaya wa maneno katika utamkaji. Madai ya Fry (1969:71-73) yanaungwa mkono na Biber, Johansson, Leech, Conrad na Finegan (1999), ambao wanathibitisha kuwa, urudiaji, ukatishaji wa mazungumzo au maneno na ugugumizi ni miiongoni mwa makosa yanayofanywa na wazungumzaji wa Kiingereza yasababishayo ukosefu wa mtiririko mzuri wa mazungumzo na mantiki ya lugha. Biber na wenzake (1999: 1053) wanaesema yapo makosa mengine ya utendaji kama usemi kuachwa ukielea.

Madai ya kuwapo kwa makosa ya mazungumzo katika lugha yaliyothibitishwa na Fry, Biber na wenzake, yanaafikiana na matokeo ya utafiti wa Hohenberger na Waleschkowski (2005) ambao walibainisha makosa ya kimazungumzo katika lugha ya Kijerumani kama urudiaji wa neno; ubadilishaji wa neno, mzizi na viambishi awali; udondoshaji na makosa mengine. Kwa maoni ya Berger (2003), makosa hayo hayafanywi ovyo. Anadai kuwa ikitokea kwa mfano, mtu akatamka neno ambalo hakulitarajia, atapakobadili atatamka neno ambalo liko katika kategoria ileile ya neno la mwanzo. Mathalani, mtu anasema kwamba '*funga mlango*' badala ya dirisha, atajirekebisha na kusema '*funga dirisha*'. Neno 'dirisha' ni nomino kama 'mlango.' Utafiti huo ulimsaidia mtafiti kufahamu baadhi ya makosa yanayofanywa katika mazungumzo na kujua sababu zake. Maarifa yanayopatikana katika tafiti za

wanataaluma hao yalimsaidia mtafiti kuchunguza jinsi watangazaji wa vyombo veya habari veya Tanzania wanavyoweza kufanya makosa ya utamkaji na sababu zake. Hata hivyo, mtafiti alikwenda mbali zaidi na kuchunguza habari zilizoandikwa katika tovuti za vyombo teule.

King'ei na Kobia (2007) wakitafiti jinsi *sheng* inavyoweza kukwaza lugha kuwa kitambulisho, wanaeleza kuwa wanafunzi huchanganya *sheng* katika kuwasiliana kwa Kiswahili au Kiingereza. Jambo hilo liliripotiwa na watafitiwa (walimu na wanafunzi) kuwa kuchanganya lugha ya *sheng* na, ama Kiswahili au Kiingereza ni kosa kwa sababu haitakiwi. King'ei na Kobia (2007:326) wanatoa mfano kwamba baadhi ya majina ya Kiingereza hutumiwa vibaya kwa kutanguliza kibainishi *a* mwanzoni. Pamoja na kwamba watafiti hao walimakinikia wanafunzi wa sekondari wakichunguza lugha za Kiswahili, Kiingereza na mtindo wa *sheng*, bado utafiti wao ulimsaidia mtafiti kuchunguza uchanganyaji wa misimbo kwenye habari za Kiswahili za vyombo veya habari veya Tanzania.

Idarus (2010: 173-187) alijikita kuchunguza makosa yanayofanywa kila mara na wazungumzaji wa Kiswahili katika mkoa wa Dar es Salaam. Uchunguzi wake uliibuka na makosa makuu manne ya msamiati, muundo, tafsiri sisisi na matamshi. Makosa hayo kwa mujibu wa Idarus, husababishwa na umilisi hafifu wa msamiati wa Kiswahili, athari ya lugha mama na lugha ya Kiingereza, tafsiri sisisi na Kiswahili cha mtaa. Uchunguzi wa Idarus (2010), unaungwa mkono na Masebo na Nyangwine (2016), Saluhaya (2016:120-121) na Mushumbwa (2018:13-17) wanapoonesha kuwa makosa ya kisarufi katika lugha ya Kiswahili ni ya kimatamshi, kimuundo, kimsamiati, kimantiki, kimaumbo na tafsiri sisisi. Kwa upande wa utafiti huu,

makosa yaliyochunguzwa ni ya kimsamiati, kimatamshi, kimiundo na kimaana tu. Nafees (2018) alifuata mkondo wa Idarus akishughulikia makosa ya mara kwa mara kwenye mawasiliano. Kwa mujibu wake, baadhi ya makosa ya kisarufi na mengine yanayofanywa mara kwa mara kwenye mawasiliano ni matumizi mabaya ya njeo, uteuzi mbaya wa msamiati, kukosea matumizi ya umoja na wingi katika vitenzi nya Kiingereza. Makosa mengine ni ya tahajia, toni na muundo. Nafees (ameshatajwa) anasema kuwa makosa hayo husababishwa na kutojua vema maana ya maneno, kuchanganya maana, kuongea harakaharaka. Pia, athari ya lugha mama yaweza kusababisha matamshi mabaya katika lugha nyingine. Bila kuwa mbali na Idarus na Nafees, Wangari (2019), anataja kuwa tatizo la msamiati, makosa ya kimaksudi, hali ya kiakili wakati mtu anapokuwa anatumia lugha, kutoelewa kanuni na ujumlishaji wa kanuni za lugha, na makosa ya kimantiki ni sababu za makosa ya lugha katika Kiswahili. Tafiti hizi kwa ujumla zilimsaidia mtafiti kufahamu kwa undani baadhi ya makosa ya kisarufi yanayofanywa mara kwa mara na watumiaji wa lugha duniani. Zaidi, zilimsaidia kujua sababu za makosa hayo. Hivyo basi, mtafiti aliongozwa na maarifa hayo kuchunguza kwa makini matini za habari katika vyombo nya habari vilivyoteuliwa ili kujua ni makosa ya kisarufi yapi hufanyika na kwa nini nayafanyika.

2.2 Makosa ya Lugha na Makosa ya Kisarufi kwenye Vyombo nya Habari

Makosa ya lugha na makosa ya kisarufi katika mawasiliano ya watumiaji wa lugha kama ilivyooneshwa kwenye vipengele vilivyotangulia, huendelea kufanywa kwenye habari za kila siku kupitia vyombo nya habari. Katika kipengele hiki, tunajadili tafiti na maandiko mengine yaliyoeleza makosa ya lugha na makosa ya kisarufi kwenye vyombo nya habari nya Kiswahili na lugha zingine.

2.2.1 Makosa ya Lugha na Makosa ya Kisarufi kwenye Vyombo vyat Habari

Vinavyotumia Lugha Zingine

Rowan (2003) anaripoti kwamba katika tafiti ambazo zimefanywa miaka ya 1970-1980 kuhusu habari zinazoripoti taarifa za masuala ya sayansi katika vyombo vyat habari, zilikutwa na makosa ya udondoshaji na kutokuelewka kwa uwazi. Kwa upande wa tafiti za Isani (2011) na Hassoon (2016), zinabaini kwamba habari za magazetini, hasa vichwa vyat habari hukiuka sheria na kanuni za kisarufi katika uandishi wa habari zake. Kutokana na ukiukwaji huo, waandishi wa magazeti hufanya makosa ya udondoshaji wa vibainishi, unominishaji, matumizi ya njeo ya wakati uliopo, matumizi ya kitensi ‘kuwa’, matumizi ya viunganishi, matumizi ya sitiari, matumizi ya maneno ambayo hayatumiki tena au kwa wingi, finyazo, vifupisho, maneno ya mtaani, kutumia kauli tendwa pale ambapo kauli tendi ingetumika. Hivyo, tafiti za wataalamu hao zilimsaidia mtafiti kuyaelewa makosa yanayofanyika katika magazeti na vyombo vingine vyat habari ijapokuwa utafiti huu ulijikita kwenye taarifa za habari zinazotolewa katika televisheni, ambapo kwa mujibu wa wanahabari na wanaismu, taarifa ya habari huwasilishwa kwa lugha rasmi na fasaha (Getyngo, 1997; van Dijk, 1988).

Nchini Marekani, watu hupata habari kwa wingi kupitia mitandaoni. Utafiti wa Cassidy (2007) unaonesha kuwa Wamarekani milioni 50 hupata habari kupitia mitandaoni kwa siku. Chama cha Magazeti cha Amerika kiliripoti kwamba, watu wapatao milioni 112 ndani ya robo ya mwaka 2006 walitembelea tovuti za habari, ambapo 24% ya Wamarekani walisema kuwa tovuti ni vyanzo vyao vikuu vyat habari, wakati 44% yao walisema hupata habari kutoka mtandaoni angalau mara

moja kwa wiki. Kulingana na Cassidy (2007:483), tafiti kadhaa zimeonesha kuwa kumekuwapo na makosa yanayofanywa yakiwamo ya lugha na kisarufi katika habari za mitandaoni. Kutokana na makosa hayo, habari hizo zimeongeza upotofu wa taarifa katika habari zao, jambo ambalo lilifanya habari hizo kutokuaminika kwa watu. Utafiti wa Cassidy (ameshatajwa) ulikuwa muhimu katika utafiti huu kwani ulisaidia kutoa sura halisi ya habari za mtandaoni na jinsi watu wanavyozifuatilia ikizingatiwa kuwa utafiti huu ulishughulikia habari za kutangazwa kwa mdomo na zilizoandikwa katika tovuti za vyombo tafitiwa.

Kulingana na Conboy (2003), magazeti ya udaku nchini Uingereza hutumia lugha yenye makosa kadhaa, hasahaha ya lugha za mitaani na simo. Maelezo ya Canboy (ameshatajwa) yanaakisiwa na Mozūraitytē (2015) ambaye utafiti wake ulionesha kuwa gazeti la The Telegraph la Uingereza hutumia lugha yenye makosa ya kisarufi. Miongoni mwa makosa aliyotaja ni udondoshaji wa maneno, matumizi ya maneno mafupi bila sababu na unominishaji. Matokeo ya tafiti za wataalamu hawa yalimsaidia mtafiti kuelewa hali halisi ya makosa yanayofanywa katika magazeti ya Uingereza. Jambo ambalo lilimsaidia kumjenga katika utafiti wake kwa kulinganisha na vyombo vya habari vya Tanzania.

Moschonas (2014) anasema kuwa katika vyombo vya habari vya binafsi nchini Ugiriki, kumesheheni makosa mbalimbali yanayoharibu lugha. Uharibifu huo hufanyika hasa katika matamshi na ukiushi wa kanuni za lugha. Anahitimisha kuwa televisheni zina athari kwa kiwango kikubwa katika kubadili lugha kwa kwao, huo ni mtindo wao wa lugha na hujaribu kuulinda. Maoni ya Moschonas (ameshatajwa) yalikuwa na mchangano muhimu kwa utafiti huu kwani yalisaidia

mtafiti kuchunguza lugha inayotumiwa na vyombo tafitiwa kama ina makosa ya kisarufi au la.

Katika nchi za ukanda wa Ulaya ya Kaskazini, nako kumethibitika kuwapo na makosa ya lugha katika vyombo nya habari nya nchi hizo. Kwenye nchi ya Norwe, Wanorwe hawapendezwi na mabadiliko yanayoharibu sarufi ya lugha yao. Wamekuwa wakikosoa na kulalamikia magazeti na vyombo nya utagazaji juu ya kutangaza kwa lugha inayobadili sarufi ya lugha yao waliyozoea. Roksvold (2010) anasema kuwa watu wanaokosoa lugha ya magazeti wanajikita katika msingi wa sarufi. Wanasema kuwa lugha ya magazetini inapaswa kuwa sahihi: vitamatishi, viunganishi, uhusika na othografia ya lugha yao inapaswa kubaki kama ilivyo siku zote. Lugha ya utangazaji pia imekosolewa kwa upande wa matamshi. Kwao, lugha ikibaki imara ni jambo zuri. Kwa upande wa wasomaji wa magazeti wanadai kwamba lugha inayotumika miaka ya hivi karibuni katika magazeti imedumaza ubora wa magazeti ikilinganishwa na miaka ya nyuma ya 1990. Kwa hiyo, wao wanaona makosa ya lugha ndiyo yanayoharibu ubora wa magazeti hayo (Roksvold, 2010:110). Kwa upande wa Uswidi, Karlsson, Clerwall na Nord (2016) wanadai kuwa, uandishi wa habari za mtandaoni ni wa haraka sana ila wenye makosa ya kila aina lakini moja ya sifa zake ni kurekebisha makosa na kuwajulisha wasomaji wake juu ya marekebisho hayo. Lengo la utafiti wao lilikuwa ni kuchunguza mapokeo au mitazamo ya raia wa Uswidi juu ya makosa na urekebishaji wake katika uandishi wa habari za mtandaoni. Matokeo ya utafiti wao yanaonesha kwamba, zaidi ya 60% ya raia walikuwa na mtazamo hasi juu ya makosa yanayofanyika katika habari za mitandaoni, 23% walikuwa na matazamo chanya, hali 2% walisema yanavumilika.

Kwa upande wa usahihishaji wa makosa hayo, watafitiwa 66% walikuwa na mtazamo chanya wa kuafiki makosa madogo yaliyosahihishwa. Hata hivyo, 74% walipinga vikali usahihishaji wa makosa ya kiwango cha hali ya juu kwa sababu kwamba kusahihisha makosa pekee hakutoshi bali aina ya makosa yanayofanywa. Wanasema ni bora makosa kurekebishwa kabla ya habari kuchapishwa na si baada ya kuchapishwa. Tafiti hizi zilimsaidia mtafiti kuelewa jinsi ambavyo katika nchi za Ulaya Kaskazini, raia hawapendezwi na makosa ya lugha yanayojitokeza katika utoaji wa habari. Hivyo, mtafiti alichunguza jinsi wasomaji na wasilikizaji wa vyombo vyatuhusu ya habari nchini Tanzania wanavyoyachukulia makosa ya kisarufi yanayojitokeza kwenye habari.

Aditya na Amita (2017) walitafiti juu ya vitofautishi vyatuhusu ya kiisimu katika vichwa vyatuhusu ya habari na kugundua kuwa vichwa vyatuhusu ya magazeti ya India vilisheheni masuala ya udondoshaji wa vibainishi, uambatanishaji, matumizi ya nambari, vifupisho, matumizi ya maneno yasiyo sahihi, ufupishaji kienyeji, uchanganyaji misimbo, utata, uafikishaji, utumiaji wa herufi kubwa usio lazima, maneno magumu, homofoni, ukiushi wa sarufi, udondoshaji wa vitenzi na viima na kufanya vichwa hivyo vyatuhusu ya habari kuwa na makosa ya lugha. Watafiti hao wanasisitiza kuwa makosa hayo yanayopaswa kuepukwa wakati waandishi wanapoandika, vinginevyo watabananga lugha. Aidha kwa mujibu wa Ranasuriya (2015), wasailiwa wengi aliowahoji nchini Sirilanka, walipinga matumizi ya maneno ya Kiingereza katika redio za masafa ya FM zinazotangaza kwa lugha ya Sinhala. Hata hivyo, watangazaji walikiri kutumia lugha ya Sinhala yenye lafudhi ya Kiingereza. Mbali na hilo, wasailiwa walisema kuwa baadhi ya redio hutumia maneno mengi ya Kiingereza kuliko Kisinhala na hivyo walilalamika kwamba ni makosa na ni kuharibu lugha yao.

Nchini Naijeria, Ayodele (1988) alichunguza matumizi mabaya ya kibainishi ‘the’ katika magazeti na kubainisha kwamba katika makala 78 kutoka kwenye magazeti saba, makosa ya matumizi ya kibainishi hicho yalifanyika. Gazeti la National Concord lilifanya makosa 78, gazeti la New Nigerian lilifanya makosa 49, wakati gazeti lililofanya makosa machache ni Daily Stars lililokuwa na makosa 2 tu. Kwa mujibu wa utafiti huo, vyanzo vya makosa hayo ni uhamishaji wa sheria za lugha au athari za lugha mama na umilisi hafifu wa isimu. Omoera (2008a, 2008b) anabainisha kuwa magazeti na televisheni za Naijeria hufanya makosa ya matamshi, lugha isiyo rasmi, msamiati usiofaa, utotolojia, uziada, uundaji wa maneno isivytakiwa, kihuishi kisicho sahihi, upatanisho, kutumia vipashio vya umiliki visivyo sahihi, kujundia maneno yasiyokuwa ya Kiingereza, maneno yasiyowiana, utenzishaji, tahajia n.k. Makosa hayo husabishwa na kutomudu sarufi, ukosefu wa wanahabari waliofuzu, uzembe wa kuhariri kwa umakini. Omoera (2008b) anatoa ushauri kwa vyombo vyote vya habari nchini humo kwamba vinapaswa kutoa habari zake bila kukiuka na kuvunja sheria za sarufi ya Kiingereza hasa katika matangazo rasmi. Hivyo, vyombo vya habari vinapaswa kuwahimiza wafanyakazi wake kutumia lugha fasaha, kuwatafutia mafunzo ili waimarishe ujuzi wa kanuni za lugha (Omoera, 2008a). Pia, Gowon (2009) anakiri kuwapo kwa makosa ya kisarufi kwenye televisheni na redio za Naijeria. Gowon (ameshatajwa), analaumu vyombo vya habari kwamba kutokana na aina ya lugha inayotumika katika matangazo na kuyafikisha kwa wananchi huathiri pakubwa wanafunzi na watumiaji wa Kiingereza nchini Naijeria. Madai ya Gowon (2009:93-94) ni kwamba vyombo vya habari huandaa programu mbalimbali na kuzipeleka kwa wananchi pasi kujali kanuni na sheria za lugha, muktadha na maana. Hivyo, anahitimisha kwa kusema kuwa hali

hiyo huibua kizazi cha watu, hasa watoto wasioweza kuwasiliana na kujieleza kwa ufasaha kutokana na kutomudu lugha vema kwa sababu ya kuathiriwa na lugha inayotumika kwenye vyombo hivyo. Oryila na Umar (2016) walibaini kuwa matangazo ya biashara yaliyotolewa kwenye magazeti nchini Naijeria yalitumia baadhi ya maneno magumu, yasiyoelewka, yenye uvuliuvuli na utata kwa wasomaji wake. Uvuliuvuli na utata wa maneno hayo ulisababishwa na matatizo ya kisarufi, matumizi ya maneno isivyotakiwa, matumizi ya vifupisho ambavyo havijulikani katika lugha ya wenyiji. Matumizi ya maneno hayo hutokana na watangazaji kutokuwa na welewa, kukosea bila kukusudia, matumizi ya tafsida na upanuzi wa maaana ili kukidhi matakwa ya mtoa tangazo. Hivyo, maneno hayo huchangia upotoshaji, ufasili wa maana isiyodhamiriwa, kukosa kuelewa kabisa kinachomaanishwa. Pamoja na kwamba tafiti zilizofanyika Naijeria zimetoa taarifa muhimu zilizosaidia utafiti huu lakini zinatofautiana na utafiti huu katika kipengele cha eneo la utafiti. Utafiti huu umefanyikia Tanzania; hivyo, ni imani ya mtafiti kuwa mazingira na sababu za kufanyika kwa makosa zilikuwa tofauti kwa kiwango kikubwa.

Getyngo (1997) alifanya utafiti uliolenga kuchambua mitindo mbalimbali ya Kiingereza inayotumika katika magazeti ya Kenya. Miongoni mwa mitindo inayotumika ni mtindo wa lugha rasmi na sanifu inayofuata kanuni za kisarufi ambao hutumika katika kuripoti habari rasmi. Utafiti huo unakinzana sana na madai ya Mwaura (2015) anapotanabaisha kuwa vyombo vya habari vya Kenya hasa magazeti, hufanya makosa ya lugha katika uandishi wa habari zao. Makosa mengi ni ya kisarufi hasa ya mpangilio mbaya wa sentensi na yale ya kimantiki; makosa ya

uandishi na tahajia. Gazeti la Daily Nations hufanya makosa mengi ya kisarufi na taipografia, tahajia na matumizi ya maneno yasiyostahili. Aidha, makosa hayo husababishwa na uzembe na kutofanya uhariri kwa umakini. Hata hivyo, anakiri kwamba vyombo vya habari havipaswi kuwa na makosa ya lugha kwani, yanakera wasomaji na wasikilizaji huku akitoa mifano ya wasomaji wawili waliomwandikia juu ya makosa hayo. Ushauri wake ni kwamba wasomaji wasisite kuchunguza makosa hayo na wakiyabaini wayaripoti kwao ili wawasadie kuyarekebisha. Tafiti hizo zilichangia pakubwa kusukuma mbele utafiti huu ila utofauti ni kwamba zenyewe zilishughulikia vyombo vya habari vinavyotumia Kiingereza na huu ulichunguza vyombo vya habari vya Kiswahili.

2.2.2 Makosa ya Luga katika Vyombo vya Habari Vinavyotumia Kiswahili

Kwa upande wa vyombo vya habari vinavyotumia Kiswahili, tafiti na maandiko kadha yanaonesha kuwapo kwa makosa yanayosababisha uharibifu wa lugha. Mwansoko (1995) anataja mfano mmoja wa magazeti ya Mzalendo na Mfanyakazi kuwa yamewahi kufanya kosa la kuingiza kiholela istilahi za Kiingereza magazetini wakati zipo za Kiswahili, na yalitumia kikasuku istilahi za vyama na dola tawala. Kulingana na Mwansoko (1995:8), watumiaji wengi wa Kiswahili wanakerwa na hali hiyo katika magazeti ya Kiswahili na kama waandishi wangefanya utafiti wangepata istilahi bora za Kiswahili zinazowakilisha dhana na istilahi za Kiingereza. Hata hivyo, malengo ya Mwansoko, yalikuwa ni kueleza dhima ya vyombo vya habari katika kukuza, kueneza na kusanifisha istilahi na siyo kuchunguza makosa. Makunja (1995) anaelekea kukubaliana na Mwansoko (ameshatajwa) anapotaja kwamba wakati mwingine kuna matumizi mabaya ya msamiati na ukiushi wa sarufi katika

matangazo ya vyombo vya habari. Anashauri kwamba mafunzo ya kuimarisha lugha na sarufi kwa waandishi wa habari yatolewe ili kuepuka hali hiyo. Hata hivyo, Makunja (ameshatajwa) hakuonesha aina za makosa hayo na sababu zake, na hakutaja kwa umahususi vyombo hivyo. Kwa upande wa Idarous (1995) vyombo vya habari vya Tanzania huchangia sana kufanya na kueneza tafsiri za maneno mapya. Hata hivyo, hukabiliwa na matatizo kadha ikiwa ni pamoja na waandishi kutopewa mafunzo ya fani ya tafsiri jambo ambalo husababisha tafsiri zisizo sahihi, zisizoleweka na zinazopotosha maudhui ya matini chanzi. Tatizo lingine ni ujuzi mdogo wa istilahi kwa baadhi ya waandishi. Idarous (1995:52-60) alilenga kueleza masuala ya tafsiri kwenye vyombo vya habari ila siyo kuchunguza makosa ya lugha ya kisarufi. Ponella (1995:54-56) anakubaliana na madai ya Mwansoko (1995) kwa kutolea mfano matumizi mabaya ya lugha ya Kiswahili katika redio kwamba kuna baadhi ya redio husikika zikitumia maneno kama ‘kumchukulia salamu, kumhitajia maisha marefu na anayefanya kazi hospitalini’ badala ya ‘kumsalimia, kumtakia maisha marefu na anayefanya kazi hospitali.’ Vilevile anasema kuna watangazaji ambao hufanya makosa ya kuchanganya lugha, vitenzi au vivumishi katika matangazo yao na hutumia lugha kinyume na usahihi wake. Kama wenzake, Ponella (ameshatajwa) amedokeza tu baadhi ya mifano ya makosa ya lugha katika vyombo vya habari vya Kiswahili pasipo kuzama kwa kina na kuwa mahususi kwa vyombo husika kama utafiti huu ulivyofanya. Hii ni kwa sababu andiko lake lililenga kueleza matumizi ya Kiswahili katika kanda ya nchi zitumiazo Kiswahili. Kwa mtazamo wa Massamba (1995), ni kwamba mara nyingi kumetokea malalamiko kutoka kwa wasikilizaji wa redio na wasomaji wa magazeti juu ya matumizi mabaya ya Kiswahili lakini bado tatizo hilo halijapatiwa ufumbuzi. Anasema tukijiuliza tatizo

hili linasababishwa na nini tutapata majibu. Hivyo, Massamba (1995: 7-8) anadai kuwa ukiyachunguza kwa makini matatizo ya Kiswahili kwenye vyombo vyahabari utabaini kuwa ni ya aina mbalimbali yakisababishwa na ujuzi kidogo wa lugha ya Kiswahili, kutozingatia fani, kutomakinikia kazi na uhariri dhaifu. Kama waandishi wenzake, Massamba (ameshatajwa) pia hamakinikii vyombo mahususi bali makala yake iligusia matatizo hayo kama sababu ya kukwamisha dhima ya Kiswahili kama lugha ya mawasiliano. Pia, katika andiko lake hachambui wala kutaja matatizo hayo bali lengo lake lilikuwa ni kueleza jinsi Kiswahili kilivyofikia hadhi ya lugha ya mawasiliano.

Utafiti wa King'ei (2000) unatoa matokeo sawa na tafiti zilizolezwa katika aya iliyotangulia kwamba, kuna matatizo ya matumizi ya lugha kwenye vyombo vyahabari vyakisababishwa na nchini Kenya. Matatizo hayo ni kutomudu msamiati vizuri, makosa ya matamshi na tahajia, muundo wa maneno na wiano, wingi na uchache, mpangilio wa maneno kwenye ngeli, tafsiri na utohozi, na matumizi ya sentensi changamano zenyetutata. Utafiti wa King'ei (ameshatajwa) ulishughulikia vyombo vyahabari vyakisababishwa na nchini Kenya. Hata hivyo, utafiti huu ulichunguza vyombo vyahabari vyakisababishwa na nchini Tanzania. Kihore (2004) anaonesha kuwa, magazeti ya Kiswahili ya mitaani Tanzania husheheni matumizi mengi ya maneno ya mkopo kutoka kwenye Kiingereza; hufuata miundo ya lugha ya Kiingereza na hutumia msamiati ambao sisani. Kwa upande wa Shoo (2004), vyombo vyahabari vinavyotumia Kiswahili katika matangazo yake hasa magazeti na redio hutumia baadhi ya maneno ya Kiswahili kimakosa, ikiwemo BBC na DW. Anataja baadhi ya maneno kama ‘denti, teja, uroda, noma, aidha, vinjari na mhanga.’

Utafiti mwingine ulifanywa na Mukhono (2008) kuhusu uarifu katika habari za Kiswahili kwenye vyombo vya habari vya Kenya na kubaini kuwa taarifa nyingi huarifu kwa kiasi kikubwa. Pamoja na hayo, uarifu huo hutingwa na vikwazo vya ukosefu wa upatanisho wa kisarufi, matumizi mabaya ya vihusishi na vitenzi vilivyonyambulishwa, kutumia msamiati usioeleweka kwa wasikilizaji na wasomaji, matumizi ya vivumishi vya idadi isiyo dhahiri na matamshi yasiyosikika vizuri. Aidha, maelezo ya Mukhono (ameshatajwa) kuhusu vikwazo vya uarifu katika habari yanaelekeana na ya Maina (2013, 2014) katika maandiko yake yaliyoshughulikia makosa yanayoharibu lugha katika redio na magazeti ya Tanzania. Kwa mujibu wa maelezo ya Maina (ameshatajwa), vyombo vya habari huharibu lugha kwa kufanya makosa ya kutumia maneno yasiyofaa, kuacha tungo ikielea, upatanisho wa kisarufi, kuacha taarifa muhimu zinazopaswa kusemwa, mantiki, matamshi au lafudhi na uchanganyaji wa maneno ya Kiingereza. Katika habari za kwenye blogu nako kuna makosa. Kulingana na Jagero, Mohochi na Indede (2013), lugha inayotumika sana katika blogu ni ile yenyeye vifupisho visivyo sanifu, uchanganyaji na ubadilishaji misimbo, matumizi mabaya ya lugha, maneno yasiyo sanifu, herufi kubwa na uwakilishi wa lugha ya mazungumzo kwa kutumia ishara mbalimbali.

Onyango na Odawo (2016) pamoja na kwamba wanasifu kuwa watangazaji wa Kenya hujidhatiti kutumia lugha inayoafiki viwango vya sarufi vilivyokubalika; bado wanakiri kwamba makosa mengi yanayohusu msamiati wa Kiswahili yanadhihirika. Wanataja baadhi ya makosa hayo kwa kumnunguu MBAABU (1991) kuwa ni uvurugaji wa ngeli kiholela, matumizi ya tafsiri sisisi au neno kwa neno. Ufafanuzi wa wataalamu hao unaungwa mkono na Mugambi, Mukuthuria na Kobia (2016a, 2016b)

katika tafiti zao zilizoshughulikia makosa ya lugha katika ya redio KBC, idhaa ya Kiswahili na redio Citizen, pamoja na kuchanganua makosa ya msamiati. Kutokana na tafiti hizo, makosa ya kisarufi, kileksika, kitahajia, kisemantiki na kipragmatiki yalipatikana katika habari zilizoandikwa huku katika utafiti mwingine walioufanya mwaka huohuo, makosa 168 ya kileksika yalidhihirika wazi kutoka kwenye habari 37 walizochunguza (Mugambi, 2016b:3023-3027). Kulingana na utafiti huo, makosa ya kisarufi yalitokea mara nyingi, yakifuaatiwa na ya tahajia, ya msamiati, ya kipragmatiki na semantiki. Sababu za makosa hayo ni uharaka wa kutokufanya uhariri wa kina na muda wa kupitia kwa makini maandishi; welewa finyu wa sarufi ya lugha na tafsiri ya moja kwa moja (Mugambi na wenzake, 2016a:179). Utafiti huo ulidhihirisha kwamba makosa ya lugha katika habari yaliharibu na kusababisha ufasiri mbovu wa taarifa zilizotolewa kwa wasilikizaji.

Katika mapitio haya, tafiti nyingi zilizofanyika kuhusu makosa ya lugha katika vyombo vya habari vya Kiswahili zinakiri kwamba, makosa ya lugha yanayofanywa kwenye vyombo hivyo huharibu lugha ya Kiswahili. Hivyo, yanahitajika kutazamwa kwa jicho la karibu sana ili kuweza kuyarekebisha kwa ustawi wa lugha hii. Kutokana na madai yaliyotolewa katika tafiti hizo, na uzoefu ambao umebebwa kwenye maandiko hayo, mtafiti amenufaika na maandiko hayo kwani yalimwongezea maarifa yaliyomwongoza kuchunguza kwa kina makosa ya kisarufi kwenye televisheni za TBC1, ITV na STAR TV ijapokuwa tafiti hizo zilijikita kuchunguza redio, magazeti na blogu.

2.3 Pengo la Utafiti

Kwa upeo wa mtafiti ni kwamba wataalamu wa lugha wamejaribu kuandika juu ya makosa ya lugha katika vyombo vya habari katika maeneo mbalimbali duniani lakini

bado kwa Tanzania, tafiti na maandiko mengi yamejikita zaidi kujadili makosa ya lugha katika magazeti na redio kuliko televisheni hasa zile zinazotumia lugha ya Kiswahili. Kutotoa kipaumbele kwa televisheni, kunatufanya tuamini kuwa bado kuna mambo mengi yanayohusu makosa ya lugha ambayo yanahitaji kuchnguzwa kwa upande wa televisheni ili kupata ufahamu wake. Miongoni mwa mambo hayo, ni makosa ya kisarufi katika televisheni za Tanzania zinazotangaza kwa Kiswahili ambapo hatujafahamishwa kuhusu aina za makosa ya kisarufi yanayotokea katika utoaji wa habari kwenye chaneli za televisheni za Tanzania. Vilevile, hatujafahamishwa sababu za kufanya kwa makosa hayo na hatua zinazopaswa kuchukuliwa ili kuepuka kufanya makosa hayo. Kwa hivyo, ili kuziba pengo hilo, utafiti huu ulijikita kuchunguza na kuchanganua aina za makosa ya kisarufi ambayo yanafanya katika vyombo vya habari vya Tanzania katika chaneli za televisheni. Pia, utafiti ulijikita kuchunguza na kubainisha sababu za kufanya kwa makosa ya kisarufi katika televisheni za Tanzania na hatua zinazopaswa kuchukuliwa ili kuepuka ufanyaji wa makosa ya kisarufi katika utoaji wa habari nchini Tanzania. Zaidi, utafiti huu ulifanya katika chaneli za TBC1, ITV na STAR TV kama kiwakilishi cha televisheni zingine kwa sababu ni sehemu ambayo tafiti tangulizi hazijapapa kipaumbele kama ilivyo kwenye redio na magazeti.

Hivyo, kuchanganua makosa ya kisarufi katika televisheni za TBC1, ITV na STAR TV kutatoa taswira mpya ya makosa ya lugha yanayoharibu ufasaha wa Kiswahili. Pia, utafiti huu umefaulu kubainisha makosa ya kisarufi ya Kiswahili tofauti na tafiti zilizochunguza makosa ya lugha au ya kisarufi katika lugha kama Kiingereza, Kisinhala na Kigiriki. Jambo mbalo halikupewa kipaumbele katika tafiti zilizotangulia.

2.4 Kiunzi cha Nadharia

Utafiti huu uliongozwa na viunzi viwili vya nadharia. Viunzi hivyo ni Uchanganuzi wa Habari Kisarufi (UHK) na Uchanganuzi Makosa (UM) katika kukusanya data, kuzichambua na kuwasilisha matokeo ya utafiti.

2.4.1 Kiunzi cha UHK

Hiki ni kiunzi kinachojenga Nadharia ya Uchanganuzi wa Habari kama Usemi/Matini (NUHU/M) (*The Analysis of News as Discourse*) iliyoasisiwa na Teun A. van Dijk (1988). Katika kitabu chake cha *New Analysis* (1988), van Dijk kama mtaalamu wa isimu na habari alianzisha kiunzi cha UHK ambacho kwa Kiingereza alikiita “Grammatical Analysis.” Lengo lake lilikuwa ni kufafanua jinsi habari inavyoweza kuchanganuliwa kwa mtazamo wa kisarufi. Kwenye kitabu hicho, van Dijk (10-12) anasema kuwa katika mtazamo wa kimuundo, uchanganuzi wa lugha kidhanifu husaidia kufanya utofauti katika viwango mbalimbali vya usemi/matini. Katika uzalishaji na ufhamu halisi wa watumiaji wa lugha, viwango hivyo vyaweza kuchakatwa zaidi au kidogo kwa wakati mmoja au kutumiwa kwa utaratibu maalumu kwa njia mbalimbali ili kupata taarifa nyingi iwezekanavyo kutoka kila kiwango. Sehemu ya viwango hivyo vya usemi/matini hufasiliwa na wanaisimu kuwa ni mifumo ya kanuni na kategoria za uchanganuzi dhanifu wa sauti, maneno, miundo ya sentensi na maana zake. Kwa mtindo huo, tunapata uchanganuzi wa kifonolojia, kimofolojia, kisintaksia na kisemantiki wa sentensi. Katika sarufi usemi/matini, uchanganuzi wa miandamo ya sentensi kwa mujibu wa van Dijk (1988) ni muhimu kwa sababu, vipashio katika muundo wa sentensi (mf: mpangilio wa maneno) au vya maana ya sentensi vyaweza kutegemea vipashio vya muundo wa

sentensi nyingine katika usemi/matini. Mathalani, kiwakilishi ‘*yeye*’ katika matini chawenza kuwa sawia katika matumizi yake endapo kitakuwa kinarejelea mtu ambaye ndani ya matini hiyo alishatangulia kutajwa. Kwa mfano, ‘*babu alipokuwa akitembea barabarani alikuwa akiangalia huku na kule kama kuna kitu anakitafuta. Watu wengi walimshangaa ila yeye hakushutushwa na jambo hilo.*’ Katika matini hii, kiwakilishi *yeye* kilivyotumika kinaonesha kuwa kinahusiana na nomino *babu* ambayo ilitangulia kuelezwaa katika sentensi ya kwanza. Kwa hiyo, kulingana na van Dijk, ni wajibu wa mwanaisimu kuhakikisha anafafanua muundo wa namna hiyo kwa misingi ya kinadharia juu ya uwezekano wa miundo ya kisarufi ya namna hiyo katika lugha mahususi za binadamu. Katika utafiti huu mtafiti, alisoma na kusikiliza kwa makini matini za habari akizichuja kwa kanuni za kisarufi ili kupima kama miundo ya tungo zake ilikidhi kanuni za sarufi ya Kiswahili.

van Dijk (ameshatajwa) anaendelea kupambanua kuwa lengo la uchanganuzi wa usemi/matini katika ripoti za habari si tu kuzingatia uwezekano ila kuzingatia miundo halisi ya kisarufi au iliyokubaliwa ambayo hufasili utumiaji wa lugha katika muundo wa usemi/matini. Hii humaanisha kuwa matini za habari hulinganishwa na matumizi ya lugha katika matini au miktadha mingine ambayo hudhihirisha tofauti za muundo wa sarufi katika muktadha tofauti. Ni katika mkondo huo huibuka mtazamo wa kimtindo, yaani utumiaji wa lugha kwa mtindo fulani kulingana na usemi/matini husika. Hata hivyo, kwa mujibu wa van Dijk, katika hali rasmi na lugha andishi huwa tunatumia maneno sanifu, changamano, yaliyokamilika, na sentensi zenye muundo sahihi wa kisarufi kuliko ilivyo kwenye mawasiliano yasiyo rasmi. Mhimili huu ulikuwa msingi mkubwa wa utafiti huu. Ili kubainisha makosa kwenye

matumizi yoyote ya lugha, ni lazima mtafiti achunguze na kuhakikisha kuwa miundo ya sentensi zinazounda usemi/matini fulani ni sahihi kwa mujibu wa kanuni za sarufi ya lugha husika. Katika utafiti huu, mtafiti alisoma na kusikiliza habari huku akihakiki kama miundo yake ilitumia maneno sanifu na sahihi, sentensi kamilifu na miundo inayokubalika katika sarufi ya Kiswahili.

Vilevile, katika vyombo vya habari makini, ripoti za habari zao hujengwa na sentensi ndefu na changamano, unominishaji na istilahi rasmi zilizoazimwa kutoka kwa wanasiaya (van Dijk, 1988:11). van Dijk (ameshatajwa) anaendelea kufafanua kuwa wakati mwingine, ripoti za habari hudhihirisha miundo ambayo ni nadra kuwa katika aina nyingine za matini, kama muundo wa sentensi arifu pindu. Uchanganuzi wa kisarufi wa matumizi ya lugha katika vyombo vya habari unaweza kudhihirisha pia msimamo/mtazamo wa mwandishi au gazeti. Mpangilio wa sentensi hufafanua uamilifu wa kisemantiki wa vijenzi vyake kuhusu jambo kutopteka na mpangilio wa maneno, uhusiano kiuamilifu (kiima, kiarifu) au matumizi ya kauli tendi na tendwa. Katika utafiti huu, mtafiti alihuisha mpangilio wa vipashio vya tungo na maana zilizodokezwa na sentensi hizo ili kuona kama zinaendana kimantiki au la. Kwa hiyo, mhimili huu ulisaidia kuchunguza makosa ya kisemantiki.

Akifafanua dhana ya usemi/matini kama mfuatano wa sentensi ziletazo ushikamani, van Dijk (1988) anasema kuwa usemi/matini, na hasa ripoti za habari huwa hazijengwi na sentensi pwekepweke. Mbali na mtazamo wa sarufi na isimu mapokeo wa sentensi, miundo mingine ya usemi/matini imedaiwa kuwapo. Kwa hivyo, hatua ya kwanza na ya wazi katika uchambuzi wa namna hiyo ni kuchunguza miandamo ya sentensi. Hii inamaanisha kuwa, kati ya mambo mengine, muundo au maana za

sentensi katika usemi hutambuliwa kwa njia ya miundo na tafsiri za mazingira, ambayo hutangulia sentensi katika fungu matini moja. Mpangilio na kazi ya maneno au uamilifu kisemantiki unaoambatana nayo hutegemea muktadha wa usemi huo (akimnukuu, Givón, 1979). Ila kwa maneno mengine ni kwamba, si kila mara maana na mawazo ya usemi/matini idhihirishwe tu na mpangilio wa kisintaksia wa sentensi bali, vishiriki/vijenzi viambatanavyo na sentensi hiyo kwenye matini. Kwa hiyo, vijenzi hivyo vinavyoshirikiana kujenga ushikamani wa kisemantiki huitwa vipashio vya ushikamani (akiwanukuu Halliday & Hasan, 1976). Zipo kanuni na taratibu zinazoleta ushikamani, na ni muhumu kuchunguza kama ripoti za habari kwa ujumla au habari maalumu zimetumia au zimekiuka kanuni hizo. Katika utafiti huu, mtafiti alichunguza kama kanuni za ushikamani, mfano matumizi ya viunganishi, urejeleaji na vipashio vya upatanisho vimetumika katika kuripoti habari ili kujenga mantiki na maana inayoleweka kwa wasilikizaji na wasomaji. Mhimili huu ulisaidia kutambua makosa ya kisemantiki kama anavyosema van Dijk (1988:12) kuwa katika kiwango cha semantiki, uchambuzi wa usemi/matini kama mwambatano wa sentensi hutoa msingi wa tafsiri yakini. Maana au urejeleaji wa maneno, vishazi au sentensi huchunguzwa kutokana na sentensi tangulizi. Hivyo, kwa mtazamo huo, maana ya sentensi katika matini itategemea ushikamani ambapo sentensi huungana na nyingine kwa mtiririko maalumu ili kujenga tukio.

Kutokana na kiunzi hiki, mtafiti aliona kinafaa kuchunguza matini za habari ambazo ziliteuliwa. Wakati wa usomaji na usikilizaji wa habari za televisheni, mtafiti alitumia maarifa ya kiunzi hiki kuhakiki habari na kuzipima kwa kuzingatia mihimili iliyofafanuliwa hali kutokana na upimaji huo, alibaini makosa ya kisarufi

yaliyofanywa ndani ya matini hizo. Nadharia hii ilimsaidia mtafiti kupata data zilizohitajika kwa kutumia kanuni za kisarufi wakati wa kuchunguza habari. Hata hivyo, utafiti huu si wa kwanza kutumia kiunzi hiki kuchunguza makosa ya lugha bali watafiti wengine kama Akbari na Kheirabadi (2015) walikitumia kuchunguza makosa ya kiisimu katika vyombo vya habari na walipata matokeo sahihi. Hivyo, kilikuwa kiunzi mwafaka kwa utafiti huu. Pamoja na hayo, udhaifu wa nadharia hii ni kwamba inaishia katika kuchambua habari na kubaini makosa ya kisarufi tu. Haiwezi kumsaidia mtafiti kwenda mbele zadi kuweza kuchanganua makosa hatua kwa hatua na kisha kueleza kiwango na sababu za utokeaji wa makosa hayo katika matini. Kutokana na udhaifu huo, mtafiti aliona ni vema kuhusisha nadharia ya UM.

2.4.2 Kiunzi cha Nadharia ya UM

UM ni nadharia iliyoasisiwa na mwanaisimu wa Kiingereza, Stephen Pit Corder, mnamo 1967 katika andiko lake la *The Significance of Learner's Errors*. Nadharia hii iliibuka kama mbadala wa nadharia ya ulinganishaji na ulinganuzi wa makosa (contrastive analysis) iliyokuwa ikitumika kuchunguza makosa yaliyofanywa na wajifunzaji wa lugha ya pili. Katika andiko lake, Corder (1967) anaona kuwa kuliko kuchukulia makosa kama jambo bayo linalotakiwa kurekebishwa/kudhibitiwa na walimu, bora yatazamwe kwa faida na kwa umuhimu wake yenyewe katika mchakato wa kujifunza lugha ya pili. Hii ni kwa sababu makosa hayo hutoa mwanga na uwezo wa mjifunzaji lugha ya pili. Hivyo, yasichukuliwe kama ni matokeo ya ukosefu wa usahihi.

Baadaye, nadharia hii iliendelezwa na wanaisimu kadhaa ambapo miongoni mwao ni Gass na Selinker (2008). Kwa mujibu wa Gass na Selinker (2008:102), UM ni aina

ya uchambuzi wa kiisimu unaoshughulikia makosa yafanywayo na wanaojifunza lugha. Katika mchakato wa uchanganuzi makosa, Grass na Selinker (wameshatajwa) wanapendekeza hatua sita za kufuata ambazo ni:

- a) Kukusanya data – japo hii hufanywa kwa data za maandishi lakini pia hata mazungumzo inawezekana.
- b) Kutambua makosa – makosa ni yapi? (mf: matumizi mabaya ya nyakati, miundo mibaya ya vitenzi, makosa ya umoja na wingi n.k).
- c) Kuainisha makosa – ni makosa ya kundi lipi (makosa ya upatanisho au miundo mibaya?)
- d) Kuonesha mdafao wa makosa. Makosa ya upatanisho yametokea mara ngapi?
- e) Kufafanua vyanzo vyakosa.
- f) Kusahihisha makosa hayo kwa hatua za kipedagogi zaidi.

Katika utafiti huu, mtafiti alifuata hatua tano muhimu (isipokuwa (d)) zilizopendekezwa na Grass na Selinker (wameshatajwa) katika uchambuzi na uchanganuzi wa data. Japokuwa UM ni nadharia iliyoasisiwa kwa lengo la kushughulikia makosa ya wajifunza lugha, kwa mtazamo wa mtafiti inafaa pia kuchanganua makosa yanayofaywa na wajuzi wa lugha au wasemaji wa lugha asilia katika mawasiliano yao. Kipengele ambacho kinafaa zaidi katika uchanganuzi wa makosa ni zile hatua zilizopendekezwa na Gass na Selinkar (2008:103). Nadharia hii imetumiwa sana na wachunguzi wa makosa ya lugha kwa wanaojifunza lugha na watafiti wa makosa ya lugha kwenye vyombo vyakosa.

Mugambi na wenzake (2016b) na imekuwa na matokeo mazuri.

Katika utafiti huu, mtafiti alitumia viunzi vyote viwili – yaani UHK na UM katika kukusanya, kuchanganua data na kuwasilisha matokeo. Kiunzi cha UHK kilitumika katika ukusanyaji wa data hasa wakati wa kusoma na kusikiliza matini za habari. Pia, kilisaidia kutoa ufanuzi wa kuthibitisha kuwa data zilizokusanywa zilikuwa kweli ni makosa ya kisarufi kwa kuzingatia mihimili ya kiunzi hicho. Kiunzi cha UM kilitumika zaidi katika uchambuzi na uwasilishaji wa matokeo ya utafiti.

2.5 Muhtasari wa Sura

Sura hii imefafanua vipengele vya dhana za makosa ya lugha na makosa ya kisarufi; makosa ya lugha na makosa ya kisarufi kwa watumiaji wa lugha; makosa ya kisarufi katika vyombo vya habari vinavyotumia lugha zingine; na, makosa ya lugha na makosa ya kisarufi katika vyombo vya habari vya Kiswahili. Vilevile, sura imeeleza pengo la utafiti na viunzi vya nadharia viliviyotumika katika utafiti huu.

SURA YA TATU

MBINU ZA UTAFITI

3.1 Utangulizi

Utafiti huu ulichunguza makosa ya kisarufi katika vyombo vya habari vya Tanzania, umahususi ukiwekwa kwa TBC1, ITV na STAR TV. Hivyo, sura hii inaeleza mbinu zilizotumiwa katika mchakato wa utafiti. Vipengele vinavyofafanuliwa hapa ni eneo la utafiti, sampuli na usampulishaji, mbinu za kukusanya data, mkabala wa uchambuzi na uwasilishaji matokeo ya utafiti.

3.2 Eneo la Utafiti

Eneo katika utafiti hurejelea mwelekeo wa kijiografia na kitaaluma kulingana na asili ya mada yenye (Ponera, 2019). Utafiti huu ulikuwa wa kimaktaba kwa kiwango kikubwa kwani, ulitegemea data nyingi kutoka maktabani ambapo mtafiti alisoma na kusikiliza matini za habari kutoka kwenye vyombo vilivyoteuliwa. Kwa mujibu wa Ponera (2019: 66), zipo tafiti za kimaktaba ambazo hazihusiani na safari ya uwandani. Anaendelea kusema kuwa katika tafiti kama hizi, kipengele cha eneo la utafiti kitaishia katika kueleza eneo la kitaaluma pamoja na eneo la kupata vyanzo vya kimaktaba. Kwa mantiki hiyo, utafiti huu ulifanyikia wilaya ya Kwimba ambapo mtafiti alikusanya data kwa kusoma, kusikiliza na kutazama taarifa za habari za chaneli zilizotafitiwa. Maana yake ni kwamba, mtafiti alitazama televisheni na kusoma habari zilizoandikwa katika tovuvi za TBC1, ITV na STAR TV. Kwa upande wa data zilizohitajika kutoka kwa watafitiwa, mtafiti alizikusanya kutoka kwa hadhira wanaoishi katika wilaya ya Kwimba na wanahabari ambao wanafanya kazi kwenye vituo vya TBC1 na ITV vya Dar es Salaam, na STAR TV cha Mwanza.

Data zilichunguzwa kwa misingi ya kisarufi, na hivyo utafiti umejikita kwenye taaluma ya habari na sarufi.

3.3 Wango la Utafiti/ Watafitiwa

Kwa mujibu wa Ponera (2019:66), wango la utafiti ni jumla ya watu au vitu vyote vinavyofaa kutafitiwa kadiri ya mwelekeo wa mada ya utafiti husika. Hivyo, wango la utafiti huu lilikuwa ni vyombo vya habari vya Tanzania na hadhira ya vyombo hivyo. Hii ni kwa sababu mada iliyotafitiwa inahusu habari zinazotolewa na vyombo hivyo. Vyombo vya habari hutoa habari kwa hadhira (wasikilizaji/watazamaji na wasomaji). Utafiti huu ulitumia kundi la hadhira ya televisheni zilizoteuliwa wenye maarifa ya masuala ya lugha na sarufi pamoja na wanahabari wa vyombo vilivyoteuliwa kutafitiwa

3.4 Sampuli na Usampulishaji

3.4.1 Sampuli ya Utafiti

Sampuli ni sehemu ya wango ambayo imeteuliwa ili kusaka majibu ya tatizo la utafiti (Kothari, 2009 na Dawson, 2002 wakinukuliwa na Ponera, 2019: 67). Hivyo, sampuli katika utafiti ni idadi fulani ya watafitiwa walioteuliwa na mtafiti kutoka kwenye wango kwa ajili ya kuchunguzwa. Utafiti ulikuwa na sampuli za aina tatu: Vyombo vya habari, wanahabri na hadhira.

Idadi ya vyombo vilivyoteuliwa ni chaneli tatu (3) za televisheni ambazo ni TBC1, ITV na STAR TV kutoka kwenye chaneli kumi (10) zinazotazamwa na hadhira katika maeneo mengi ya Tanzania kwa mujibu wa utafiti wa MOMT (2018).

Jedwali 3.1: Wango la Chaneli na Sampuli yake

Chaneli Lengwa	Sampuli Iliyotafitiwa
Azam Two	
Channel Ten	Star TV
Clouds TV	
East Africa TV	TBC1
ITV	
Star TV	ITV
TBC1	
TBC2	
TVE	
TV1	

Kwa mujibu wa jedwali 3.1, mtafiti aliteua chaneli tatu kibahati nasibu kutoka kwenye wango la chaneli kumi ambazo ziliteuliwa kwa kigezo cha kufuatiliwa na hadhira wengi kuliko chaneli zingine katika maeneo mengi ya Tanzania. Kwa sababu hiyo, makosa ya lugha mbayo yanafanyika kwenye chaneli hizo yanasantaa haraka na kuenea kwa hadhira katika maeneo mengi kuliko chaneli ambazo si za kitaifa. Kwa kuzingatia kanuni ya uwakilishi wa asilimia 10 – 30, chaneli za TBC1, ITV na STAR TV ziliteuliwa kama sampuli. Aidha, kutoka kwenye televisheni hizo, jumla ya matini 105 za habari zilikuwa vyanzo vyta data za utafiti huu. Jedwali lifuatalo linaonesha kwa muhtasari sampuli ya chaneli na matini za habari zilizotafitiwa.

Jedwali 3.2: Idadi ya Matini za Habari

Chombo cha Habari	Matini za Habari		Jumla
	Za Tovutini	Za Runingani	
TBC1	30	05	35
ITV	30	05	35
STAR TV	30	05	35
Jumla Kuu	90	15	105

Kulingana na jedwali 3.2, mtafiti alisoma matini 90 za habari kutoka kwenye vyombo teule, ikiwa ni sawa na matini 30 kutoka kila chaneli. Vilevile, mtafiti alitazama na kusilikiza vipindi 15 vya taarifa za habari, ikiwa ni sawa na jumla ya vipindi 5 kwa kila chaneli.

Kwa upande wa watafitiwa, hadhira 15 na wanahabari 5 walisailiwa ili kutoa data za utafiti. Idadi hiyo ilipatikana kwa kutokana na mwongozo wa ramani ya idadi ya watafitiwa (Ponera, 2019:75) ambapo mtafiti alilenga kupata data kutoka kwa hadhira wenye ujuzi wa masuala ya lugha na sarufi na wanahabari. Jedwali 3.3 linaonesha kwa muhtasari idadi ya watafitiwa.

Jedwali 3.3: Idadi ya Watafitiwa (Hadhira na Wanahabari)

HADHIRA		WANAHABARI	
Kiwango cha Elimu ya Lugha	Idadi	Chombo Anachofanyia Kazi	Idadi
Astashahda	0	ITV	02
Stashahada	02		
Shahada ya Kwanza	13	TBC1	02
Shahada ya Umahiri	00		
Shahda ya Uzamivu	00	STAR TV	01
JUMLA KUU: 20			

Jedwali 3.3 linaonesha jumla ya watafitiwa 20 ambao wote walikidhi vigezo vilivyozingatiwa kuwateua. Vigezo hivyo ni kuwa na taaluma ya lugha kwa hadhira na taaluma ya habari kwa wanahabari. Jedwali linaonesha kwamba wasailiwa ambao ni hadhira wote walikuwa na elimu ya lugha (isimu) kwa kiwango cha stashahada na shahada ya kwanza. Wasailiwa wa stashahada walikuwa 02 na wa shahada ya kwanza walikuwa 13. Pia, wanahabari waliosailiwa wote walikuwa na taalumua ya habari na walifanya kazi kwenye vyombo vya habari vilivyotafitiwa ambapo idadi iliyoteuliwa ni wanahabari 05.

3.4.2 Usampulishaji

Usampulishaji kama mbinu ya utafiti, ni mchakato wa uteuzi au uchaguzi wa sampuli kutoka kwenye wango la watafitiwa ili kupata idadi ambayo itachunguzwa na mtafiti kwa ajili ya kutoa data za utafiti zinazohitajika (Kumar, 2011; Pandey na Pandey, 2015). Usampulishaji hutimizwa na mchakato unaohusisha mbinu mbalimbali ili kuweza kupata sampuli faafu. Mtafiti alitumia usampulishaji lengwa kupata sampuli iliyompatia data zilizotakiwa. Mbinu iliyotumiwa na mtafiti kupata idadi ya sampuli ni uchaguzi au uteuzi lengwa. Kulingana na Ponera (2019:7), katika mbinu hii mtafiti huchagua watafitiwa/vitafitiwa kwa kujiegemeza katika kuwapo kwa sifa za kipekee zinazofanya ufaafu na uhusika wao katika utafiti husika kuwa wa kipekee. Kwa msingi huo, sampuli ya utafiti huu iliteuliwa kwa kuzingatia sifa zilizoifanya kuwa lengwa. Mtafiti alizingatia sifa za ueneaji na wingi wa ufuatiliwaji wa channeli za televisheni kutoka kwa hadhira kwa vyombo teuliwa; kiwango cha maarifa ya wasailiwa juu ya data zilizohitajika; pamoja na usasa wa habari na muda wa utafiti.

Uteuzi wa sampuli ya vyombo vyta habari uliongozwa na mbinu ya usampulishaji lengwa. Kwa kuwa makosa ya lugha yanayofanyika kwenye vyombo vyta habari huwa na athari kwa hadhira ya vyombo hivyo, ni muhimu kufanya utafiti wa kurekebisha makosa yanyofanyika kwenye vyombo vyta habari kwa manufaa ya hadhira na ufasaha wa lugha. Utafiti huu ultumia vigezo vyta kuaminika kwa chombo cha habari, wingi wa hadhira wanaofuatilia chombo husika na ufikiaji wa maeneo mengi nchini wa chombo husika. Kwa mujibu wa utafiti wa MOMT (ishatajwa), televisheni ni aina ya chombo cha habari kinachoongoza kwa kuaminiwa

na hadhira kwa habari zake kwa 73% na ni chombo cha habari cha pili baada ya redio kama chanzo cha habari kwa hadhira. Vigezo hivyo vilimwongoza mtafiti kuteua televisheni badala ya magazeti na redio. Kulingana na MOMT (ishatwajwa) chaneli za televisheni 10 za Kiswahili ndizo zinazoongoza kwa kufuatiliwa na hadhira katika maeneo mengi ya Tanzania na zina hadhira kubwa kuliko chaneli zingine, nazo ni (kwa mpangilio wa kialfabeti) Azam Two, Channel Ten, Clouds TV, East Africa TV, ITV, Star TV, TBC1, TBC2, TVE na TV1.

Hata hivyo, mtafiti asingeweza kutafiti chaneli zote hizo kwa muda uliopangwa wa utafiti huu. Hivyo, ili kupata sampuli halisi ambayo ilitafitiwa kama kiwakilishi cha chaneli zilizotajwa, ilibidi kutumia kanuni ya uwakilishi wa asilimia 10 – 30 (Ponera, keshatajwa). Kwa nia ya kupata data ya uhakika na kutosha, mtafiti aliteua asilimia 30 kuwa uwakilishi wa idadi ya sampuli yake. Hivyo, 30% ya chaneli 10 ni chaneli 03. Kwa sababu ya kuepuka uwapo wa mwanya wa upendeleo katika kuteua sampuli, mtafiti aliandika majina ya chaneli kumi katika vikaratasi ambapo kila kikaratasi kilikuwa na jina moja, akavichakata kwa kuvitikisa kwenye kopo na kisha kuvimwaga chini, akamuomba msaidizi wake kuokota vikaratasi vitatu kwa kufumba macho. Baada ya kuokota vikaratasi hivyo, mtafiti alimuomba msaidizi wake asome jina la kila kikaratasi na ndipo yalibainika majina ya chaneli za STAR TV, ITV na TBC1.

Kwa upande wa watafitiwa, usampulishaji lengwa ultumika kwa kuzingatia kigezo cha taaluma ya lugha na habari ili kupata idadi ya wasailiwa 20 (wanahabari na hadhira). Katika utafiti wa kitaamuli, mtafiti hushauriwa kutoweke idadi halisi ya watafitiwa/vitafitiwa kwani kigezo cha utoshelevu wa taarifa zinazohitajika ndicho

kinachoongoza idadi ya sampuli (Lopez na Whitehead, 2013). Hii ni kusema kuwa, mtafiti katika utafiti wa kitaamuli, hupaswa kuweka ramani ya idadi ya watafitiwa itakayomuongoza na si idadi halisi ambapo mtafiti anaweza kuishia katika idadi ambayo anaona imempatia data anazotaka na hakuna taarifa mpya kadiri anavyoendelea kukusanya kutoka kwa watafitiwa (Ponera, keshatajwa). Katika utafiti huu, mtafiti aliongozwa na ramani ya watafitiwa kati ya 10 na 30 kama ambavyo wanamethodolojia wa kitaamuli wanapendekeza. Alianza kukusanya data na alipofikia watafitiwa 20 aligundua kuwa hakukuwa na taarifa mpya ambazo zilitolewa na wasailiwa wake na hivyo kuweka ukomo.

Mbinu ya uchaguzi wa wasailiwa iliyotumika ni ya kuzingatia usampulishaji wa kiutalaamu kama mbinu mojawapo ya usampulishaji lengwa. Usampulishaji huu hutumia mbinu ambayo watafitiwa huchaguliwa kwa njia isiyo nasibu kulingana na utaalamu wao juu ya jambo linalochunguzwa (Bhattacherjee, 2012). Hivyo, wasailiwa walioteuliwa ni wale ambao wana taaluma ya lugha na habari tu. Kwa upande wa hadhira, mtafiti alibaini kuwa eneo sahihi la kupata hadhira yenye taaluma ya lugha kwa urahisi ni kwenye taasisi za shule ambapo kuna walimu walioajiriwa kufundisha masomo ya lugha. Wasailiwa hao, mmojmmoja walipewa hojaji na kuzijaza, ambapo shule tano za sekondari zilitembelewa na mtafiti na kupata idadi ya wasailiwa 15. Hata hivyo, waliota taarifa ni wale tu ambao walikiri kufuatilia matangazo na taarifa za habari za channeli zilizoteuliwa tu. Data kutoka kwa watafitiwa hao zilioana sana na hakukuwa na data mpya ambazo zingemfanya mtafiti aendelee kusaka taarifa na hivyo kuamua kuishia kwa hadhira 15. Kwa upande wa wanahabari, mtafiti aliamua kutafiti wanahabari wa TBC1, ITV na STAR

TV ambao wanaendesha vipindi nya lugha ya Kiswahili ambapo kwa TBC1, kuna *Lulu za Kiswahili*; ITV kuna *Kumepambazuka Kiswahili* na STAR TV kuna *Kamusi ya Mtaa*. Kwa upande wa TBC1 na ITV, walipatikana watangazaji wawiliwaili na kwa STAR TV alipatikana mmoja ambaye ndiye anayeendesha kipindi cha Kamusi ya Mtaa. Jumla wakawa watafitiwa 5 kwa upande wa wanahabari.

Kuhusu idadi ya matini zilizochunguzwa, mtafiti alizingatia ukomo wa muda wa utafiti na usasa wa habari iliyotolewa. Mtafiti alitakiwa kukusanya data kwa muda wa mwezi mmoja. Kwa kufanya hivyo, aliweka ratiba ya kusoma matini mojamoja kutoka kwenye tovuti za channeli zilizoteuliwa kila siku ambapo ni sawa na matini 30 huku akisikiliza na kutazama taarifa ya habari moja ndani ya siku mbili kutoka channeli mojamoja ambapo kwa siku 30 alifanikiwa kusikiliza na kutazama vipindi 15 nya taarifa za habari. Hivyo, mtafiti aliweza kusoma na kutazama/kusilikiza matini 105 za habari kwa muda wa mwezi mmoja tangu 29 Oktoba 2020 hadi 31 Novemba 2020.

3.5 Mbinu za Ukusanyaji wa Data

Data za utafiti huu zilipatikana na kukusanya kwa kutumia mbinu tatu zifuatazo:

3.5.1 Usomaji wa Matini

Mbinu hii ilitumika kupata data kutoka kwenye matini andishi za habari. Mtafiti alifungua tovuti za vyombo tafitiwa (www.tbc.go.tz, www.itvtanzania.co.tz na www.startv.co.tz) na kusoma kwa makini habari mbalimbali zilizochapishwa katika tovuti hizo. Wakati wa usomaji, mtafiti alifuatilia kwa makini usahihi na makosa katika matini hizo kwa kuongozwa na kiunzi cha nadharia cha UHK huku akinukuu makosa ya kisarufi yaliyothibitika. Matini zilizosomwa ni za kati ya mwezi Machi na

Novemba, 2020 (tazama *kiambatanisho* 2). Mbinu hii ni faafu kwa aina ya data zinazotakiwa kwani, ili kupata taarifa za kimaandishi lazima mtafiti asome matini husika. Mbinu hii ilitumika kukusanya data za lengo la kwanza.

3.5.2 Utazamaji na Usikilizaji

Mbinu hii ilitumika kupata data kutoka kwenye matini za habari zilizosomwa na kuwasilishwa kwenye channeli za TBC1, ITV na STAR TV. Mtafiti alilazimika kufuatilia vipindi nya taarifa za habari na kisha kusilikiza na kutazama kwa makini huku akinukuu makosa yaliyojitekeza kwa wasomaji wa habari hizo. Mbinu hii iliteuliwa kwa sababu, kwa aina ya data zilizohitajika ilifaa zaidi kwani, ili kubainisha usahihi au mkosa ya lugha kwa wasemaji ni lazima kuwasikiliza au kuwatazama. Mtafiti alihudhuria vipindi nya taarifa za habari kati ya mwezi Oktoba 29 na Novemba 31, 2020 kwa kuwa taarifa ya habari ya televisheni huwa mbashara kwa muda ambao inasomwa au marudio yake. Vipindi 5 kwa kila televisheni vilitosha kupata data ya makosa ya utamkaji kwa wanahabari. Pia, mbinu hii ilitumika kukusanya data za lengo la kwanza.

3.5.3 Hojaji

Hojaji ni seti ya maswali yaliyoandikwa au kauli zinazohusiana na suala linalotafitiwa ambayo mtafiti hutoa kwa wasailiwa kwa minajili ya kuibua habari, majibu, maoni, mitazamo na mikabala mahususi kuhusu mada ya utafiti (Buliba, Gwachi na Matinde, 2014). Hojaji ni za aina mbili ambazo ni maswali fungo na maswali ya wazi. Katika hojaji ya maswali fungo, mtafiti huandaa maswali yenye machaguo ya majibu ambayo humtaka msailiwa achague jibu analoliona linafaa kutoka katika majibu hayo. Hapa mtafiti humfunga msailiwa ili achague majibu

yaliyoainishwa na mtafiti. Aidha, kwa upande wa hojaji ya maswali ya wazi, mtafiti huandaa maswali yasiyo na majibu na kisha humwachia nafasi msailiwa atoe majibu au maoni kwa mtazamo na lugha yake (Buliba na wenzake, 2014: 91-92). Mtafiti alitumia mbinu hii kukusanya data za msingi kutoka kwa watafitiwa. Kulingana na mada ya utafiti, majibu ya wasailiwa yenyе mtazamo binafsi na ufanuzi wa kina yalifaa kuliko majibu fungo. Hivyo, mtafiti alitumia maswali ya wazi kuwasaili watafitiwa. Hii ni kwa sababu aina ya wasailiwa walioteuliwa ni wale wenye ujuzi wa masuala ya lugha na isimu tu pamoja na wanahabari. Mbinu ya hojaji imeteuliwa kwa kuangalia kigezo cha muda wa utafiti kuwa mfupi hali wasailiwa wenye sifa zilizobainishwa hawapatikani wengi katika eneo moja hivyo si rahisi kuwafikia wote kwa muda mfupi. Kutokana na sababu hiyo, mtafiti alituma hojaji kwa njia ya barua pepe (Kothari, 2004) au mtandao wa Whatsapp kulingana na makubaliano kati ya mtafiti na msailiwa hasa kwa wanahabari ambao walikuwa mbali sana na mtafiti na asingeweza kuwafikia wote kwa haraka kwa muda uliopangwa. Kwa wasailiwa (hadhira) ambao walikuwa maeneo yanayofikiwa kwa haraka na mtafiti (yaani shule) walifuatwa na mtafiti akawapatia hojaji nao kuzijaza. Mbinu ya hojaji ilitumiwa kukusanya data za lengo la pili na la tatu.

3.6 Uchambuzi wa Data na Uwasilishaji wa Matokeo

Data zimechambuliwa na kuwasilishwa kwa mkabala wa kitaamuli. Kulingana na William (2011), data za kitaamuli haziwezi kupimwa na kuhesabiwa kwa usahihi bali hufafanuliwa kwa maneno kuliko takwimu. Isipokuwa data za namna hiyo huwasilishwa kwa njia ya maelezo. Buliba na wenzake (2014: 13) wanasisitiza kwamba kwa asilimia kubwa tafiti zinazohusu lugha, isimu na fasihi ni za

kimaelezo. Kama wanavyosema William, Buliba na wenzake, utafiti huu ulikuwa wa kitaamuli kwa sababu ulishughulikia lugha. Kauli hii inaungwa mkono na Ponera (2019:11) anaposema kwamba mkabala wa kitaamuli hufaa kutumiwa na watafiti wa masuala ya taaluma kama sosholojia, anthropolojia, lugha na mambo mbalimbali yahusuyo utamaduni. Ponera anazidi kusisitiza kwamba utafiti wa kitaamuli ni uchunguzi wa kina wa kisayansi ufanywao kwa kutafakari na kuchanganua jambo maalumu kwa lengo la kupata maarifa.

Kwa kuwa utafiti huu ulichunguza makosa ya kisarufi yanayofanywa kwenye vyombo vyta habari, mkabala wa kitaamuli kwa kutumia mbinu ya maelezo na ufanuzi wa kina, ultumika katika kuchambua data na kuwasilisha matokeo. Baada ya kukusanya data, mtafiti alianza kubainisha makosa ya kisarufi aliyonkuu, kisha akayachambua kwa kina akibainisha ni makosa gani, akayatenga katika makundi, akayafanua kwa mifano, na hatimaye akayasahihisha. Mara baada ya hayo, alieleza kwa mifano thabitii kutokana na data vyanzo vyta makosa hayo na akamalizia kwa kubainisha hatua zilizopendekezwa kuthibiti makosa ya kisarufi katika vyombo vyta habari vyta Tanzania. Uchambuzi umejikita zaidi katika ufasiri wa hali halisi ya data zilizopatikana kutoka katika vyanzo vilivyotafitiwa. Madai haya yanasisitizwa zaidi na Bhattacherjee (2012:133) anaposhauri kuwa uchambuzi wa kitaamuli hutegemea zaidi uwezo wa uchanganuzi na maarifa ya kiutangamano ya mtatifi kutokana na kuelewa vema data zake na hali halisi ya muktadha wa jamii ambamo data hizo zimepatikana.

3.7 Muhtasari wa Sura

Sura hii imefafanua kwa kina mbinu za utafiti ambazo mtafiti alitumia katika kukusanya, kuchambua data pamoja na kuwasilisha matokeo ya utafiti. Kwa maana hiyo, sura imeeleza eneo la utafiti, wango la utafiti, sampuli na mbinu za usampulishaji, mbinu za kukusanya data na mkabala wa uchambuzi na uwasilishaji wa data.

SURA YA NNE

UWASILISHAJI NA UCHAMBUZI WA DATA

4.1 Utangulizi

Sura hii inawasilisha na kuchambua data zilizokusanywa kuhusu malengo ya utafiti. Katika kutimiza azma hiyo, uwasilishaji na uchambuzi wa data ulizingatia malengo matatu ya utafiti. Katika §4.2, data za lengo la kwanza, kwa kujibu swalii la kwanza la utafiti, zimewasilishwa. Hivyo, makosa ya kisarufi katika televisheni za TBC1, ITV na STAR TV yamebainishwa na kuchanganuliwa kulingana na aina zake. Kwenye §4.3, data zinaonesha sababu za makosa ya kisarufi katika vyombo vyaa habari vilivyotafitiwa. Kwa kufanya hivyo, sehemu hiyo ilijibu sawali la pili na kutimiza lengo la pili. Sehemu ya 4.4 imechambua data za lengo la tatu na kujibu swalii lake kwa kufafanua hatua zilizopendekezwa ili kuepuka makosa ya kisarufi katika vyombo vilivyozunguza. Hatimaye, §4.5 imetoa muhtasari wa sura.

4.2 Makosa ya Kisarufi katika Habari za TBC1, ITV na STAR TV

Data zilizokusanywa zinaonesha uwapo wa makosa ya kisarufi kwenye vyombo vyaa habari vilivyotafitiwa. Kwa kuzingatia mihimili ya nadharia, data zilizokusanywa zimewasilishwa kwa kufuata hatua za nadharia ya UM na kuchambuliwa kwa kuzingatia mihimili ya nadharia ya UHK. Maana yake ni kwamba, usomaji na usikilizaji wa matini za habari, ubainishaji wa makosa na ufanuzi wake, umezingatia mihimili ya nadharia ya UHK; matendo ya ubainishaji, uainishaji na uwasilishaji wa data hizo umezingatia hatua muhimu za nadharia ya UM (rejea § 2.4.1 na § 2.4.2). Kulingana na Gass na Selinkar (2008:103), zipo hatua za UM katika lugha. Miongoni mwanzo, hatua ya kwanza hadi ya pili zilizingatiwa na

mtafiti wakati wa mchakato wa ukusanyaji wa data. Hatua hizo ni ukusanyaji wa data na utambuzi wa makosa. Baada ya hatua hizo, hatua zinazofuata ni uainishaji (uchanganuzi) wa makosa na usahihishaji wake. Kwa upande wa data, ukusanyaji ulijikita katika vipengele vitano vya sarufi ya Kiswahili ambavyo ni msamiati, matamshi, maumbo, miundo na maana. Kwa hivyo, data zilibainisha kwamba makosa yaliyofanyika kwenye vyombo vya habari ni ya aina tano. Makosa hayo ni ya kimsamiati, kimatamshi, kimaumbo, kimuundo na kisemantiki (tazama *kiambatanisho.2*).

4.2.1 Makosa ya Kimsamiati

Msamiati ni jumla ya maneno yatumikayo katika lugha (Massamba, 2007:81). Kila lugha ina misamiati yake na utaraibu wa kuzingatia katika utumiaji wa misamiati hiyo. Kiswahili kina utaratibu wa matumizi ya maneno yake pia. Utaratibu huo hupaswa kuzingatia muktadha sahihi wa matumizi, uandishi fasaha na sanifu wa maneno n.k. Kwa mujibu wa nadharia ya UHK, uchambuzi wa habari kisarufi hupaswa kuzingatia kanuni za kila kipengele cha sarufi ya lugha husika (van Dijk 1988:10). Mtafiti alichunguza kwa makini msamiati wa matini zilizotafitiwa na kubaini makosa. Hivyo, makosa ya kimsamiati ni miongoni mwa aina za makosa ya kisarufi yaliyobainika kwenye matini za habari. Hata hivyo, data zilithibitisha kuwapo kwa aina mbalimbali za makosa ya kimsamiati (tazama *kiambatanisho 3*) kama zinavyofafanuliwa hapa chini.

4.2.1.1 Matumizi ya Neno la Kiingereza

Katika matini zilizosomwa, kutazamwa na kusikilizwa, channeli zote (TBC1, ITV na STAR TV) zilisheheni makosa ya kutumia neno la Kiingereza badala ya Kiswahili.

Makosa hayo yalifanyika katika maandishi au matamshi. Jedwali lifuatalo linaonesha mifano ya kosa la matumizi ya neno la Kiingereza.

Jedwali 4.2.1.1: Kosa la Matumizi ya Neno la Kiingereza

Chombo cha Habari	Mifano ya Makosa
TBC1	(a) ... <i>COVID-19</i> ... (b) Mitihani ya <i>Form VI</i> ... (c) Unaweza kuona hiyo <i>gap</i> ...
IVT	(d) ...apiga <i>stop</i> wageni kuingia... (e) <i>Visa zao</i> ... (f) <i>cement</i>
STAR TV	(g) Kuelekea <i>derby</i> hii ya Kariakoo... (h) Matibabu ya <i>Utra Sound</i> (i) Tahadhari dhidi ya <i>COVID-19</i> ...

Jedwali 4.2.1.1 ni mifano inayoonesha wazi kwamba matini zilizotafitiwa katika vyombo husika zilisheheni makosa ya kutumia neno la Kiingereza badala ya neno la Kiswahili. Haya ni makosa kwa sababu habari zililenga hadhira ya Waswahili. Inapotokea dhana ikawa na neno la Kiswahili ila ikawasilishwa kwa lugha ya kigeni, basi hilo ni kosa la kimsamiati. Katika (a) na (i) neno *COVID-19* lenye kirefu cha *Corona Virus Disease-19* lina tafsiri ya Kiswahili ambayo ni UVIKO -19 yaani ‘Ugonjwa wa **Virusi** vya **Korona -19**.’ Aidha, data inaonesha kuwa maneno *form VI, gap, stop, visa, cement, derby* na *ultra sound* yalipaswa kuandikwa kwa tafsiri zake za Kiswahili ambazo ni *kidato cha sita, pengo, marufuku, viza, saruji* na *mchezo wa mahasimu wa jadi*.’ Neno *derby* hutafsiriwa kwa maneno zaidi ya moja kwa sababu, mpaka sasa, katika Kiswahili hakuna tafsiri sanifu zilizoidhinishwa na mamlaka. Pia, wanaisimu wa Kiswahili hawajashughulika na uga huo hasa kufasiri baadhi ya

istilahi zake zisizo na visawe katika Kiswahili. Hivyo, tafsiri maana ya ‘mchezo wa mahasimu wa mji mmoja’ ilifaa kutumiwa. Inawezekana uchumi wa maneno na mtindo wa ufupishaji katika taaluma ya habari ni sababu mojawapo ya kutumia maneno ya lugha nyingine ambayo hayana neno moja kama kisawe cha Kiswahili. Hata hivyo, hiyo si sababu ya msingi kwani kutumia maneno ya lugha za kigeni katika habari za Kiswahili huiacha njia panda hadhira kwa kuwa idadi kubwa ya hadhira ya channeli zilizotaftiwa haielewi lugha za kigeni.

Kosa la utumiaji wa neno la Kiingereza au lugha nyingine za kigeni limedhihirika pia kwenye data zilizokusanywa kutoka kwa wasailiwa (msailiwa [MS]) ambao ndio hadhira ya vyombo vilivyochunguzwa. Walitaja kwa mifano ya maneno ya Kiingereza waliyoshuhudia kwenye vyombo vya habari vilivyotafitiwa.

- (j) Kuchanganya lugha kwa mfano *of course* (MS10)
- (k) Kuandika au kusema *Live* badala ya Mbashara (MS13)
- (l) Kuchanganya lugha ya Kiswahili na lugha ya Kiingereza, mfano; *Unamaind, tunatrend, tuko newsroom, tuko live* n.k (MS15)

Kwa mujibu wa mifano hii, TBC1, ITV na STAR TV hufanya makosa ya kutumia maneno ya lugha za kigeni katika uwasilishaji wa habari. Maneno mengi yaliyothibitika kutumiwa ni ya Kiingereza. Hali hii imesababishwa na athari ya lugha ya Kiingereza kuwa ni lugha yenyewe nguvu na inayozungumzwa maeneo mengi duniani kuliko lugha nyingine kutokana na sababu mbalimbali hasa za kihistoria, kibiashara na kielimu. Ikumbukwe kwamba katika mfumo wa elimu ya Tanzania, Kiingereza ni lugha inayotumika rasmi kimawasiliano kwa ngazi ya sekondari, baadhi ya vyuo vya kati na vyuo vikuu. Kwa hiyo, wanahabari wameathiriwa na Kiingereza kwa namna moja au nyingine. Mifano (j) – (l) imedhihirisha kuwa

wanahabari walitumia *of course* badala ya ‘*bila/pasi shaka*’, *live* badala ya ‘*mbashara*’; *unamaind, tunatrend, newroom* badala ya ‘*unachukia/unakasirika, tunavuma/tunasikika hewani, chumba cha habari.*’ Data hizi zimethibitisha kuwa utumiaji wa maneno ya Kiingereza katika habari za Kiswahili umejitokeza katika sura ya uchanganyaji na uhamishaji wa msimbo (Ng’waje, 2017). Mifano (l) umethibitisha uchanganyaji wa msimbo hali mifano ya (j) – (k) imethibitisha uhamishaji wa msimbo. Hii ni kusema kwamba wanahabari wa vyombo vilivyotafitiwa walifanya kosa la kubadili/kuchanganya msimbo wakati wa kuwasilisha habari zao ilihali dhana walizozieleza zinalezekwa Kiswahili sanifu. Hivyo, usahihi wa makosa hayo ulipaswa kuwa kama:

- (a) ... (UVIKO-19)...
- (b) Mitihani ya kidato cha sita ...
- (c) Unaweza kuona pengo hilo ...
- (d) ... apiga marufuku wageni kuingia ...
- (e) Viza zao ...
- (f) Saruji
- (g) Kuelekea mchezo huo wa mahasimu wa jadi wa Kariakoo...
- (h) Matibabu ya mionzi...
- (i) Tahadhari dhidi ya UVIKO-19
- (j) Bila/pasi shaka
- (k) Mbashara
- (l) Unachukia/unakasirika, tunavuma/tunasikika hewani, chumba cha habari n.k.

4.2.1.2 Matumizi ya Neno Lisilostahili

Kosa lingine la kimsamiati ambalo lilibainika, ni kutumia neno ambalo halikustahili kutumika kwa muktadha husika kulingana na ujumbe ambao ulilengwa. Kwa maoni ya Kemunto na Ontieri (2018) uteuzi wa msamiati usiostahili katika maandishi husababishwa na mtu kuwa na msamiati sahihi ila akashindwa kutofautisha ni msamiati gani mwafaka wa kutumia katika sentensi husika. Hali hiyo humfanya mtu

akanganywe na maneno na kuyatumia vibaya anapajaribu kujieleza (Aruba, 2017).

Utafiti huu ulibaini kuwa kosa la kutumia neno lisilostahili lilifanyika katika vyombo vyaa habari vilivyochunguzwa. Kwa mfano:

Jedwali 4.2.1.2: Kosa la Kutumia Neno Lisilostahili

Chombo cha Habari	Mifano ya Makosa
TBC1	(a) Filamu ambazo <i>ziliuza...</i> (b) <i>Tujaalie</i> yaliyojiri huko Dodoma...
ITV	(c) Watu <i>waliofariki na corona</i> (d) Kuendelea <i>kusalia</i> klabuni hapo ... (e) Kunaweza <i>kupelekea</i> jumuiya nyingine kuondoa vikwazo ...
STAR TV	(f) Waandamanaji Marekani wameendelea <i>kutanda</i> nchini humo ... (g) Hatua za kutoarabiana <i>kwenye</i> umbali wa mita mia moja na kujilinda... (h) ... ameitisha kikao <i>na</i> baraza la ulinzi nchini mwake...

Mifano ya jedwali 4.2.1.2 inathibitisha kwamba matini za habari ziliwu na baadhi ya maneno yasiyostahili. Hapa ieleweke kuwa hayo ni maneno ya Kiswahili ambayo yamesanifiwa ila hayakustahili kutumika kwa sababu hayakuwasilisha ujumbe sahihi uliokusudiwa. Maneno sanifu yanayomaanishwa hapa ni yale yote ambayo yamefuata taratibu za kuidhinishwa na mamlaka kuwa ni maneno ya Kiswahili na yanafaa kutumiwa, yaliyo kwenye kamusi na nyaraka nyingine za mamlaka za usimamizi wa lugha (BAKITA, lishatajwa). Kwa hiyo, utafiti huu unapodai kuwa maneno yaliyobainishwa yalitumika isivyostahili hauna maana ya kuwa hayo si

maneno ya Kiswahili bali kwa muktadha wa habari husika, hayakupaswa kutumika kwa jinsi yaliyotumika.

Katika (a) neno *ziliuza* maana yake haiwiani kabisa na nomino ambayo neno hilo linafafanua. Kimantiki, ‘filamu’ haziwezi kufanya tendo la kuuza. Matendo hayo hufanywa na binadamu. Kwa upande wa (b) neno *tujaalie* halikupaswa kutumika kwani muktadha wa kimantiki wa kifungu hicho cha habari unaonesha kuwa kilicholengwa hapo ni kuarifiwa kwa jambo lililotokea. Sambamaba na hayo, maneno *fariki na, kusalia na pelekea* hayakustahili kutumiwa kwani yanaleta mkanganyiko wa kimaana na kimantiki. Wakati huohuo, neno *tanda* halikupaswa kutumika katika (f) kwani maana yake inavihu vitu na viumbe ambavyo si binadamu kama maji, sisimizi, ndege, wingu n.k. Kwa upande wa (g) – (h) maneno *kwenye na na* hayakustahili kutumika kwa kuwa uwapo wake unaleta utata na kupoteza mantiki ya tungo. Kwa msingi huo, maneno yaliyostahili kutumika ni: (a) *zilizopata soko*, (b) *tujuze/tupashe*, (c) *waliokufa kwa*, (d) *kubaki*, (e) *kusababisha*, (f) *kutandaa*, (g) *kwa*, (h) *cha*. Kwa usahihi, tungo hizo zilipaswa kuwa kama ifuatavyo:

- a) Filamu ambazo zilipata soko...
- b) Tujuze/tupashe yaliyojiri huko Dodoma...
- c) Watu waliokufa kwa korona
- d) Kuendelea kubaki klabuni hapo...
- e) Kunaweza kusababisha jumuiya nyingine kuondoa vikwazo ...
- f) Waandamanaji Marekani wameendelea kutandaa nchini humo
- g) Hatua za kutokaribiana kwa umbali wa mita mia moja na kujilinda...
- h) Ameitisha kikao cha baraza la ulinzi nchini mwake...

4.2.1.3 Kuandika Neno Isivyo

Kuandika neno isivyo ni kuandika neno bila kufuata kanuni au taratibu zilizokubaliwa ili kuwasilisha umbo sahihi la neno kwa kuzingatia tahajia sahihi ya

Kiswahili. Data zilidhahirisha uwapo wa kosa hilo hasa kuvuruga umbo sahihi la neno. Mtafiti alibaini kuwa kosa hili lilihusisha uunganishaji na utenganishaji wa maneno. Kwa mfano:

Jedwali 4.2.1.3.1: Kosa la Kuunganisha Maneno

Chombo cha Habari	Mifano ya Makosa
TBC1	(a) Uzalendo <i>wakweli...</i>
ITV	(b) ... <i>kwasababu...</i> (c) ... <i>inaidadi</i> kubwa ya watu... (d) ... <i>nani</i> shirika la umma ambapo serikali imewekeza...
STAR TV	(e) Mkutano wa SADC ni <i>wakwanza...</i> (f) ... <i>kwasababu</i> ya janga la... (g) ... <i>kwakuwa</i> tayari ameshakamatwa ... (h) ... amesema Wakenya <i>wanajukumu...</i> (i) ... <i>kwahiyo</i> bodi...

Mifano katika jedwali 4.2.1.3.1 inaonesha kuwa matini za habari zilizoandikwa kwenye tovuti za channeli zilizotafitiwa ziliikuwa na kosa la uunganishaji wa maneno mawili kusomeka kama neno moja. Jambo hili ni kinyume na kanuni za uunganishaji wa maneno katika Kiswahili. Ileweke kuwa kuunganisha neno si kosa la jumla katika Kiswahili kwani yapo maneno ambayo kanuni za uundaji wake zinaruhusu maneno zaidi ya moja kuunganishwa na kuwa neno moja. Kwa mfano, mwana+mke → mwanamke, mwana+nchi → mwanchi, kanda+mbili → kandambili, mwana+wangu → mwanangu, pima+maji → pimamaji, vunja+jungu → vunjajungu n.k. Hata hivyo, si kila maneno katika Kiswahili sanifu huruhusu kuunganishwa na kuwa neno moja pomoja na kwamba zipo kanuni za uunganishaji wa maneno. Kuunganisha maneno ambayo hayapaswi kuunganishwa ni kosa la kimsamiati kama 4.3.1 inavyothibitisha.

Mifano inaonesha kwamba kiunganishi *kwa* kimeunganishwa na maneno *sababu*, *kuwa* na *hiyo* yakiandikwa *kwasababu*, *kwakuwa*, *kwahiy* ambayo yanatosomeka kama neno moja badala ya ‘*kwa sababu*, *kwa kuwa*, *kwa hiyo*.’ Pia, katika mfano huohuo kihuishi *wa* kimeunganishwa na maneno *kweli* na *kwanza* yakiandikwa *wakweli*, *wakwanza* badala ya ‘*wa kweli*, *wa kwanza*.’ Kitenzi *kuwa* ambacho kimejitokeza kwa maumo ya *ina* na *wana* kimeunganishwa na maneno *idadi* na *jukumu* na kuandikwa kama ‘*inайдади*, *wanajukumu*.’ Wakati huohuo maneno *na* na *ni* yameunganishwa yakiandikwa *nani* kama neno moja. Kwa kuzingatia taratibu za uunganishaji wa maneno, mifano iliyotolewa hapa imekiuka kanuni hizo na hivyo ni makosa kisarufi. Kwa hiyo, usahihi wa maandishi ya maneno hayo ulipaswa kuwa kama inavyooneshwah hapa chini.

- a) Uzalendo wa *kweli*...
- b) Kwa *sababu*...
- c) Ina *idadi* kubwa ya *watu*...
- d) Na *ni* shirika la umma ambalo serikali imewekeza...
- e) Mkutano wa SADC *ni* wa *kwanza*....
- f) Kwa *sababu* ya *janga* la...
- g) Kwa *kuwa* tayari ameshakamatwa...
- h) Amesema Wakenya *wana jukumu* ...
- i) Kwa *hiyo* bodi...

Vilevile, kosa la kuandika neno isivyo limejitokeza kwa kutenganisha neno moja. Maneno ya Kiswahili yana tabia ya kunyambulishwa. Mzizi au shina la neno linaponyambulishwa huhesabika kuwa ni neno moja kiumbo. Tafiti zinaonesha kuwa wazungumzaji wa Kiswahili hufanya makosa ya utenganishaji wa meneno hasa vitenzi kwa kujua au kutojua. Aruba (2017:78) anashadidia hoja hii kwa kusema kuwa kosa la kutenganisha neno moja hupatikana sana katika maandishi. Waandishi

wengi hutatizwa na neno refu sana kiasi cha kufikiria kulitenganisha ili yawe mawili au zaidi. Hali hiyo imethibitishwa na mfano ufuatao:

Jedwali 4.2.1.3.2: Kosa la Kutenganisha Neno

Chombo cha Habari	Mifano ya Makosa
ITV	(j) ...visa <i>zilizo isha</i> muda... (k) ...wote <i>wanao kaidi</i> ... (l) ...watumishi <i>wa nne</i> ...

Mifano hii inaonesha jinsi ambavyo makosa ya utenganishaji wa neno moja hufanyika kwenye vyombo vya habari vya Tanzania. Inaonesha kuwa mashina *isha*, *kaidi* na *nne* yametenganishwa na viambishi awali vyake ambavyo kwa pamoja huunda neno lenye umbo moja. Vitenzi ‘*zilizoisha*’ na ‘*wanaokaidi*’ vimeandikwa kimakosa kama *zilizo isha*, *wanao kaidi* wakati huohuo, kivumishi ‘*wanne*’ kimeandikwa isivyo kama *wa nne* kwa kutenganisha shina na kiambishi awali cha upatanaisho. Kimaandishi, maneno yakitenganishwa hivyo huonekana ni maneno mawili tofauti yenyе kubeba maana ya kileksika, jambo ambalo si sahihi kisarufi. Hii ni kwa sababu viambishi awali vinavyotenganishwa na shina hukosa maana kileksika. Kwa hivyo, usahihi wa tungo hizo ulipaswa kuwa kama inavyoonekana hapa hini.

- (j) ... viza *zilizoisha* muda ...
- (k) ... wote *wanaokaidi*
- (l) ... *watumishi wanne*

4.2.1.4 Udondoshaji wa Neno

Kwa mujibu wa BAKITA (2015:1055) udondoshaji ni utaratibu wa kuondoa kipashio kimojawapo cha kiisimu katika silabi, neno, kirai au sentensi. Akiunga

mkono wazo hili Ontieri (2015) anasema kuwa udondoshaji ni kuondoa kipashio katika tungo kwa njia inayokiuka taratibu za lugha. Udondoshaji kama dhana ya kisarufi si kosa isipokuwa pale ambapo tendo hilo linafanyika kinyume na taratibu za lugha husika. Mathalani, kuondoa neno linalotakiwa katika miandamo ya sentensi ni kosa la kiudondoshaji. Kulingana na data ya utafiti huu, kosa la udondoshaji lililofanyika lilihusu maneno.

Jedwali 4.2.1.4: Kosa la Udondoshaji wa Neno

Chombo cha Habari	Mifano ya Makosa
TBC1	(a) <i>Kazi inaenda vizuri_sababu hakuna...</i> (b) <i>Kutokana_kuwa na wateja wengi...</i>
ITV	(c) <i>Maambukizi_virusi_Corona...</i> (d) ...ikiwa ni <i>siku moja_kuagiza wamiliki...</i> (e) <i>Mashabiki_Simba na Yanga wasiende na silaha uwanjani</i> (f) ... <i>afisa_TRA...</i>
STAR TV	(g) Ofisi ya serikali ya mtaa <i>yateketea__moto.</i> (h) <i>Wakazi_Bukoba waeleza matumaini yao kwa rais.</i> (i) ... <i>walishtumiwa_kosa hilo...</i>

Jedwali 4.2.1.4 ni baadhi ya mifano ya kosa la udondoshaji wa maneno katika matini za habari zilizochunguzwa. Katika (a), (g) na (i) neno *kwa* limedondoshwa kwenye tungo hizo. Katika (e), (h) na (f) udondoshaji ulihusisha neno *wa* wakati katika mifano (b), (c) na (d) maneno *na, ya, vya, baada ya* yalidondoshwa kwenye matini za habari. Maneno hayo yaliyodondoshwa, tukiyachunguza kwa makini tunabaini kuwa ni kihuishi au kiunganishi (*kwa, wa, vya, baada ya*). Hivyo, maneno hayo yalipaswa kuwapo katika miandamo ya tungo hizo ili kuепusha kosa la udondoshaji

kwani kukosekana kwayo kunaleta hitilafu ya kisarufi hasa ya kimaana. Kwa maana hiyo, tungo hizo zilipaswa kuwa kama ifuatavyo:

- (a) Kazi inaenda vizuri kwa sababu hakuna...
- (b) Kutokana na kuwa na wateja wengi...
- (c) Maambukizi ya virusi vya korona...
- (d) ...ikiwa ni siku moja baada ya kuagiza wamiliki...
- (e) Mashabiki wa Simba na Yanga wasiende na silaha uwanjani.
- (f) ...afisa wa *TRA*...
- (g) Ofisi ya serikali ya mtaa yateketea kwa moto.
- (h) Wakazi wa Bukoba waeleza matumaini yao kwa rais.
- (i) Walishutumiwa kwa
- (j) Kosa hilo

4.2.1.5 Uchopekaji wa Neno Lisilohitajika

Uchopekaji katika tasnifu hii ni kuingizwa kwa kipashio au neno katika miandamo ya maneno au vipashio vinavyojenga tungo husika. Uchopekaji huchukuliwa kuwa ni kosa la kisarufi pale ambapo neno au kipashio chochote ambacho hakitakiwi kuwapo katika miandamo ya tungo. Utafiti umeonesha kufanyika kwa kosa la uchopekaji wa maneno ambayo kulingana na mpangilio wa tungo hayakupaswa kuwapo.

- (a) ... waliokuwa wanaumwa *na* ugonjwa wa Corona wamefariki...
- (b) ... ambao *walikuwa* walihukumiwa katika mahakama ya mwanzo....

Mifano hii inaonesha uwapo wa kosa la uchopekaji wa maneno ambayo hayakupaswa kuwapo katika tungo hizo. Katika matini za ITV tuliweza kubaini uchopekaji wa neno *na* kwenye mfano (a) ilhali kwenye matini za STAR TV tuliweza kubaini uchopekaji wa neno *walikuwa* ambalo halikupaswa kuwapo katika mpangilio wa maneno ya tungo kwenye mfano (b). Kwa maana hiyo basi, tungo hizo zilipaswa kuwa kama:

- (a) ... waliokuwa wanaumwa ugonjwa wa korona wamefariki...
- (b) ... ambao walihukumiwa katika mahakama ya mwanzo...

4.2.1.6 Kosa la Kutumia Maneno Yasiyo Sanifu

Kila lugha huwa na maneno sanifu yatumikayo katika mawasiliano. Maneno sanifu ni yale ambayo yamekubalika kutumika kwenye mawasiliano rasmi. Lugha ya Kiswahili ina maneno yaliyosanifishwa ili yatumike kwenye mawasiliano rasmi. Hata hivyo, maneno yasiyo sanifu huibuliwa na kutumiwa na wazungumzaji wa lugha kwa ajili ya kutimiza matakwa yao ya kimawasiliano. Zipo sababu mbalimbali zinazowafanya wazungumzaji wa lugha kutumia maneno yasiyo sanifu. Katika muktadha rasmi, maneno sanifu yanayopaswa kutumika. Kwa mujibu wa van Dijk (1988), katika hali rasmi na lugha andishi huwa tunatumia maneno sanifu, changamano, yaliyokamilika, na sentensi zenye muundo sahihi wa kisarufi kuliko ilivyo kwenye mawasiliano yasiyo rasmi. Matini za habari hutumia lugha rasmi na sanifu kama asemavyo van Dijk (ameshatajwa). Kwa kuzingatia msingi wa urasmi na usanifu wa lugha, data zilionesha kwamba chaneli za TBC1, ITV na STAR TV zilisheheni matumizi ya maneno ya mtaani. Mifano ifuatayo inaonesha kosa hilo.

- (a) Kuna baadhi ya watangazaji wana matumizi makubwa sana ya *rejestra za mtaani* kama *wakulungwa, kwiho* na mengine mengi (MS11)
- (b) Matumizi mengi ya *misimu* kama, mfano *wajuba, wanyabi* (MS10)
- (c) *Kutotumia lugha sanifu au fasaha* kwa kipindi chote cha kutangaza habari hiyo yote ni pamoja na *kutumia lugha za mitaani ambazo sio sanifu* (MS6)
- (d) Tatizo la kutumia *maneno yasiyo sanifu* (MS3)
- (e) *Matumizi ya lugha ya mtaani* hasa kwa Televisheni ya star TV, mfano *Nipe gwala*, na kwenye kipindi cha kamusi ya mtaani *matumizi ya misimu* kama “*buku*” n.k. (MS14)

Ni dhahiri kwamba mifano hii inaonesha jinsi ambavyo vyombo vyaya habari vinatumia lugha na maneno yasiyo sanifu na fasaha. Data zimeonesha kuwa

wanahabari wa vyombo hivyo wanatumia misimu, rejestra za mitaani na maneno yasiyo sanifu. Kwa kawaida misimu huwa ni maneno yasiyo sanifu au rasmi yanayoibuliwa na watu kwa ajili ya kuwasiliana. Pia, rejestra ni mtindo wa lugha kulingana na kundi fulani la watu katika jamii. Miongoni mwa rejestra ni ile ya mtaani ambayo haizingatii ufasaha na usanifu. Tumeona kuwa wasailiwa walitaja baadhi ya maneno ya mtaani kama *wakulungwa, kwiho, wajuba, wanyabi, gwala* na *buku* kuwa yanatumika kwenye vyombo vya habari. Tafsiri yake ni kwamba mazoea ya kutumia maneno kama hayo kwenye vipindi vingine yaweza kusababisha watangazaji wa habari kutumia maneno hayo kwenye habari za michezo na burudani ambazo ni sehemu ya taarifa ya habari ambayo hutumia lugha sanifu, rasmi na fasaha. Kwa hiyo, ni wajibu wa wanahabari wa vyombo hivyo kutumia maneno sanifu, rasmi na fasaha ili kuepuka kosa la matumizi maneno yasiyo sanifu.

4.2.2 Makosa ya Kimatamshi

Matamshi ni namna au jinsi ya kutamka au jinsi ya utamkaji wa sauti katika lugha (TATAKI, 2013: 320; BAKITA, 2015: 594). Kila lugha ina kanuni zinazoongoza utamkaji wa sauti na maneno. Kwa mfano, sauti za Kiswahili zina kanuni za utamkaji zinapokuwa mojamoja na zinapounganishwa kuunda vipashio vikubwa zaidi ya fonimu. Kwa maana hiyo, Massamba, Kihore na Msanjila (2004) wanaeleza kwamba neno ‘matamshi’ katika taaluma ya fonolojia lina maana moja tu ambayo ni ule utaratibu utumikao katika utoaji wa sauti za maneno ya lugha ya binadamu. Fasili hii inaonesha kwamba matamshi yana utaratibu wake. Zipo taratibu mbalimbali za utamkaji wa sauti na maneno ya Kiswahili. Taratibu hizi huzingatia mahali pa utamkiaji na namna ya utamkaji wa sauti (Massamba na wenzake, 2004:7). Majedwali yafuatayo yanaonesha sifa za utamkaji wa sauti za Kiswahili.


Jedwali 4.2.2.1: Taratibu za Utamkaji wa Konsonanti za Kiswahili kwa Sifa za Mahali na Jinsi ya Utamkaji

Jinsi ya Matamshi		Mahali pa Matamshi						
		Midom o	Midom o-Meno	Men o	Ufizi i	K/Gum u	K/Lai ni	Koromo eo
VIPASUO	Ghuna	b			d		g	
	Visoghu na	p			t		k	
	Mpumuo				t ^h		g ^h	
VIZUIO-KWAMIZA	Ghuna	p ^h				j		
	Visoghu na					č		
	Mpumuo					č ^h		
VIKWAMIZI	Ghuna		v	ð	z		y	h
	Visoghu na		f	θ	s	ʃ		
NAZALI		m			n	ɲ	ŋ	
VITAMBAZA					l			
VIMANDENDE					r			
VIYEWUSHO		w				y		

Chanzo: Massamba, Kihore na Msanjila (2004:44)

Kulingana na jedwali 4.2.2.1, kanuni mojawapo ya utamkaji wa konsonanti za Kiswahili ni sifa zake za matamshi. Kanuni hii ni kanuni ya namna ya utamkaji na mahali konsonanti inapotamkiwa.

Jadwali 4.2.2.2: Taratibu za Utamkaji wa Irabu za Kiswahili



Chanzo: Ufaraguzi wa Mtafiti (2020)

Nazo irabu za Kiswahili hutamkwa kwa kuzingatia kanuni ya sifa ya utamkaji ambayo ni kanuni ya namna (mkao wa mdomo na ulimi) na mahali pa utamkiaji (mbele, kati, nyuma, chini, kati na juu).

Majedwali hayo yanaeleza mojawapo ya kanuni za utamkaji wa sauti za lugha ya Kiswahili. Kanuni hiyo ni namna sauti zinavyopaswa kutamkwa na mahali ambapo sauti hizo zinapaswa kutamkiwa ili kutoa matamshi fasaha na sahihi ya Kiswahili. Kanuni nyingine mionganoni mwa nyingi, ni kwamba konsonanti za Kiswahili kama sauti mojamoja hutamkwa na kusikika kwa athari ya sauti /e/ (Kihore, Massamba na Msanjila, 2003). Kwa mfano, tunasema /be, che, de, fe, ge/ n.k lakini inapotokea zimeungana na sauti nyingine zikiambatana na irabu katika silabi au maneno basi utamkaji wa konsonanti hufuata irabu zinazoandamana nazo (Kihore na wenzake, 2003:16). Hii ni kusema kuwa /b/ hutamkwa [be] ikiwa pekee ila ikiambatana na irabu nyingine tofauti na /ɛ/ utamkaji wake utaathiriwa na irabu ilioandamana nayo. Kwa mfano, ikiambatana na irabu /u/ au /ɔ/ itatamkwa /bɔ/ au /bu/. Pia, kanuni nyingine ya utamkaji katika Kiswahili ni kuzingatia mkazo, kiimbo na lafudhi sahihi ya Kiswahili. Kanuni hii hutawala zaidi vipashio vikubwa kuliko sauti. Hivyo basi, kwa kuzingatia kanuni hizo, mtafiti alibaini uwapo wa kosa la utamkaji wa maneno ya Kiswahili katika habari zilizochunguzwa kama ifuatavyo:

Jedwali 4.2.2.3: Makosa ya Kimatamshi

Chombo cha Habari	Mifano ya Makosa
TBC1	(a) <i>Waakti</i> (b) <i>Kalika</i>
ITV	(c) Mashabiki <i>watakaoudhuria</i> mtanange huo... (d) <i>Eidha</i> ...
STAR TV	(e) Baada ya uchaguzi uliofanyika <i>kumalidhika</i> (f) Amechukua fomu ya kuwania <i>tchena</i> uspika ... (g) Karibu sasa <i>kalika</i> habari ... (h) Kifungo <i>chia</i> mwaka mmoja...

Hii ni baadhi ya mifano ya makosa ya matamshi yaliyofanywa na wanahabari wa TBC1, ITV na STAR TV. Katika (a) neno *wakati* lilitamkwa /wa:kti/ ambapo irabu /a/ ilivutwa wakati haikupaswa kuvutwa. Wakati huohuo, irabu /a/ ya kati ya /k/ na /t/ ilidondoshwa na kufanya utamkaji wa neno hilo kuwa na makosa mawili ya uvutaji na udondoshaji kinyume na inavyotakiwa. Kwa upande wa (b) na (g) kipasuo /t/ cha ufizi kilitamkwa kama kitambaza /l/ cha ufizi na kufanya neno *katika* kutamkwa /kalika/ badala ya /katika/. Hii inaweza kusababishwa na sauti hizo kuwa si ghuna na zinatamkiwa eneo moja, jambo ambalo linaweza kusababisha mtamkaji anayetamka kwa haraka kutamka /l/ badala ya /t/. Kwa upande wa (c) kikwamizi ghuna /h/ cha koromeo kilidondoshwa katika utamkaji wa *watakaohudhuria* na neno hilo kutamkwa /watakaouðuria/ badala ya /watakaðhuðuria/. Baadhi ya wazungumzaji wa Kiswahili hawawezi kutamka sauti /h/ hasa inapoambatana na irabu, hivyo hujikuta wakitamka irabu iliyoandamana na kikwamizi hicho. Kwa mfano, tafiti zinaonesha kwamba baadhi ya makabila ya Waswahili husikika

yakitamka /abari/ badala ya /habari/, /akuna/ badala ya /hakuna/, /uja/ badala ya /huja/ n.k.

Vilevile, maneno *aidha*, *kumalizika*, *tena*, na *cha* yalitamkwa kimakosa na wanahabari kama /eiða, kumaliðika, tčëna, čia/. Kwenye (d) irabu /a/ ya chini ilitamkwa kama irabu /ε/ ya chini-kati. Kosa hili linawezekana kutokea kwa haraka kwa sababu /a/ na /ε/ zimekaribiana kuliko irabu nyingine. Mfano (e) umehusisha kosa la kutotamka kikwamizi-ghuna /z/ cha ufizi na kutamka kikwamizi-ghuna /ð/ cha meno. Kosa kama hili ni rahisi kufanyika kwa wazungumzaji ambao katika mfumo wao hawana sauti /ð/ na badala yake wana /z/ pekee au wale ambao wana kithembe. Kwa hiyo, inakuwa vigumu kwao kutamka /dh/. Katika kuepuka athari hiyo, hujikuta wakitamka /ð/ badala ya /z/.⁷ Kwa upande wa (f), tatizo la utamkaji lilitokea lilihusu uchopekwaji wa kizuio-kwamizi kisoghuna cha kaakaa laini /č/ ambacho hakikupaswa kuwapo ilhali kwenye (h) irabu /i/ ya juu mbele ilichopekwa pia. Hivyo, katika 7(f)-(h) utamkaji ulihuisha uchopekwaji wa vitamkwa ambavyo havikutakiwa kuwapo.

Kosa la matamshi lilidhihirishwa vilevile na hadhira ya vyombo vy a habari iliyosailiwa. Watafitiwa walipotakiwa kutaja makosa ya kisarufi ambayo wameyashuhudia katika TBC1, ITV na STAR TV, walisema kwamba kosa au tatizo la matamshi mabaya ni mionganini mwa makosa ya kisarufi yanayofanywa kwenye vyombo hivyo (MS2, MS5, MS7 na MS8). Zaidi ya hayo, wasailiwa wawili walifafanua kwa kina na kutoa mifano kama ambavyo MS3 aliandika: ‘1. *Kuweka mkazo ambapo hapatakiwi* 2. *Makosa ya matamshi mf. badala ya kusema barabara anasema balabala.*’ MS12 alisema: *matamshi mabaya mfano hichi kipindi = hiki*

kipindi. Kutokana na hayo, utamkaji sahihi wa maneno yaliyotamkwa vibaya ulipaswa kuwa:

- (a) *Waakti* → wakati /wakati/
- (b) *Kalika* → katika /katika/
- (c) *Mashabiki watakaoudhuria* mtanange huo... → watakaohudhuria /watakaøhuðuria/
- (d) *Eidha* → aidha /aiða/
- (e) Baada ya uchaguzi uliofanyika *kumalidhika* ... → kumalizika /kumalizika/
- (f) Amechukua fomu ya kuwania *tchena* uspika... → tena /tëna/
- (g) Karibu sasa *kalika* habari ... → katika /katika/
- (h) Kifungo *chia* mwaka mmoja... → cha /ča/

4.2.3 Makosa ya Kimaumbo

Kwa mujibu wa Massamba (2007:144) umbo ni jinsi kitu kilivyojengeka au kilivyoundwa. Katika sarufi, dhana ya umbo hurejelea jinsi neno lilivyoundwa au kujengeka. Sarufi maumbo ni taaluma inayohusika na maelezo ya uchambuzi wa maneno kwa kuchunguza jinsi maneno yalivyoundwa (Wesana-Chomi, 2013). Uchunguzi huo huongozwa na kanuni mbalimbali. Zipo sheria au kanuni zinazotawala taaluma ya mofolojia kwa kila lugha. Miongoni mwa kanuni za mofolojia ya Kiswahili ni zile zinazoongoza upachikaji wa vipashio mbalimbali vinavyounda maneno ya Kiswahili. Kwa mfano, kanuni za uambishaji na unyambulishaji wa maneno; uchanganuzi wa mofu za maneno; na kanuni za mpangilio wa viambishi awali na tamati kwenye mizizi ya maneno. Kwa upande mwingine, ukiukwaji wa kanuni hizi ni makosa kisarufi. Kwa kuongozwa na mhimili wa uchanganuzi wa matini za habari kwa kuzinagtia kanuni za kila kiwango cha sarufi (van Dijk, 1988: 11-12), tajiriba ya mtafiti kuhusu kanuni za miundo ya maneno ya Kiswahili, mtafiti aliweza kuchunguza kwa makini mpangilio wa maumbo ya maneno yaliyojenga matini za habari. Katika uchunguzi huo, ilibainika

kwamba baadhi ya maneno yalikuwa na makosa ya kimaumbo. Makosa hayo ni ya aina tatu ambazo ni umoja na wingi, uchopekaji na udondoshaji wa vipashio vyateno.

4.2.3.1 Kosa la Umoja na Wingi

Katika mawasiliano ya Kiswahili, imekuwa kawaida kwa watumiaji wake kufanya makosa ya maumbo ya umoja na wingi. Mara nyingi hali hii hutokea pale ambapo maneno hupewa maumbo ya umoja na wingi isivyo au kutopewa maumbo hayo hali yakihitajika au maumbo hayo kuchanganywa. Data zilionesha uwapo wa kosa la umoja na wingi katika matini za habari za TBC1, ITV na STAR TV kama ifuatavyo:

Jedwali 4.2.3.1: Kosa la Umoja na Wingi

Chombo cha Habari	Mifano ya Makosa
TBC1	(a) ... ilikuwa ni ndani ya <u>masaa</u> ishirini na nne...
ITV	...maziwa ya unga <u>maofisini</u> . <u>Madhaifu</u> yaliyojitekeza...
STAR TV	(b) ... nyimbo zenyet <u>jumbe</u> mbalimbali...

Mifano katika jedwali 4.2.3.1 inaonesha makosa ya umoja na wingi yaliyofanywa na wanahabari wakati wa kuwasilisha habari. Inaonekana mofu {ma} ilipachikwa katika mzizi {saa} ili kudokeza dhana ya wingi wa saa. Hili ni kosa kwa kuwa ‘saa’ ni mzizi huru ambaa haupokei kiambishi chochote cha umoja wala wingi. Hata hivyo, hali hii imekuwa mazoea kwa wazungumzaji wengi wa Kiswahili kuongeza mofu za umoja au wingi katika neno ‘saa’. Kwa mfano, watu mbalimbali, mara kwa mara, husikika wakisema ‘lisaa limoja na nusu, masaa matano n.k.’ Hii inaonesha kuwa katika akili za wazungumzaji wa Kiswahili kuna dhana kwamba nomino ‘saa’

hupokea viambishi nya umoja na wingi kumbe sivyo. Hali hiyo hujitokeza pia katika maneno ya (b)-d). Katika mifano hiyo, mizizi {ofisi, dhaifu, ujumbe} imepachikwa mofu {ma} ya wingi katika (b)-(c) na mofu kapa ya wingi katika (d). Kuongezwa kwa {ma} katika mizizi {ofisi, dhaifu} kulilenga kudokeza wingi; kudondosha silabi \$u\$ katika mzizi {ujumbe} kulilenga kudokeza wingi jambo ambalo ni makosa kisarufi. Haya ni makosa kwa sababu mizizi {ofisi, dhaifu} hairuhusu kupokea mofu za wingi. Vilevile, neno *ujumbe* halina mofu ya wingi, hivyo kudondosha \$u\$ na kubaki *jumbe* kwa maana ya wingi ni makosa kisarufi. Hata hivyo, hali hii imekuwa ikijitokeza mara kwa mara ikichukuliwa kuwa ni sahihi kwa wazungumzaji wa Kiswahili wakiwamo wanahabari. Kwa mfano, maandishi na mazungumzo mengi ya watumiaji wa Kiswahili hujaa maneno yenyе makosa ya umoja na wingi kama 'mashule, maofisi, madhaifu, jumbe za wasilikizaji, oni langu, mahospitali n.k. Kulingana na upotofu huo, maneno hayo yalipaswa kuandikwa kwa usahihi kama:

- a) ...ilikuwa ni ndani ya saa ishirini na nne...
- b) ...maziwa ya unga ofisini...
- c) Udhifu uliojitokeza...
- d) ... nyimbo zenyе ujumbe mbalimbali.

4.2.3.2 Kosa la Uchopekaji wa Kipashio Kisichostahili

Katika uchunguzi wa matini za habari, utafiti huu ulibaini kuwa baadhi ya maneno maumbo yake yalikuwa na hitilafu za kimaumbo ambapo vipashio (mofu/silabi/sauti) vilichopekwa pasipo kustahili. Iteleweke kuwa kipashio kisichostahili ni kile ambacho hakikupaswa kuwa sehemu ya umbo la neno husika. Vipashio hivyo vyaweza kuwa ni fonimu/sauti, silabi au mofu. Kwa mfano:

Jedwali 4.2.3.2: Kosa la Uchopekaji wa Kipashio Kisichostahili

Chombo cha Habari	Mifano ya Makosa
TBC1	(a) Virusi hivyo <i>vinavyosababishwa</i> homa ya mapafu... (b) Kipindi <i>hichi</i> ... (c) ...dosari alizotaja kuwa <i>zinaikabilia</i> taasisi hiyo...
ITV	(d) Burundi ilituhumiwa <i>kutoheshimisha</i> haki za binaamu. (e) <i>Mubashara</i> (f) ... <i>akasema</i> atashughulikia...
STAR TV	(g) ... <i>alijadiliana</i> mgogoro huo na mshirika wake ... kwa njia ya simu... (h) ...hatua zitakazochukuliwa na serikali yake <i>kurejelea</i> shughuli za kawaida... (i) ... ambaye <i>amewahi</i> kuwania urais mara nne...

Katika mifano ya jedwali 4.2.3.2 kuna makosa ya uchopekaji wa vipashio ambavyo havipaswi kuwa sehemu ya maumbo ya maneno hayo. Ikumbukwe kuwa katika taaluma ya mofolojia, maumbo ya kimofolojia (mofu na mzizi) huwa na maana za kileksika au kisarufi. Mofu huru zina maana za kileksika na mofu fungo zina maana za kisarufi. Hivyo, kila umbo la neno huwakilisha maana fulani inayokuwa sehemu ya maana ya neno zima. Uwekaji wa umbo ambalo lina maana tofauti na iliyolengwa katika shina au mzizi wa neno ni kufanya kosa la kiumbo. Kwa kuzingatia muktadha wa matini za habari na maana zilizodhamiriwa, mtafiti alibaini maumbo ambayo hayakupaswa kuwa sehemu ya maneno yaliyounda matini za habari. Hii ni kwa sababu uwapo wake unabadili au unaharibu maana zilizokusudiwa.

Katika mifano (a) – (i) isipokuwa mfano (b) na (e), maumbo yaliyopigiwa mstari hayakupaswa kuwapo kwani yanavuruga maana zilizodhamiriwa. Katika mfano (a) mofu {w} iliongezwa na kuunda mofu {eshw} ya ‘utendeshwa’ wakati dhana iliyolengwa ilikuwa ni ‘utendesha’. Hivyo, mofu hiyo haikustahili kuwapo. Mfano

(c) nao una kosa la kuwa na mofu tamati {a} ambayo uwapo wake unajenga dhana ya ‘utendea’ hali dhana iliyodhamiriwa kuwasilishwa na kitensi hicho ni ‘utenda.’ Pia, katika mfano (d) mofu {ish} ya utendesha na mofu tamati {a} zilipachikwa kwenye kitensi na kukifanya kipoteze dhana ya ‘utenda’ iliyodhamiriwa na kubebeshwa dhana ya ‘utendesha.’ Hali kadhalika, katika mfano (f) mofu {ka} ya utimilifu ilitumiwa badala ya {li} ya wakati uliopita. Hilo ni kosa kwani habari iliyowasilishwa ilihusu tukio lililotokea nyakati za nyuma. Mfano (g) una kosa la kupachikwa kwa mofu {an} ya kutendana na mofu tamati {a}. Uwapo wa mofu hizo umefanya kitensi kiwe na kauli ya kutendana wakati tukio lililoelezwa zilipaswa kuelezwa kwa kauli ya kutenda ikizingatiwa kuwa kitensi hicho kiliambatana na nomino ambayo ni mtendwa. Mfano (h) una kosa la kuwapo kwa mofu {le} ambayo uwapo wake unapotosha kabisa maana ya kitensi na kukifanya kieleze tukio la *kurejea* badala ya tukio la *kurudisha* ambalo lingedokezwa kwa mofu {sh} ya kutendesha. Mfano (i) una kitensi ambacho kina kosa la kuwa na mofu {me} ya hali timilifu hali tukio lililoelezwa lilitokea wakati uliopita. Kwa upande wa mifano (b) na (e) makosa yaliyofanyika ni kutumia mofu {chi} ambayo inavuruka upatanisho wa kisarufi badala ya {ki} katika (b) ilhali kosa la uongezaji wa irabu /u/ lilifanyika katika umbo {mu} badala ya {m}. Kwa maelezo haya, tungo hizo zilipaswa kuandikwa kwa usahihi kama inavyooneshwa hapa chini.

- (a) Virusi hivyo vinavyosababisha homa ya mapafu...
- (b) Kipindi hiki...
- (c) ...dosari alizotaja kuwa zinaikabili taasisi hiyo...
- (d) Burundi ilituhumiwa kutoheshimu haki za binaamu.
- (e) Mbashara
- (f) ...alisema atashughulikia...
- (g) ... alijadili mgogoro huo na mshirika wake kwa njia ya simu...

- (h) ...hatua zitakazochukuliwa na serikali yake kurejesha shughuli za kawaida...
- (i) ...ambaye aliwahi kuwania urais mara nne...

4.2.3.3 Kosa la Udondoshaji wa Kipashio

Data zilizokusanywa zinaonesha uwapo wa kosa la udondoshaji wa vipashio ambavyo vilipaswa kushiriki kujenga maumbo ya maneno. Vipashio vilivyopaswa kujenga maumbo ya maneno na vikadondoshwa ni mofu au silabi au fonimu. Kutokuwapo kwa vipashio hivyo, kumesababisha tungo husika kupoteza maana na hivyo kuharibu ujumbe wa matini husika. Kwa mfano:

Jedwali 4.2.3.3: Kosa la Udondoshaji wa Kipashio

Chombo cha Habari	Mifano ya Makosa
TBC1	<ul style="list-style-type: none"> (a) ...imeanza <i>kutolea</i> bandarini... (b) ... ambaye ni kati ya Wairan <i>walizuiliwa</i>... (c) Ombi ambalo <i>litajadili_na</i> mamlaka...
ITV	<ul style="list-style-type: none"> (d) Basi la abiria <i>lilokuwa</i> likitokea... (e) Watu hao <i>_tano</i> wamepona... (f) Lengo na <i>_dhumuni</i>...
STAR TV	<ul style="list-style-type: none"> (g) ... mkutano wa kwanza kwa mawaziri <i>wanahusika</i> na... (h) Majanga <i>yaliotokea</i>... (i) ...ambao <i>wamekua</i> mitaani kila uchao...

Kama asemavyo Ontieri (2015:6) kuwa udondoshaji ni kuondoa kipashio katika neno kwa njia inayokiuka taratibu za lugha, ndivyo mifano ya jedwali 4.2.3.3 inavyoonesha. Katika mifano hiyo, maeneo yaliyopigiwa mistari ndipo ambapo vipashio vilivyodondoshwa vilipaswa kuwa. Katika mfano (a) mofu {w} ya kutendwa imedondoshwa kwenye kitenzi *kutolea*; mfano (b) mofu {o} ya urejeshi wa mtendwa imedondoshwa na kitenzi kuandikwa *walizuiliwa* ambapo mofu hiyohiyo imedondoshwa kwenye mfano (g). Aidha, silabi \$wa\$ ilidondoshwa na

kitenzi kuandikwa *litajadili* katika mfano (c) wakati kwenye mfano (d) mofu {li} ya njeo ya wakati uliopita ilidondoshwa kwenye kitenzi *lilokuwa*. Kosa hilo lipo pia katika mfano (e) ambapo neno lililoathiriwa na hali hiyo ni kivumishi. Badala ya kivumishi kuwa na umbo *watano* kimeandikwa *tano* ambapo mofu {wa} ya upatanisho wa kisarufi imedondoshwa. Kwenye mfano (f), silabi \$ma\$ inayojenga nomino *madhumuni* ilidondoshwa. Kwa upande wa mfano (h), fonimu /y/ inayounda mofu {yo} ya urejeshi ilidondoshwa kwenye kitenzi *yaliyotokea*. Kwenye mfano wa mwisho, udondoshaji ulikumba fonimu /w/ ambayo inaunda mzizi wa kitenzi *kuwa* na kitenzi kuandikwa *wamekua*. Kulingana na ithibati hizi, inamaanisha kuwa kosa la udondoshaji lililoathiri maumbo ya maneno lilihusisha udondoshaji wa mofu, silabi na fonimu. Kwa hiyo, maneno hayo yalipaswa kuandikwa kwa usahihi kama ifuatavyo:

- (a) ...imeanza kutolewa bandarini...
- (b) ... ambaye ni kati ya Wairani waliozuiliwa...
- (c) Ombi ambalo litajadiliwa na mamlaka...
- (d) Basi la abiria lilokuwa likitokea...
- (e) Watu hao watano wamepona...
- (f) Lengo na madhumuni...
- (g) ... mukutano wa kwanza kwa mawaziri wanaohusika na...
- (h) Majanga yaliyotokea...
- (i) ... ambao wamekuwa mitaani kila uchao...

4.2.4 Makosa ya Kimuundo

Muundo unaorejelewa hapa ni ule utaratibu wa mpangilio wa vipashio vyta tungo katika sentensi unaoleta maana katika lugha. Kila lugha inazo taratibu zinazoongoza mpangilio sahihi na unaokubalika wa maneno na vipashio vingine katika sentensi. Ukiukwaji wa taratibu hizo ndio unaorejelewa hapa kama makosa ya kimuundo. Nadharia ya UHK husisitiza kuwa lengo la uchanganuzi wa ripoti za habari si tu

kuzingatia uwezekano ila kuzingatia miundo halisi ya kisarufi au iliyokubaliwa ambayo hufasili utumiaji wa lugha katika muundo wa matini. Mhimili huu ulimwongoza mtafiti kuchunguza kwa makini miundo ya sentensi katika matini za habari ili kubaini uwapo wa makosa ya kimuundo. Kama wasemavyo Odeo na Geoffrey (2008), makosa ya kimuundo hutokea pale ambapo wazungumzaji au waandishi wanapojenga sentensi bila kuzingatia utaratibu au mpangilio wa maneno unaokubalika katika lugha. Hata hivyo, makosa ya kimuundo hayatokei katika kiwango cha sentensi tu bali hata katika vipashio vidogo zaidi ya sentensi kama kirai na kishazi. Data zilizokusanywa na mtafiti zilionesha kuwapo kwa makosa ya kimuundo katika matini za habari zilizochunguzwa. Ilibainika kwamba vyombo vyahabari vya TBC1, ITV na STAR TV vilifanya makosa ya kimuundo ya upatanisho wa kisarufi, mpangilio usiofuata sarufi ya Kiswahili na urudiaji wa maneno.

4.2.4.1 Kosa la Upatanisho wa Kisarufi

Upatanisho wa kisarufi ni uhusiano wa kisintaksia ambapo neno moja hutawala umbo la kimofolojia la neno au maneno mengine katika tungo. Katika lugha za Kibantu, neno linalotawala umbo la kimofolojia la neno au maneno mengine ni nomino au kiwakilishi. Kwa mfano, 'mkulima analima shamba zuri' nomino 'mkulima' inatawala umbo la kitenzi 'analima' kwa kufanya shina la kitenzi hicho kuambikwa kiambishi awali nafsi {a} kinachodokeza mtenda wa jambo. Uwapo wa kiambishi awali nafsi katika kitenzi hicho unafanya sentensi hiyo iwe na upatanisho wa kisarufi. Hivyo, shina au mzizi wa kitenzi unapobeba kiambishi awali ambacho hakiendani na nomino inayotawala katika sentensi hiyo ni ukiukwaji wa kanuni ya upatanisho wa kisarufi. Katika data zilizokusanywa kosa la upatanisho wa kisarufi

lilithibitika. Hadhira iliyosailiwa kwa upande mwingine, ilitaja wazi kwamba wanahabari wa TBC1, ITV na STAR TV hufanya makosa ya upatanisho, kwa mfano: (a) *nyimbo hii* (MS12), (b) *nyimbo ya msanii badala ya wimbo wa msanii* (MS13). Kama walivyoonesha watafitiwa, wanahabari walikiuka kanuni ya upatanisho, hivyo walipaswa kusema ‘*nyimbo hizi, wimbo wa msanii/nyimbo za msanii.*’ Mifano zaidi ya makosa ya upatanisho kutoka kwenye matini zilizochunguzwa ni kama ifuatayo:

Jedwali 4.2.4.1: Kosa la Upatanisho wa Kisarufi

Chombo cha Habari	Mifano ya Makosa
TBC1	(a) ... <i>kuzipatia</i> mgao wa fedha <i>vilabu</i> vya ngazi ya juu... (b) ... <i>kuitumikia</i> kwa uaminifu <i>chama</i> hicho... (c) <i>Anga ya</i> kimataifa...
ITV	(d) <i>Shirika la MNH imekuwa</i> bega kwa bega... (e) ...wamesema <i>tatizo</i> la kuadimika kwa mafuta <i>imekuwa</i> changamoto kubwa kwao... (f) Wananchi <i>waipongeza jeshi</i> la polisi.
STAR TV	(g) ... <i>yaliyoyafanya</i> serikali ya Zanzibar kuja na sera.... (h) ... <i>hizi ni mitambo</i>

Kanuni za kisarufi zinatuelekeza kuwa viambishi vya upatanisho wa kisarufi vinavyowekwa kwenye mashina au mizizi ya vitenzi au vivumishi lazima viakisi nomino inayotawala. Hii ina maana kwamba, kila nomino ina viambishi vinavyoiwakilisha katika ngeli. Kwa msingi huo, upatanisho wa kisarufi huletwa na viambishi ngeli vya nomino katika tungo husika. Uambilaji wa viambishi ngeli tofauti katika kitenzi au kivumishi ni ukiukwaji wa upatanisho wa kisarufi. Kosa la upatanisho hutokea baada ya mzizi wa kitenzi au kivumishi kupachikwa kiambishi cha mtenda/mtendwa ambacho hakioani na nomino husika. Katika jedwali 4.2.4.1

kosa hilo limethibitishwa. Kwenye mfano (a) kiambishi {zi} kimekiuka kanuni ya upatanisho kwa kuwa hakiakisi nomino *vilabu*. Viambishi ngeli inavyoakisi nomino hiyo ni {ki} – umoja na {vi}-wingi na hivyo, kiambishi {vi} kilipaswa kutumika na si {zi}. Katika mfano (b) kiambishi kipatanishi kilipaswa kuwa {ki} na si {i} kwani nomino iliyokuwa inarejelewa ni *chama* ambayo huakisiwa na viambishi ngeli via {ki} – umoja na {vi} – wingi. Aidha, kwenye mfano (c) kipatanishi *ya* kimetumika kimakosa kuunda kihuishi. Hii ni kwa sababu nomino *anga* huakisiwa na kiambishi ngeli {li} hivyo kipatanishi chake kilipaswa kuwa *la*. Kwa upande wa mifano (d) – (f) kosa lilofanyika ni kutumia kiambishi kipatanishi {i} katika vitenzi via tungo hizo badala ya kiambishi {li} kwani nomino *shirika*, *tatizo* na *jeshi* ambazo zinarejelewa katika tungo hizo huakisiwa na viambishi ngeli {li} – umoja na {ya} – wingi. Kadhalika, mfano (g) nao una kosa la upatanisho ambapo kiambishi cha mtendwa {ya} kilichotumika kwenye kitenzi hakikustahili. Hii ni kwa sababu nomino inayorejelewa kwenye kitenzi hicho ni *serikali* ambayo huakisiwa kwa viambishi ngeli {i} – umoja na {zi} – wingi, hivyo kiambishi {i} kilipaswa kutumika. Kwa upande wa kosa la mfano (h), kiambishi kipatanishi kilichotumiwa na mwanahabari ni {zi} badala ya {i} kwani nomino *mitambo* huakisiwa na kiambishi ngeli {i} – wingi na {u} – umoja. Kwa hiyo, usahihi wa tungo hizo ulipaswa kuwa kama inavyooneshwa hapa chini:

- (a) ... kuvipatia mgao wa fedha vilabu via ngazi ya juu...
- (b) ... kukitumikia kwa uaminifu chama hicho ...
- (c) Anga la kimataifa...
- (d) Shirika la MNH limekuwa bega kwa bega ...
- (e) ... wamesema tatizo la kuadimika kwa mafuta limekuwa changamoto kubwa kwao...
- (f) Wananchi walipongeza jeshi la polisi.
- (g) ...yaliyoifanya serikali ya Zanzibar kuja na sera...

(h) ... hii ni mitambo

4.2.4.2 Kosa la Mpangilio Usio Sahihi

Kila lugha ina sheria za mpangilo wa maneno au vipashio vingine katika tungo. Lugha ya Kiswahili ina utaratibu wake wa kupanga vipashio au maneno katika tungo. Ni kanuni mojawapo kwamba, kwa kawaida sentensi ya Kiswahili huanza na nomino ya mtenda, mtendwa au mtendewa na kufuatwa na kivumishi (kama kipo) na kisha kitenzi na maneno mengine (Mochiwa, 2000; Odeo na Geoffrey, 2008:121; Masebo na Nyangwine, 2016:257). Pia sentensi za Kiswahili hutakiwa kuwa na mpangilio wa maneno unaoleta mantiki. Hata hivyo, utaratibu huu hukiukwa na wazungumzaji wa Kiswahili kwa kufanya kosa la mpangilio wa maneno katika tungo. Miongoni mwa wasailiwa, mmoja alitaja jambo hilo akisema ‘*Kuna makosa ya kimuundo katika mpangilio wa maneno wakati wa kuwasilisha kazi za kiuandishi*’ (MS15). ’ Ifuatayo ni mifano zaidi ya kosa hilo.

Jedwali 4.2.4.2 Kosa la Mpangilio Usio Sahihi

Chombo cha Habari	Mifano ya Makosa
TBC1	a) Mapema <i>hii leo</i> ... b) <i>Kumi na sita elfu</i> ...
ITV	c) ...thamani ya TZS 210 Mil..., thamani ya TZS 56 Mil..., thamani ya TZS. 28 Mil..., thamani ya TZS.12 Mil...
STAR TV	d) ... <i>Moscow hivi majuzi ilipeleka ndege</i> ... e) <i>Bwana Kenyatta aidha</i>

Katika mifano ya jadwali 4.2.4.2, vifungu vyya maneno vilivyoandikwa kwa mlazo ndivyo vyeye makosa ya mpangilo wa maneno usiofuata sarufi ya Kiswahili. Katika

mifano (a) – (c) kosa la mpangilio wa maneno lililofanyika lilihusu vivumishi kutangulia nomino. Vivumishi *hii, kumi na sita*, na za *Kianzania*, vimetangulia nomino *leo, elfu, shilingi* wakati katika mfano (c), kiasi cha pesa zilizotajwa kimetangulia neno *milioni*. Kiutaratibu, tungo hizo zimekiuka sarufi ya Kiswahili. Kiuamilifu, kivumishi hufafanua (kuvumisha) nomino kwa hiyo kikifuata nomino kinaweza kufanya kazi hiyo kwa ufasaha zaidi kuliko kuitangulia. Aidha, kosa la mpangilio wa maneno lililofanyika kwenye (d) – (e) ni kuyaweka maneno mahali ambapo hayapaswi kuwa. Tunaona katika (d) kielezi cha mahali *hivi majuzi* kilipaswa kutangulia nomino *Moscow* au kufuata baada ya kitenzi hali katika mfano (e) neno *aidha* lilipaswa kutangulia *Bwana Kenyatta* kwani ni kiunganishi cha mwendelezo ambacho kinaonesha mwendelezo wa habari. Kwa hivyo, tungo hizo zilipaswa kuandikwa kama ifuatavyo:

- (a) Mapema leo *hii* ...
- (b) *Elfu kumi na sita* ...
- (c) ...thamani ya shilingi mil.210 za Kitanzania, ...thamani ya shilingi mil.56 za Kitanzania, ... thamani ya shilingi mil.25 za Kitanzania, ... thamani ya shilingi mil.12 za Kitanzania.
- (d) ... *hivi majuzi*, *Moscow* ilipeleka ndege.. au *Moscow* ilipeleka ndge *hivi majuzi*..., *Aidha*, *Bwana Kenyatta* ...

4.2.4.3 Kosa la Urudiaji wa Maneno

Urudiaji wa maneno au vifungu vyta maneno bila sababu ya msingi katika mawasiliano humchosha msikilizaji au msomaji. Hata hivyo, kanuni ya uchumi wa maneno huelekeza mwandishi au msemaji kutotumia maneno mengi yasiyo ya msingi ili kuleta ufasaha katika mawasiliano. Kurudiarudia maneno ambayo yamekwishasemwa bila sababu ya msingi ni kosa la kumuundo kwani sentensi hulazimika kuwa na mkururo wa maneno yasiyostahili. Data zilionesha kwamba

matini za TBC1, ITV na STAR TV ziliwa na kosa hilo. Kwa mfano, miongoni mwa makosa yaliyotajwa na wasailiwa lilikuwa ni kosa la urudiaji wa maneno. Wasailiwa baadhi walisema: ‘*makosa ya kurudia maneno* (MS5); *makosa ya kurudiarudia maneno ambayo hayana tija kwa wasilikizaji* (MS6).’ Kosa la kurudia maneno lilithibitishwa zaidi kutoka kwenye matini za habari zilizosomwa na kusikilizwa na mtafiti kama ifuatavyo:

Jedwali 4.2.4.3 Kosa la Urudiaji wa Maneno

Chombo cha Habari	Mifano ya Makosa
ITV	<p>(m) ...kuacha tabia hiyo mara moja <i>kwa kuwa kwa kufanya hivyo...</i></p> <p>(n)<i>shule</i> hizo ni za msingi na <i>shule</i> za awali...</p> <p>(o) <i>Lengo na dhumuni...</i></p> <p>(p) <i>Wachezaji wa umri chini ya umri</i> wa miaka 17...</p>
STAR TV	<p>(q) Waziri Hasunga <i>ameeleza hayo</i> leo tarehe 11 Agosti 2020 <i>ameyasema hayo wakati</i> akitangaza bei mpya ya Mbolea kwa msimu wa mwaka 2020/2021 <i>wakati akizungumza</i> na waandishi wa habari Jijini Dodoma.</p>

Kwa mujibu wa data ya jedwali 4.2.4.3 baadhi ya maneno au vifungu vilirudiwa bila sababu ya kufanya hivyo. Hata hivyo, urudiaji wa maneno hayo ulipoteza radha na ufasaha wa ujumbe uliokusudiwa kuwasilishwa kwa hadhira. Inaonekana katika (a), (b), (d), (e) kosa hilo lilihusu maneno *kwa, shule, umri, wakati* na kifungu cha maneno *ameeleza hayo/ ameyasema hayo* bila sababu yoyote. Aidha, kwa mfano (c) maneno *lengo na dhumuni* yaliandikwa yote kana kwamba ni maneno yenyewe kubeba maana tofauti. Kwa msingi huo basi, vifungu hivyo vya maneno vilipaswa kusomeka kwa usahihi kama ifuatavyo:

- (a) ...kuacha tabia hiyo mara moja kwa kuwa kufanya hivyo...
- (b) ... shule hizo ni za msingi na awali....

- (c) Lengo au madhumuni (ila si kuandika yote kwa pamoja)
- (d) Wachezaji wa umri chini ya miaka 17...
- (e) Waziri Hasunga ameeleza hayo leo tarehe 11 Agosti 2020 wakati akitangaza bei mpya ya mbolea kwa msimu wa 2020/2021 alipozungumza na waandishi wa habari jijini Dodoma.

Baada ya kuepuka urudiaji usio na uhitaji wowote katika mifano yetu inaoneka wazi kwamba vifungu hivyo vya maneno vina ladha, ufasaha, usanifu na mantiki ambayo inaufanya ujumbe kueleweka vizuri.

4.2.5 Makosa ya Kisemantiki

Semantiki ni taaluma inayohusika na uchunguzi wa maana katika viwango vyote vya lugha. Uchunguzi huo huhusisha maana pamoja na mantiki katika lugha kwa kuwa mantiki ndiyo msingi wa ujenzi wa maana inayoeleweka. Bila mpangilio wa kimantiki wa vijenzi vya maana, ujumbe wa matini husika hauwezi kueleweka ipasavyo na wakati mwingine unaweza kupotoshwa. Hivyo, makosa ya kisemantiki ni makosa yanayoweza kusababisha upotofu wa maana na mantiki katika lugha. Kwa kuzingatia nadharia ya UHK, mpangilio wa sentensi huonesha uamilifu wa kisemantiki wa vijenzi vyake kuhusu jambo linalolelezwa kutokana na mpangilio wa maneno, uhusiano wa kiuamilifu (kiima-kiarifu) au matumizi ya kauli tendi na tendwa. Hata hivyo, maana katika matini huchagizwa na ushikamani uletwao na vijenzi vyake. Ndiposa, Dijk (1988:12) anasema kuwa matini ni mfuatano wa sentensi ziletazo ushikamani na hivyo habari haijengwi na sentensi pwekepweke bali huambatana na vijenzi vingine viletavyo ushikamani. Kwa maana hiyo, mtafiti hupaswa kuchunguza vipashio vya ushikamani na uhusiano wa kisemantiki wa vipashio vya sentensi za matini za habari ili kupata fasiri au maana. Kwa kuongozwa

na msingi huu, mtafiti alichunguza vipashio vya matini za habari na kubaini uwapo wa makosa ya aina tatu ya kisemantiki.

4.2.5.1 Kosa la Utata

Utata wa kisarufi ni hali ya neno au sentensi kuwa na maana zaidi ya moja (Mushumbwa, 2018:67). Utata katika lugha hutokea pale mtu anapotumia maneno yenye maana zaidi ya moja na kumfanya msikilizaji au msomaji ashindwe kubaini ni maana ipi mzungumzaji au mwandishi alikusudia kuwasilisha. Matini ya habari inapokuwa na makosa ya utata basi maana itapotoshwa na ujumbe uliokusudiwa hautawafikia walengwa. Kutokana na uchunguzi wa matini za habari za TBC1, ITV na STAR TV mtafiti alibaini makosa ya utata kama mifano ifuatayo inavyodhahirisha hapa chini:

Jedwali 4.2.5.1 Kosa la Utata

Chombo cha Habari	Mifano ya Makosa
ITV	(a) <i>Watu waliofariki na Corona ...</i> (b) <i>Kuendelea kusalia klabuni hapo ...</i> (c) <i>Mashabiki Simba na Yanga wasiende na silaha uwanjani</i>
STAR TV	(d) <i>... ofisi ambayo imeteketea na moto ...</i>

Mifano iliyotolewa hapo juu ina utata. Utata huo ulisababishwa na waandishi kutumia maneno ambayo hayakupaswa kutumiwa. Maneno *na na salia* katika (a), (b) na (d) ndiyo yanayoleta utata kwenye tungo hizo yakisababisha maana zaidi ya moja bila kuelewa ujumbe uliodhamiriwa. Katika mfano (a) na (d) uwepo wa kihuishi *na unafanya* tungo hizo ziwe na maana mbili ambazo ni: *a) watu walikufa pamoja na ugonjwa wa korona/ofisi iliteketea na moto ukateketea; b) watu walikufa kwa sababu*

ya ugonjwa wa korona/ofisi iliteketezwa kwa moto. Kwa upande wa mfano (b), neno *kusalia* linafanya tungo iwe na maana mbili: *a) kuendelea kubaki kwenye klabu; b) kufanyia ibada katika eneo la klabu.* Katika mifano hiyo, kosa lililofanyika ni la utata wa kileksika kwa kuwa maneno ndiyo yaliyosababisha utata huo. Hii ni kusema kwamba waandishi walifanya kosa la kuteua maneno yasiyo sahihi. Kwa upande wa mfano (c) kosa lililofanyika ni la utata wa kimuundo kwani kirai *mashabiki Simba na Yanga...* ndicho kinacholeta utata katika sentensi kwa sababu ya udondoshaji wa kihusishi *wa*. Hii imesababisha tungo kuwa na maana mbili: *a) mashabiki wanaotajwa ni wa klabu za Simba na Yanga; b) mashabiki wanaotajwa wana majina ya Simba na Yanga.* Kwa msingi huo, tungo hizo zilipaswa kuwa na maneno pamoja na muundo sahihi ili kutokuwa na utata.

- (a) Watu waliokufa kwa korona ...
- (b) Kuendelea kubaki klabuni hapo ...
- (c) Mashabiki wa Simba na Yanga wasiende na silaha uwanjani
- (d) ... ofisi ambayo imeteketea kwa moto ...

4.2.5.2 Kosa la Kukosa Mantiki

Mantiki ni mtiririko wa fikra zilizopangwa ili kujenga hoja yenyе kukubalika (TATAKI, 2013:314). Makosa ya kimantiki ni kukosa utaratibu mzuri wa kufikiri hasa wakati wa kuzungumza na kuandika (Saluhaya, 2016: 121). Katika mawasiliano ya kila mara zikiwamo taarifa za habari, makosa ya kimantiki hufanywa na wawasilianaji. Kwa mujibu wa Odeo na Geoffrey (2008:120) makosa ya kimantiki husababishwa na upotofu wa mawazo au mpangilio wa maneno katika sentensi pamoja na watu kuandika au kuzungumza kwa kasi. Baada ya kuchunguza uhusiano wa uamilifu wa kisemantiki wa vijenzi vya tungo katika matini za habari, mtafiti

alibaini ukiukwaji wa mantiki katika uwasilishaji wa habari. Mifano ifuatayo inaonesha makosa ya kimantiki.

Jedwali 4.2.5.2 Kosa la Kukosa Mantiki

Chombo cha Habari	Mifano ya Makosa
ITV	(a) kirusi cha <i>Covid 19...</i> (b) ... <i>kuugua virusi vya corona...</i> (c) Wananchi <i>wametahadharishwa kutopokea</i> watu wasiowafahamu
STAR TV	(d) ... alimteua kuwa Waziri wake wa Bajeti, <i>wadhifa uliomstahili</i> kwa sababu Rose Raponda ni mchumi

Katika data (a) kutumika kwa neno *covid 19* kunaharibu mantiki ya ujumbe kwa kuwa neno hilo tayari ni jina la kirusi. Hivyo, kusema ‘kirusi cha *covid 19*’ kunamaanisha kuwa *covid 19* ni ugonjwa wenyе kirusi chake wakati ugonjwa ni *korona* na kirusi kinachosababisha ugonjwa huo ni UVIKO 19 (COVID 19). Vilevile, mfano (b) una hitilafu ya kimantiki kwa kuwa mtu huugua ugonjwa na wala si virusi vinavyosababisha ugonjwa. Korona ni ugonjwa ambao mtu anaupata kwa kuambukizwa na virusi vya UVIKO 19. Hivyo, tungo ilipaswa kuwa ugonjwa wa korona na si virusi vya korona. Kwa upande wa mfano (c), kosa la kimantiki lilisababishwa na matumizi ya kikanushi *kutopokea* wakati tayari neno *tahadharililishatangulia*. Kimantiki, ilipaswa kuwa ‘*wananchi wametahadharishwa kupokea watu...*’ kwani tendo lililofanya watahadharishwe ni upokeaji wa watu wasiowajua na si kutopokea. Kwenye mfano (d), kosa la kimantiki lilisababishwa na matumizi ya neno *kumstahili* likimaanisha kuwa *wadhifa* hustahili kumpata mtu badala ya mtu kustahili kupata *wadhifa* kwa kuwa *wadhifa* ni sifa. Biandamu hustahili kuwa na sifa

na wala si sifa zinazostahili kuwapata binadamu. Kwa hiyo, ilipaswa kuandikwa *wadhifa aliostabili*. Kutokana na ufanuzi huo, usahihi wa tungo hizo ulipaswa kuwa kama ifuatavyo:

- (a) kirusi cha korona ...
- (b) ...kuugua ugonjwa wa korona...
- (c) Wananchi wametahadharishwa kupokea watu wasiowafahamu
- (d) ... alimteua kuwa Waziri wake wa Bajeti, *wadhifa aliostabili* kwa sababu Rose Raponda ni mchumi.

4.2.5.3 Kosa la Kutokueleweka kwa Kilichoelezwa

Ili ujumbe uliokusudiwa uweze kuwafikia walengwa ipasavyo ni lazima kinachoelezwa kieleweke kwa ufasaha. Kutokueleweka kwa habari ni kikwazo cha mawasiliano. Hivyo, kutokueleweka kwa tungo au neno katika matini ni kosa la kimaana ambalo hufanywa na wazungumzaji au waandishi. Utafiti unaonesha wazi kuwa baadhi ya tungo katika matini za habari zilizotafitiwa ziliwu na makosa kadhaa ya kutokueleweka. Tazama mifano katika jedwali 4.2.5.3 hapa chini.

Jedwali 4.2.5.3 Kosa la Kutokueleweka kwa Kilichoelezwa

Chombo cha Habari	Mifano ya Makosa
ITV	(a) <i>Makosa yanayowakabili, Kula njama kutenda kosa, kughushi ...</i>
STAR TV	(b) <i>Kesi hiyo ya uchochezi namba 327 ya mwaka 2018, Zitto alikuwa anakabiliwa na mashtaka matatu ya uchochezi...</i> (c) <i>...ameona kutia nafasi kwa mtu mwingine kushiriki kwenye uchaguzi huo.</i> (d) <i>... siku tatu baada ya rais Keita, madarakani tangu 2013, kutimuliwa mamlakani ...</i>

Kwa mujibu wa data hii, baadhi ya vifungu vyatmaneno kwenye matini za habari vilione kana kutokueleweka kabisa. Hata pale mtafiti alipojaribu kuhusisha muktadha

wa matini nzima bado maana ya msingi iliyobebwa na vifungu hivyo haikueleweka. Kama inavyoonekana, kutokueleweka kwa vifungu hivyo kumesababishwa na mpangilio mbaya wa maneno (katika mfano (d)), kukosa mantiki (katika mfano (c)), ukosefu wa vishikamanishi (katika (a) na (b)). Hivyo, tungo hizo zilipaswa kuwa sahihi kama ifuatavyo:

- (a) Makosa yanayowakabili ni kula njama na kughushi ...
- (b) Katika kesi hiyo ya uchochezi namba 327 ya mwaka 2018, Zitto alikuwa anakabiliwa na mashtaka matatu ya uchochezi...
- (c) ...ameona kutangaza nia kwa mtu mwingine kushiriki kwenye uchaguzi huo.
- (d) ... siku tatu baada ya rais Keïta kutimuliwa madarakani tangu alipoingia 2013.

4.2.6 Mjadala

Hadi kufikia hapa utafiti umeweza kutimiza lengo mahususi la kwanza kwa kubainisha makosa ya kisarufi kwenye vyombo vya habari vya TBC1, ITV na STAR TV. Data zimechambuliwa kwa miongozo ya nadharia zilizoteliwa. Mihimili ya UHK ilimwongoza mtafiti kuchunguza, kubaini na kufafanua makosa ya kisarufi. Nadharia ya UM imesaidia katika kuwasilisha matokeo kwa kufuata hatua zilizopendekezwa. Katika hatua hii uwasilishaji na uchanganuzi wa makosa ya kisarufi umezingatia hatua mbili za UM ambazo ni kuainisha makosa na kuyasahihisha. Mtafiti ameyachambua makosa katika aina zake na kisha kuyachanganua kwa mifano anuwai huku akieleza usahihi wake.

van Dijk (1988:10-12) kupitia kiunzi cha UHK anasisitiza kuwa uchunguzi wa habari kisarufi uongozwe na uzingatie mifumo ya kanuni zinazojenga mifumo midogomidogo ya vitengo vya lugha. Kwa kuzingatia mwongozo huo, mtafiti alikusanya na kupata data za makosa ya kisarufi katika sampuli iliyoteuliwa. Makosa

hayo yalihusu vipengele vitano vya lugha – yaani msamiati, matamshi, maumbo, muundo na maana. Makosa ya kimsamiati yaliyobainika ni matumizi ya maneno ya Kiingereza, matumizi ya maneno yasiyostahili, kuandika maneno isivyo (kuunganisha na kutenga maneno), udondoshaji wa maneno, uchopekaji wa maneno na utumiaji wa maneno yasiyo sanifu. Hii ina maana kwamba wanahabari wa vyombo vya habari vya Tanzania hufanya makosa ya msamiati mara kwa mara. Matokeo haya yanafanana na madai yaliyotolewa na Mwansoko (1995), Conboy (2003), Mozūraitytē (2015), Ranasuriya (2015), Hassoon (2016), na Aditya na Amita (2017) kwa kutaja wachache. Watafiti hawa, kama ambavyo matokeo ya utafiti huu yanavyoonesha, nao walibaini kuwa vyombo vya habari katika maeneo walijotafiti hufanya makosa mbalimbali ya msamiati. Mathalani, Mwansoko (1995:8) anakiri kuwa magazeti ya Tanzania hutumia kiholela istilahi za Kiingereza wakati za Kiswahili zipo. Matokeo kama haya pia, yanajitokeza kwa Ranasuriya (2015: 265-271) kuwa, kuna makosa ya matumizi ya maneno ya Kiingereza katika redio za Sirilanka. Conboy (2003:50) anaonesha kuwa lugha yenyе maneno yasiyo sanifu na ya mtaani ndiyo msingi wa magazeti ya udaku nchini Uingereza. Mozūraitytē (2015: 20-37) anaripoti kuwa gazeti la Telegraph la Uingereza hufanya makosa ya udondoshaji wa maneno miongoni mwa mengine, kosa ambalo lilibainishwa na Hassoon (2016:1227) pia. Aidha, matokeo ya utafiti huu yanaoana na matokeo ya utafiti wa Aditya na Amita (2017) waliobainisha utumiaji wa maneno yasiyo sahihi katika vichwa vya habari.

Kadhalika, matokeo yameonesha kwamba makosa ya utamkaji wa maneno ya Kiswahili kwa ufasaha hufanyika katika utangazaji wa habari za TBC1, ITV na

STAR TV. Ushahidi katika §4.2.2 umethibitisha kuwa baadhi ya watangazaji walikosea kutamka maneno kama inavyopaswa. Lafudhi za luga zao zilisababisha utamkaji usio sahihi; uharaka katika usemaji nao ulichangia makosa kwenye matamshi. Kwa mfano, neno *katika* lilitamkwa *kalika /kalika/* badala ya */katika/*; neno *cha* lilitamkwa *chia /čia/* badala */ča/* na sauti */z/* ilitamkwa */ð/*. Matokeo kama haya yamewahi kuthibitishwa na King'ei (2000:52) aliyebainisha hilo kwenye vyombo vya habari vya Kenya. Pia, Mukhono (2008:103) aligundua kuwa vyombo vya habari vya Kenya hutumia matamshi yasiyosikika vizuri. Maina (2013) alibainisha kuwa magazeti na redio za Tanzania hufanya makosa ya matamshi kama kuandika sauti */th/* badala ya */dh/* pia watangazaji hutumia matamshi yenyе lafudhi mbaya (Maina, 2014). Huu ni ushahidi kwamba kuna makosa mengi ya utamkaji katika vyombo vya habari vya Kiswahili. Jambo hili linaonekana ni la kawaida na si kwamba linatokea kwenye vyombo vya habari tu; bali, hata kwenye mawasiliano ya kawaida kama ambavyo anasisitiza Fry (1969:69-73) kuwa mara nyingine mawasiliano ya mdomo hukumbwa na hitilafu ya utamkaji wa sauti, umbo na maneno. Hata hivyo, Fry (ameshatajwa) anasisitiza kuwa msikilizaji na msemaji makini hurekebisha hali hiyo inapotokea. Kwa hivyo, utafiti huu ni ushahidi wa wazi kwamba makosa ya utamkaji kwa vyombo vya habari vya Kiswahili yanatokea mara kwa mara na wahusika hawayafanyi marekebisheso kama alivyodai Fry (1961:71-73).

Watumiaji wa luga hufanya makosa ya kimofolojia pia. Kulingana na Shigini (2020) mtu huchukuliwa katenda kosa la kimofolojia pale anapotumia mofu isiyo sahihi katika nafasi ya neno isiyo sahihi. Pia, fasili hii inaweza kujumuisha udondoshaji wa mofu katika neno; uunganishaji wa maneno unaoweza kusababisha

neno lenye muundo usio sahihi (Shigini, 2020:105). Kile alichosema Shigini (ameshatajwa) kimethibitishwa na data za utafiti huu. Hii ni kwa sababu matini za habari zilizochunguzwa zilisheheni makosa ya kimofolojia yakiwamo ambayo Shigini (2020) ameyadokeza (rejea §4.2.3). Baadhi ya maumbo yalidondoshwa kimakosa kama ambavyo umbo {w} la utendwa lilivyodondoshwa kwenye neno *kutolea* badala ya *kutolewa*; umbo {o} la yambwa lilidondoshwa kwenye neno *walizuiliwa* badala ya *waliozuiliwa*; umbo {li} la njeo lilidondoshwa kwenye neno *lilokuwa* badala ya *lililokuwa*. Mbali na udondoshaji wa maumbo, data za utafiti huu zinathibitisha kosa la *uchopekaji* wa maumbo ambayo hayakupaswa kuwa sehemu ya mofolojia ya maneno hayo. Mathalani, tumeona kuwa umbo tamati {a} likiwa kwenye neno *zinaikabilia* badala ya *zinaikabili*; umbo {w} la utendwa likiwa kwenye neno *vinavyosababishwa* badala ya *vinavyosababisha*; na maumbo {ish-a} ya utendesha na tamati yakiwa sehemu ya mofolojia ya neno *kutoheshimisha* badala ya *kutoheshimu*. Kosa lingine la kimofolojia lillothibitika ni umoja na wingi. Matokeo yameonesha wazi kwamba wanahabari walishindwa kutambua kama maneno *ofisi*, *saa* na *dhaifu* hayana maumbo dhahiri ya wingi na hivyo kuyaandika na kuyatamka kama *maofisini*, *masaa* na *madhaifu*. Kwa mujibu wa matokeo haya ni wazi kwamba makosa ya kimaumbo hutokea mara kwa mara katika matangazo ya habari za televisheni za Tanzania. Hata hivyo, mbali na matokeo haya kuoana na ya Shigini (2020), pia yanalandana na ufanuzi wa Masebo na Nyangwine (2016:258) pale wanapotaja uongezaji wa viambishi kwenye mofolojia ya neno kama mionganoni mwa makosa ya kisarufi. Wataalamu hao wanasema kuwa baadhi ya wazungumzaji huongeza vitamkwa/viambishi mahali pasipohitajika. Wanatoa mifano kadhaa kama *amekwenda* badala ya *amekwenda*; *mtoto msafi* badala ya *mtoto safi*; na *msichana*

mhodari badala ya *msichana hodari*. Makosa haya vilevile yalitambulishwa na Nafees (2018:2197-2200) alipogundua kuwa watumiaji wa Kiingereza hufanya makosa ya kimaumbo ya matumizi mabaya ya mofu za njeo na za umoja na wingi.

Vilevile, matokeo yanaonesha kuwapo kwa makosa ya kisarufi ya kimuundo. Utafiti ulibainisha makosa ya upatanisho wa kisarufi ambapo baadhi ya tungo zilikosa upatano kati ya nomino zilizotawala sentensi na vipashio vilivyoandamana nazo (vitenzi, vihusishi, vivumishi) katika matini. Kwa mfano, tumeona katika §4.2.4.1 makosa kama *anga ya kimataifa* badala ya *anga la kimataifa* na *hizi mitambo* badala ya *hii mitambo*. Pia, makosa ya kimuundo yaliyothibitika ni mpangilio mbaya wa maneno katika tungo. Data inaonesha baadhi ya tungo za Kiswahili katika matini zilizochunguzwa zilikiuka kanuni ya kutangulia kwa nomino na kisha kufuatisha maneno mengine kwenye tungo kama *hii leo, kumi na sita elfu* badala ya *leo hii, elfu kumi na sita*. Zaidi, urudiaji wa maneno usio wa lazima ulidhihirika katika baadhi ya vifungu vyta maneno katika matini za vyombo vyta habari vilivyotafitiwa. Hata hivyo, matokeo haya hayapishani na matokeo ya tafiti zilizofanywa na watafiti wengine. Omoera (2008a: 62-77) alibaini kwamba redio za Naijeria zilifanya makosa ya lugha mbalimbali yakiwamo yale ya utotolojia na upatanisho wa kisarufi. Pia, Mwaura (2015) alithibitisha kutendeka kwa makosa ya mpangilio mbaya wa sentensi katika magazeti ya Kiingereza nchini Kenya. Hivyo, utafiti huu si wa kwanza kuibuka na matokeo yanayoonesha makosa mbalimbali ya kimuundo kama ilivyothibishwa na watafiti tulioarejelea hapa.

Kadhalika, utafiti uliweza kupata data iliyothebitisha makosa ya kisemantiki (kimaana) katika vyombo vyta habari vilivyochunguzwa. Data inaonesha kuwa

makosa ya kisemantiki yaliyofanyika yalikuwa ni ya utata, kukosa mantiki na kutokueleweka kwa tungo. Kwa upande wa utata, ilionekana kwamba wanahabari walitumia baadhi ya maneno yaliyoibua utata na miundo ya tungo ambayo ufasiri wake unaibua maana zaidi ya moja kwa hadhira. Hii imethibitishwa katika jedwali 4.2.5.1. Makosa ya kukosa mantiki yalikuwa sehemu ya makosa ya kisemantiki ambapo imethibitika wazi kwamba baadhi ya maneno, vipashio na miundo ya sentensi zilizounda matini za habari zilisababisha ukosefu wa mantiki. Mifano ya jedwali 4.2.5.2 imethibitisha baadhi ya tungo zilizo na mtiririko mbaya ya kimantiki. Hatimaye, kosa la mwisho lilikuwa ni kutokueleweka kwa tungo ambapo hadhira ya vyombo vya habari isingeweza kubaini nini matini hizo zilikuwa zikieleza. Kama utafiti huu, baadhi ya tafiti tangulizi zilifanikiwa kuibuka na matokeo kama haya. Mugambi, Mukuthuria na Kobia (2016a:173-188) waliibuka na matokeo ya uwapo wa makosa ya kisemantiki na kipragmatiki miongoni mwa mengine katika redio za KBC na Citizen za Kenya.

Makosa ya kisarufi yaliyothibitika kwenye utafiti huu, yalipatikana kutoka kwenye vyombo vya habari teule. Hata hivyo, si kwamba makosa yote yalipatikana kwa kila chombo bali kuna makosa ambayo yalipatikana kwa baadhi ya vyombo. Tafsiri yake ni kwamba japo utafiti huu ulijikita katika vipengele vitano vya sarufi ya Kiswahili, ila si kwamba kila televisheni ilifanya makosa ya vipengele vyote. Data zimeonesha kuwa makosa ya kisemantiki yalifanyika kwenye habari za ITV na STAR TV hali TBC1 iligundulika kuwa na makosa ya msamiati, matamshi, maumbo na miundo tu. Pia, makosa ya msamiati yalipatikana katika vyombo vyote isipokuwa utofauti upo kwenye aina za makosa ya msamiati. Imethibitishwa kwamba kosa la utenganishaji

wa maneno lilifanywa na ITV tu ilhali kosa la kuchopeka neno lilifanywa na vyombo vyta ITV na STAR TV pekee. Hadi kufikia hapa utafiti huu ulifanikiwa kutimiza lengo mahususi la kwanza. Uchambuzi unaofuata utajibu swalii la lengo la pili la utafiti.

4.3 Sababu za Makosa ya Kisarufi katika Habari za TBC1, ITV na STAR TV

Baada ya kubainisha makosa ya kisarufi kwenye vyombo vyta habari teule (rejea §4.2), kipengele hiki kinawasilisha na kuchambua matokeo ya lengo la pili ambapo, sababu za makosa ya kisarufi kwenye vyombo vyta habari vilivyotafitiwa zimebainishwa. Kulingana na hatua za nadharia ya UM, baada ya kuainisha makosa katika lugha, hatua inayofuata ni mtafiti kubainisha na kueleza sababu za makosa hayo. Sehemu hii inaonesha sababu za makosa ya kisarufi katika vyombo vyta habari vyta Tanzania. Data zilizokusanywa zilihusu TBC1, ITV na STAR TV ilhali taarifa nyingi za sababu za makosa ya kisarufi katika vyombo hivyo zilikusanywa kutoka kwa wasailiwa ambao ni hadhira na wanahabari wa vyombo hivyo. Hivyo, data zimeonesha kwamba sababu zifuatazo ni vyanzo vyta makosa ya kisarufi katika vyombo hivyo:

4.3.1 Kukosa Umahiri wa Lugha

Umahiri wa lugha ni ustadi wa kuitumia lugha kwa ufasaha na usahihi (TUKI, 1990:26; Massamba, 2007:144). Umahiri wa lugha hudhahirika katika mawasiliano ya mtumiaji wa lugha kwa kiwango cha hali ya juu. Ili umahiri uonekane ni wa kiwango cha juu, ni lazima uthibitishwe katika stadi nne za kusikiliza, kuzungumza, kusoma na kuandika (Masebo na Nyangwine, 2016:408). Kulingana na fasili hiyo, ni wazi kuwa kutokuwa na umahiri wa kutosha wa lugha ni sababu mojawapo ya

watumiaji wa lugha kufanya makosa ya kisarufi. Kwa mujibu wa data zilizokusanywa, ukosefu wa umahiri wa lugha ultajwa kuwa sababu ya makosa ya kisarufi kwenye habari za vyombo vyta habari vya Tanzania hususani TBC1, ITV na STAR TV. Wasailiwa walisema kuwa ukosefu wa umahiri wa lugha kwa wanahabari ni chanzo cha kufanya makosa ya kisarufi na makosa ya lugha katika kutangaza na kuandika habari. Kwa mfano:

Kutokuwa mahiri katika lugha ya Kiswahili. Mfano mwandishi wa habari anashindwa kuongea lugha kwa ufasaha kutokana na kutokusoma kwa umakini na kumudu misingi inayomwongoza mwandishi k.v kutumia neno ambalo kimsingi ni tafsiri sisisi badala ya kutumia ‘au’ mwandishi anatumia ‘eidha’ (MS14).

Kutokuwa mahiri katika lugha ya Kiswahili ni mionganini mwa sababu za vyombo vyta habari kufanya makosa ya lugha (MS3, MS 13).

Mifano hii ni baadhi ya majibu ya wasailiwa ambao walitaja kuwa ukosefu wa umahiri ni sababu ya makosa ya kisarufi kwenye vyombo vyta habari vya TBC1, ITV na STAR TV. Tumeona kuwa MS14 alijaribu kufafanua kwa welewa wake kuwa utamkaji mbaya (usomaji) wa maneno na sauti za Kiswahili unatokana na wanahabari kutomudu misingi ya lugha ambapo hali hiyo husababishwa na ukosefu wa umahiri wa lugha. Kwa mujibu wa maelezo ya MS14, uteuzi wa maneno yasiyo sahihi katika habari husababishwa na wanahabari kutokuwa mahiri katika stadi zote za lugha.

Kama ambavyo data kutoka kwa hadhira ilivyodhibitisha, pia wanahabari waliotaftiwa walikiri kuwa mionganini mwa sababu za makosa ya kisarufi kwenye vyombo vyta habari vya Tanzania ni kukosa msingi imara wa lugha ambao unamfanya mtu awe mahiri katika lugha. Majibu ya mwanahabari mmojawapo yanasema:

Kwanza ni msingi tulioanzia kujengewa kutoka shule ya msingi mpaka vyuoni, kama Kiswahili fasaha kingetumika katika kufundishia kuanzia msingi mpaka vyuoni nadhani wanahabari na watu wengine wangetumia na kuzungumza Kiswahili kwa ufasaha (MS16).

Mfano huu unaonesha maoni ya mwanahabari wa STAR TV akisema kuwa wanahabari pamoja na watumiaji wengine wa Kiswahili hushindwa kutumia Kiswahili fasaha kwa sababu ya kutokuwa na msingi bora wa lugha ambao ungewajengea umahiri wa kutumia lugha hiyo bila makosa. Hii inamaanisha kuwa kuna tatizo la kukosa umahiri wa lugha kwa watumiaji wa Kiswahili wakiwamo wanahabari wa Tanzania. Data ya makosa yaliyobainika imedhihirisha jambo hili. Mathalani, imethibitika kuwa baadhi ya maneno yasiyostahili yalitumika kueleza dhana badala ya maneno yaliyostahili kutumika (rejea § 4.2.1.2). Maana yake ni kuwa, mionganini mwa sababu nydingine, ukosefu wa umahiri wa lugha kwa wanahabari wa Tanzania wa vyombo vyaya habari vinavyotumia Kiswahili ni sababu ya msingi ya kufanya makosa ya kisarufi na makosa ya lugha kwa ujumla. Umahiri wa lugha si tu ni tatizo kwa wanahabari tu, bali hata kwa watumiaji wengine wa lugha kama asemavyo Idarus (2010: 173-187) kuwa, umilisi hafifu wa msamiati wa Kiswahili ni sababu mojawapo ya Waswahili kufanya makosa ya mara kwa mara wanapowasiliana. Hargie (2006:19), anathibitisha kuwa umahiri wa lugha ni chanzo kikubwa cha makosa ya lugha katika mawasiliano ambapo mtu mwenye umahiri wa kiwango cha juu hafanyi makosa mengi kama mwenye umahiri wa kiwango cha chini. Pia, King'ei (2000:50) alithibitisha ukosefu wa umahiri kwa wanahabari wa Kenya akisema kuwa mbali na athari ya lugha za kwanza kwa waandishi wa habari ambao sio wazaliwa wa Kiswahili; kuna mifino ya matumizi yasiyofaa ambayo hutokana na kiwango duni cha ujuzi wa msamiati mionganini mwa waandishi hao.

4.3.2 Athari ya Lugha ya Kwanza/Mama

Lugha ya kwanza ni lugha ambayo mtoto (mtu) alianza kuisikia, kuitamka na kuitumia wakati wa kulelewa kwake; inaweza kuwa lugha ya mama au lugha nyingine yoyote (BAKITA, 2015:551). Kwa wazungumzaji wanaotumia lugha zaidi ya moja huathiriwa na lugha hizo katika mawasiliano yao. Athari hiyo yaweza kuwa lugha ya kwanza kwa lugha ya pili au lugha ya pili kwa lugha ya kwanza. Kwa wanahabari wa Tanzania, Kiswahili ni lugha ya pili kwao baada ya lugha za makabila ambazo ndizo lugha mama zao. Kiswahili kimekuwa kikiathiriwa kwa namna mbalimbali na lugha za kwanza za watumiaji wake. Jambo hili lilitajwa na wasailiwa kama sababu mojawapo mionganoni mwa sababu za makosa ya kisarufi kwenye vyombo vya habari. Kwa mfano, majibu ya wasailiwa yalikuwa haya:

Kutangaza kwa kutumia lafudhi ya lugha za makabila kunakosababishwa na athari za lugha mama (kuwa mahiri katika lugha mama) husababisha habari kuwa na makosa ya matamshi ambayo yanaweza kumchanganya msikilizaji (MS3).

Athari za lugha mama za watangazaji wa TV huharibu ladha ya habari na kusababisha makosa ya kisarufi (MS7, MS8, MS10).

Ninadhani lugha zetu za makabila zinachangia sana baadhi ya wanahabari kushindwa kutamka maneno ya Kiswahili kwa ufasaha unaotakiwa. Kwa mfano, hata mimi huwa kuna wakati ninajikuta nakosea baadhi ya maneno kuyatamka nikijaribu kukwepa kuficha athari ya lugha yangu (MS19).

Hii ni mifano ya data zilizokusanywa juu ya sababu za makosa ya kisarufi katika vyombo vya habari vilivyotafitiwa. Ni ukweli kwamba lugha ya kwanza huathiri lugha ya pili au ya tatu ya msemaji wa lugha katika maandishi au mazungumzo. Makosa ya matamshi na maandishi yasiyo sahihi yamesababishwa na lugha mama kwa namna moja au nyingine. Katika §4.2.2 mfano (c) *watakaoudhuria*, (e) *kumalidhika*, sauti /h/ ilidondoshwa ikasikika /u/, kadhalika sauti /z/ ilitamkwa kama

/dh/. Hali hii hutokana na kwamba kuna baadhi ya lugha za Kibantu ambazo katika mfumo sauti wake hakuna sauti /h/ na /dh/. Hivyo, utamkaji utaathiriwa na mfumo huo; pale ambapo irabu itaambatana na sauti /h/, irabu husika itasikika na si /h/; na pale ambapo kuna sauti /z/, sauti hiyo itatamkwa kama /dh/ kwa lugha ambazo mfumo sauti wake hauna sauti /z/.

Hata hivyo, utafiti huu haukuwa wa kwanza kubaini kuwa lugha ya kwanza ya mtumiaji huathiri mawasiliano katika lugha yake ya pili. Hasa katika lugha ya Kiswahili, athari hizo zimethibitishwa na wataalamu kadhaa kama Odeo na Geoffrey (2008:117) na Masebo na Nyangwine (2016). Kwa kawaida, makosa ya kimatamshi yanatokana na athari za lugha mama (lugha ya kwanza). Kwa kuwa Kiswahili ni lugha ya pili kwa wazungumzaji wengi, hivyo lugha ya kwanza inakuwa na athari kubwa kwa mtu anayetumia lugha ya pili. Ufuatao ni ushahidi wa hilo.

Kwa kawaida makosa ya kuongeza vitamkwa/viambishi yanatokana na athari ya lugha mama (lugha ya kwanza), hasa athari ya Kisukuma au Kinyamwezi katika matumizi ya Kiswahili. Wasukuma na Wanyamwezi huongeza kitamkwa/kiambishi mwanzoni au mwishoni mwa neno wanapozungumza Kiswahili, ijapokuwa kosa hilo hufanywa hata na watu ambaa lugha hizo si lugha zao za kwanza (Masebo na Nyangwine, 2016:258).

Dondoo hili ni ushahidi kwamba baadhi ya makosa ya kisarufi katika Kiswahili husababishwa na lugha mama za wazungumzaji wake, hasa lugha za makabila yao. Lugha hizo ni kama Kihaya (k.m: **ngombe**, **ngambo** badala ya **ng'ombe**, **ng'ambo**); Kikurya (k.m: *chakura*, **bana** badala ya *chakula*, **bwana**); Kinyamwezi (k.m: *fiti* badala ya *viti*, *fyangu* badala ya *vyangu*) n.k.

4.3.3 Kasumba

Kwa mujibu wa BAKITA (2015:385), kasumba ni fikra za mtu zinazojengeka kutokana na kuathiriwa kielimu, kiutawala au kiutamaduni na jamii fulani iliyomtawala zinazomfanya athamini na kuzingatia utamaduni wa watu wengine huku akipuuza utamaduni wake; masalia ya fikra za kikoloni. Katika jamii za Kiafrika, zipo fikra zilizotawala miongoni mwa watu kwamba kila jambo linalohusishwa na wazungu basi ni bora kuliko mambo yetu ya ndani. Kwa upande wa lugha, kasumba imeathiri lugha za Kiafrika, kwani baadhi ya Waafrika wanaofahamu lugha za Ulaya, Amerika na Asia huzitumia lugha hizo hata pale ambapo wanawasiliiana na Waafrika wenzao wasiofahamu lugha hizo. Imekuwa kawaida kumkuta msomi akizungumza na mwenzake (hata kama si msomi) kwa kuchanganya lugha ya Kiswahili na Kiingereza. Tabia hii imeenea hadi kwa watu wa kawaida ambao hata hawana ufahamu wa lugha za kigeni lakini kutokana na maendeleo ya sayansi na teknolojia pamoja na utangamano, huchanganya baadhi ya maneno ya lugha za kigeni katika lugha ya Kiswahili. Kama ambavyo wasailiwa (MS8, MS9, MS15) walitaja kasumba kuwa sababu mojawapo ya kufanya makosa ya kisarufi katika vyombo vya habari, jambo hilo limethibitika kutoka kwenye data zilizokusanywa kutoka TBC1, ITV na STAR TV. Kosa la matumizi ya maneno ya Kiingereza kwenye habari za Kiswahili ikiwa dhana zilizotajwa zilikuwa na maneno ya Kiswahili, ni kasumba. Data katika mfano nambari §4.2.1.1) pamoja na maoni ya MS15 na MS18 ni ushahidi wa hilo.

Kasumba ya kuidunisha lugha ya Kiswahili inayotokana na dhana za ukoloni mamboleo na utandawazi. Kuona ufahari wa kutumia lugha ya kiingereza dhidi ya lugha ya Kiswahili (MS15).

Sababu nyingine sisi wanahabari tunakuwa na mazoea ya kutumia maneno ya lugha nyingine kama Kiingereza au lugha ya mtaani katika kutangaza kwa Kiswahili. Utakuta mtangazaji anasema ‘kutokana na ajali hiyo victims waliwahishwa hospitali’ au ‘shosti unapiga simu kutoka wapi’. Unaona kabisa kuwa hapa ni mazoea ya lugha ya mtaani na lugha ya Kiingereza (MS18).

Madondoo haya yanaonesha kuwa kuna kasumbu inayosababisha kutumia lugha ya Kiingereza au lugha ya mtaani kwa wanahabari. Pia, kuna kasumba ya kudharau lugha ya Kiswahili kama ambavyo MS15 anaeleza. Kasumba hii kwa mataifa ya Afrika hutokana na athari ya ukoloni pamoja na nguvu za kiuchumi na kisiasa za mataifa ya Ulaya na Amerika. Kwa hivyo, fikra za kuamini na kuthamini mambo ya wazungu ni kasumba inayotawala hadi masuala ya utamaduni, elimu, biashara, utawala n.k. Kwa mfano, athari hizi hujitokeza hadi kwenye mavazi, elimu tunayopata, lugha zao tunazofundishwa, bidhaa tunazonunua; na wakati mwingine, kupuuza kabisa mambo yote ambayo ni asili ya Kiafrika. Kwa upande wa lugha, nadharia ya ubeberu wa kiisimu imeathiri sana sera na mifumo ya lugha za Kiafrika hasa ambapo tunaona lugha za Ulaya, Amerika na Asia zinaenezwa kwa kasi katika jamii zetu tena pengine kwa mashinikizo kutoka mataifa hayo. Kasumba, kama sababu mojawapo ya makosa ya kisarufi katika vyombo vyaa habari inatokana na mitazamo ya ubaberu wa kiisimu iliyopandikizwa na kuota mizizi katika jamii za Kiafrika, Tanzania ikiwa mionganoni. Hali hii husababisha hata hadhi ya lugha za asili za Kiafrika kudharauliwa na kuchukuliwa kama lugha duni ambazo hazifai katika kuwasilisha mawazo ya kisomi na kisayansi kama anavyodai Kawonga (2017) kwamba:

Kiingereza ni lugha ya kigeni ambayo ni rasmi na inatumika kufundishia elimu ya sekondari, elimu ya chuo kikuu, shughuli za mahakama za rufaa na mahakama kuu, diplomasia, biashara na miamala ya kimataifa. Kwa kigezo cha dhima katika uhusiano wa

lugha hizi za makundi yote matatu, Kiingereza kina hadhi zaidi kuliko Kiswahili na lugha za Jamii.

Kulingana na dondo hili, ni wazi kwamba kasumba ndiyo msingi mkubwa wa kukikweza Kiingereza na kikitweza Kiswahili na lugha nyingine za Kiafrika. Kufanya Kiingereza kitumike katika shughuli muhimu na rasmi; kikitumia kufundishia na kukifundisha katika shule na vyuo vya elimu ya juu huwafanya wasomi wa Kiafrika (wanahabari wakiwa mionganini mwao) kutumia Kiingereza au maneno na mitindo ya uongeaji wa Kiingereza wanapokuwa wanazungumza na kuandika kwa lugha za Kiafrika. Hii ni sababu mojawapo ya kufanya makosa ya kisarufi katika vyombo vya habari.

4.3.4 Kutomudu Sarufi ya Kiswahili

Sarufi ya Kiswahili ni mfumo wa taratibu na kanuni zinazotawala matumizi sahihi ya matamshi ya maneno, maumbo ya maneno, miundo ya tungo na maana ya miundo ya Kiswahili (Taasisi ya Ukuzaji Mitaala [TUMI], 1988:28). Kanuni hizi zimeundwa ili kuwaongoza watumiaji wa Kiswahili kuzungumza, kuandika na kusoma Kiswahili sanifu na fasaha. Uzingativu wa kanuni za Kiswahili hufanya mawasiliano kueleweka kwa ufasaha. Kutojua au kuzingatia sarufi ya lugha husababisha makosa ya lugha katika mawasiliano. Hii ni sababu ya makosa ya kisarufi katika TBC1, ITV na STAR TV. Tukirejea makosa ya kimaumbo kama umoja na wingi, uchopekaji na udondoshaji wa maumbo ya maneno; makosa ya kimuundo kama upatanisho wa kisarufi na mpangilio usio sahihi wa tungo ni makosa ambayo yalifanywa na wanahabari kwa kukosa welewa wa sarufi ya Kiswahili. Mwanahabari anayemudu sarufi vizuri hawezi kufanya kosa la kusema au kuandika ‘*maofisini, madhaifu, masaa, jumbe, hizi mitambo na anga ya kimataifa.*’ Zaidi, majibu ya wasailiwa

yalitaja wazi kwamba kutozingatia sarufi ni chanzo cha makosa ya kisarufi kama inavyoonesha hapa chini.

Watangazaji wengi wa siku hizi hasa vijana hutoa habari mbali mbali na ukizisikiliza kwa makini au kuzisoma mitandaoni, utabaini kuwa kuna makosa mengi ya kisarufi. Kwa maoni yangu, makosa hayo ya kisarufi yanatokana na waandishi hao kutozingatia sarufi katika lugha husika (MS3).

Uelewa mdogo wa lugha ya Kiswahili, waandishi wengi wa habari hawana ufahamu juu ya vipengele anuai vyta sarufi ya lugha ya Kiswahili kwa hiyo huishia kufanya makosa ya matumizi mabaya ya lugha (MS15).

Wasailiwa walieleza kwamba kutokufuata kanuni za kisarufi za Kiswahili, ni chanzo cha makosa ya kisarufi kwenye vyombo vyta habari vilivyozunguza. Mifano inaonesha jinsi ambavyo wanahabari hutenda makosa ya kisarufi kwa sababu ya kutofuata kanuni na welewa mdogo wa kanuni za lugha ya Kiswahili. Kama ambavyo MS3 na MS15 wamefafanua, ni dhahiri kuwa kutomudu vizuri sarufi ya Kiswahili ni chanzo cha kukiuka kanuni na hivyo kusababisha makosa wakati wa utangazaji na uandishi wa habari za vyombo husika. Matokeo kama haya yaliwasilishwa na Wangari (2019) alipofafanua kuwa kutokuelewa kanuni za matumizi ya lugha na ujumuishaji wa kanuni za kisarufi ni baadhi ya sababu za makosa ya lugha. Ushahidi kama huu unatolewa na Odeo na Geoffrey (2008:117) kwamba kutofahamu kanuni za kisarufi ni sababu ya makosa ya lugha. Wanasema kwa kuwa Kiswahili ni lugha ya pili kwa watu wengi, wakati mwingine, watu hao hawakubobea vilivyo kwenye kanuni za kisarufi za lugha ya pili. Hii husababisha kuwapo kwa makosa ya kisarufi katika matumizi ya lugha (Odeo na Geoffrey, weshatajwa). Kulingana na Ayodele (1988) umilisi hafifu wa isimu ya Kiingereza ni

chanzo cha waandishi wa magazeti nchini Naijeria kufanya makosa ya matumizi ya kibainishi ‘the’.

4.3.5 Ufahamu wa Lugha zaidi ya Moja

Msemaji anapojuwa kuongea lugha zaidi ya moja (mlumbi) anaweza kufanya makosa ya kisarufi kutokana na kuathiriana kwa lugha anazofahamu. Mathalani MS11 aliandika ‘*kuwa umahiri wa lugha zaidi ya moja*’ ni sababu ya kufanyika kwa makosa ya kisarufi kwenye vyombo vya habari vya Tanzania. Kulingana na tajiriba ya mtafiti, ni kweli kuwa ujuzi wa lugha zaidi ya moja huchangia kwa namna moja au nyingine kufanya makosa ya kisarufi. Lugha ya kwanza huweza kuathiri lugha ya pili na lugha ya pili huweza kuathiri lugha ya kwanza na kumfanya mlumbi kufanya makosa. Matokeo yameonesha kuwa lugha ya kwanza imesababisha baadhi ya makosa ya kisarufi katika channeli zilizotafitiwa. Ulumbi huweza kuwa chanzo cha makosa ya matamshi, miundo na maana. Kwa mfano, uchanganyaji wa maneno ya Kiingereza katika matini za habari za Kiswahili (rejea §4.2.1.1) na kosa la mpangilio wa maneno usio sahihi (rejea § 4.2.4.2) yamesababishwa na ulumbi wa wanahabari wa vyombo teule. Hii ni kwa sababu wanahabari wa TBC1, ITV na STAR TV wengi wao ni wajuzi wa lugha tatu: Lugha za makabila yao, Kiswahili na Kiingereza. Wamezaliwa na kukulia katika jamii lugha za makabila yao, wamesoma katika shule na vyuo vinavyotumia Kiswahili na Kiingereza katika ufundishaji na ujifunzaji wa masomo. Hivyo, ni dhahiri kuwa makosa ya kutumia maneno ya Kiingereza kama *newsroom, live, gap, visa* n.k badala ya *chumba cha habari, mbashara, pengo, viza*; makosa kama *hii leo* badala ya *leo hii, kumi na sita elfu* badala ya *elfu kumi na sita* n.k; utamkaji wa *aidha* kama /ɛiða/ badala ya /aiða/, ni baadhi ya makosa ya kisarufi

yaliyofanywa na wanahabari kwa sababu ya kuwa ufahamu wa lugha ya Kiswahili na Kiingereza. Kwenye lugha ya Kiingereza, kivumishi hutangulia nomino kama *beautiful girl*, *bad behavior* (*mzuri msichana*, *mbaya tabia*) badala ya *msichana mzuri*, *mvulana mbaya*. Athari hiyo iliathiri miundo ya sentensi za Kiswahili zilizotolewa na wanahabari. Ulumbi kama sababu ya makosa ya kisarufi katika lugha ulibainishwa na Ojetunde (2013) kuwa, kwa sababu ya Wanajeria kufahamu lugha zaidi ya moja (lugha asili zao na Kiingereza), hufanya makosa ya uchanganyaji msimbo, upanuzi wa maana na uhamishaji wa maana. Katika matini za mawasiliano alizochunguza, Ojetunde (2013:263) anadai kwamba uchanganyaji wa msimbo ulihusisha zaidi lugha ya Kiyoruba na Kiingereza.

4.3.6 Ukosefu wa Taaluma ya Lugha kwa baadhi ya Wanahabari

Taaluma ya lugha humfanya mtu awe na kiwango fulani cha welewa juu ya masuala mbalimbali ya lugha hasa kanuni zinazoongoza matumizi ya lugha. Mtu aliyesoma isimu ana uwezo wa kutumia lugha pasipo kufanya makosa mengi kwani anajua miongozo ya matumizi ya lugha kinyume na mtu asiye na taaluma hiyo. Wanahabari wengi wana taaluma ya habari (utangazaji au uandishi) kuliko taaluma ya lugha. Hata pale ambapo baadhi wamebahatika kusoma taaluma ya lugha hawaisomi kwa kiwango cha juu bali hufundishwa kwa kiwango cha utangulizi tena ikiwa ni kozi fupi. Data zimeonesha kuwa ukosefu wa taalauma ya lugha ni chanzo cha makosa ya kisarufi katika vyombo vya habari vya Tanzania. Kwa mfano:

Kutokusomea taaluma ya lugha ni chanzo kwa watangazaji wa Tanzania kukosea mara kwa mara maana hawana welewa mzuri wa isimu ya lugha (MS5).

Kutokusomea taaluma ya lugha ambayo wanaitumia katika kutangaza habari huleteleza makosa ya hapa na pale kwenye habari wanazotoa kwenye vyombo vyao vya habari (MS6).

Sambamba na majibu ya hadhira yaliyonukuliwa hapa, mwanahabari kutoka ITV/Radio One ambaye ni mwendeshaji wa vipindi vya Kiswahili kama *Kumepambazuka Kiswahili* alikuwa na majibu sawa na hadhira kuhusu sababu za makosa ya kisarufi katika vyombo vya habari vya Tanzania aliandika yafuatayo:

*Kukosa elimu kuhusu lugha ya Kiswahili ni sababu ya makosa ya lugha kwa wanaidhaa. Wanahabari wengi wamekuwa wakiichukulia Lugha ya Kiswahili kuwa ni jambo jepesi kwa kuwa wamezaliwa wanazungumza Kiswahili hiyo hawaipi kipaumbele katika kujifunza. Lugha ya Kiswahili ni taaluma kama ilivyo taaluma nyingine zinazofundishwa katika ngazi tofauti. Hivyo basi, kutokuwa na taaluma hii ya Lugha ya Kiswahili imekuwa ni sababu ya kufanyika kwa makosa katika utendaji kazi wa wanahabari. Wanahabari wamekuwa wakijiundi maneno yao kiholela ili kukidhi matakwa ya kazi zao. Mfano **mzeiya, jombaa, skani, kitaa, na mengineyo mengi.** Kitendo cha kukosa elimu ya Lugha ya Kiswahili kwa wanaidhaa kinawafanya washindwe kutofautisha muktadha, kwamba muda upi niongee nini na je naongea na nani, lakini pia kushindwa kutofautisha lugha ya mtaani na lugha rasmi achilia mbali lugha ya mazungumzo na lugha ya maandishi (MS17).*

Maoni hayo yanaonesha kukiri kwa mwanahabari kuwa baadhi ya wanahabari wa TBC1, ITV na STAR TV hufanya makosa ya kisarufi kwa kuwa hawana taaluma ya lugha. Kukosa taaluma ya lugha ni chanzo cha makosa ya kisarufi kwenye vyombo vya habari kwa sababu wanahabari wengi husomea taaluma ya habari na si lugha. Kama wanahabari hao wangelikuwa na taaluma ya lugha wangeweza kwa kiasi fulani kuepuka makosa hayo. Mathalani, makosa ya upatanisho wa kisarufi, kutumia neno lisilostahili, udondoshaji na uchopekaji wa vipashio, umoja na wingi yasingelitokea sana katika habari zilizochunguzwa. Ukosefu wa taaluma ya lugha kama sababu ya makosa ya kisarufi kwenye vyombo vya habari imewahi

kubainishwa na wataalamu wengine pia. Kwa mfano, Nsereka (2012) alichunguza makosa ya kisarufi, sababu na utatuzi wake katika magazeti ya Naijeria, na kubaini kuwa kutofundishwa vema taaluma ya lugha hasa sarufi ni sababu ya msingi kwa waandishi wa magazeti kuandika habari zenyé makosa ya kisarufi.

Kama ambavyo data za lengo la pili zilivyochanguliwa, makosa ya kisarufi yaliyobainishwa kutoka kwenye chaneli zilizotafitiwa yanasaababishwa na sababu zilizochanganuliwa kwenye §4.3. Hivyo, swali la pili la utafiti huu limepatiwa majibu na kukamilisha lengo la pili. Sehemu inayofuata inawasilisha na kuchambua data za lengo la tatu zinazojibu swali mahususi la tatu la utafiti.

4.4 Hatua za Kuchukuliwa ili Kuepuka Makosa ya Kisarufi katika Habari za TBC1, ITV na STAR TV

Lengo mahususi lingine lilikuwa ni kubainisha hatua zinazoweza kuchukuliwa ili kuepuka makosa ya kisarufi katika vyombo vya habari vya Tanzania. Katika kipengele hiki, zinawasilishwa data za lengo la tatu la utafiti. Data zilikusanywa kutoka kwa wasailiwa. Wasailiwa walitakiwa kueleza hatua ambazo wanafikiri zinaweza kuchukuliwa na wanahabari ili kuepusha makosa ya kisarufi kwenye vyombo vya habari tafitiwa. Yafuatayo ni matokeo ya lengo la tatu la utafiti huu:

4.4.1 Ufundishaji wa Taaluma ya Lugha (Sarufi) ya Kiswahili kwa Wanahabari

Taaluma ya lugha hasa isimu huimarisha uwezo wa watumiaji wa lugha kumudu kanuni na taratibu za matumizi ya lugha na kuwaepusha kufanya makosa ya kila mara. Mbinu mojawapo ya kumfanya mtu amudu vema lugha yake, ni kumwelekeza juu ya kanuni za kisarufi. Hii husaidia kwa njia moja kupunguza makosa ya lugha.

Data zilibainisha kuwa baadhi ya wanahabari wa Tanzania hawana umahiri wa kutosha wa sarufi ya Kiswahili, kwa sababu hiyo, hufanya makosa ya kisarufi katika utangazaji na uandishi wa habari. Hivyo, hatua mojawapo iliyopendekezwa na watafitiwa ni kufundishwa kwa taaluma ya lugha kwa wanahabari. Dondoo lifuatalo ni baadhi ya mapendekezo ya watafitiwa.

Katika vyuo vinavyotoa astashahada, stashahada, shahada, shahada ya uzamili na shahada ya uzamivu wapewe mafuzo yanayohusu sarufi ya Kiswahili na matumizi yake ili wawe bora watakapopata fursa ya kuwa watangazaji na waandishi (MS15).

Watangazaji na waandishi wa habari wasomee taaluma ya lugha ili kuwasaidia kujua kanuni zinazotawala Kiswahili, kwa maana hiyo wataweza kupunguza makosa yanayotokea kutokana na kutokuwa na taaluma ya lugha (MS5).

Madondoo hayo ni mfano wa data zilizopendekeza kwamba ili kuepuka makosa ya kisarufi kwenye utangazaji na uandishi wa habari, ni lazima wanahabari wapate taaluma ya lugha ya Kiswahili. Pendekezo hili linamaanisha kwamba kupata elimu ya lugha kutawafanya wanahabari kufahamu kanuni za kisarufi zinazoongoza lugha ya Kiswahili; jambo ambalo litapunguza makosa ya lugha hasa ya kisarufi, hivyo kutoa habari zisizo na makosa. Maoni ya MS15 yanaeleza wazi kwamba endapo taaluma ya lugha ya Kiswahili itatolewa kwa wanafunzi wa habari, wataweza kutumia lugha kwa ufasaha na kwa usanifu wapatapo fursa ya kuajiriwa katika vyombo vya habari. Mapendekezo hayo ya hadhira yanaoana maoni ya wanahabari ambapo wawili miongoni mwao, walisema yafuatayo:

Kubadili mfumo wa ufundishaji kuanzia msingi mpaka vyuoni kwa kufundisha somo la Kiswahili tena Kiswahili fasaha na kuwapatia elimu zaidi ya lugha wanahabari katika mafunzo ya taaluma yao kutasaidia sana kuondoa haya makosa yanayoharibu kiswahili (MS16).

Wanahabari tuache kufanyakazi kwa mazoea, tuingie darasani tuisome lugha ya Kiswahili ili tufanye kazi zetu kwa ufasaha, tuachane na ile dhana kwa kuwa nazungumza Kiswahili basi hakuna haja ya kujifunza Kiswahili. Lugha ya Kiswahihili ni taaluma kama zilivyotaaluma nyingine nizofundishwa kila uchao (MS17).

Data inaonseha kuwa MS17 anawataka wanahabari wenzie kuacha kasumbu ya kudharu Kiswahili badala yake wajifunze lugha hiyo kama taaluma ili kuepuka makosa yanayoweza kuzuilitika endapo wakiwa na taaluma ya luga ya Kiswahili. Linalopendekezwa hapa ni jambo umuhimu katika ulimwengu wa sasa kwa sabau tangu kugunduliwa kwa taaluma katika maisha ya wanadamu, ujinga umekuwa ukiondolewa kwa taaluma mbalimbali. Kwa upande wa lugha, isimu imekuwa ni taaluma msingi ya kufuta ujinga wa kanuni za lugha husika. Kwa wanahabari ambao hufanya makosa ya lugha kwa sababu ya kutomodu sarufi ya lugha, taaluma ya lugha ni suluhisho sahihi. Watafiti wa masuala ya lugha katika habari wamependekeza kwamba ufundishaji wa sarufi au taaluma ya matumizi ya lugha ni mojawapo ya utatuzi sahihi wa makosa ya kisarufi kwenye vyombo vyahabari. Omoera (2008a: 70-72) anapendekeza kwamba ili kuepuka makosa ya lugha katika magazeti ya Naijeria, vyombo vyahabari husika vinapaswa kuwashimiza wafanyakazi wake kutumia lugha fasaha, kuwatafutia mafunzo ili waimarishe ujuzi wa kanuni za lugha. Kwa upande wa TBC1, ITV na STAR TV ufundishaji wa taaluma ya lugha utasaidia kuepuka makosa ya msamati kama utumiaji wa maneno yasiyofaa, utenganishaji na uunganishaji wa maneno; makosa ya kimatamshi; makosa ya kimaumbo kama udondoshaji na uchopekaji wa vipashio visivyostahili, umoja na wingi; makosa ya kimuundo kama upatanisho wa kisarufi, urudiaji wa maneno na mpangilio usio sahihi; makosa ya kisemantiki kama ukosefu wa mantiki na kutokueleweka kwa tungo.

4.4.2 Utoaji wa Semina za Matumizi Sahihi ya Lugha

Kwa mujibu wa BAKITA (2015:917) semina ni mukutano unaohusisha waelimishaji na waelimishwaji, ambao hufanyika ili kujifunza, kuchambua na kufafanua suala fulani kwa ajili ya utekelezaji wake mzuri. Kwa fasili hiyo, semina mbalimbali za matumizi ya lugha pamoja na kanuni zake ni jambo muhimu katika kuimarisha umahiri wa lugha ya Kiswahili kwa wanahabari wa Tanzania. Kulingana na data, utoaji wa semina juu ya matumizi sahihi ya lugha kwa wanahabri, ni hatua mwafaka ya kuchukuliwa ili kuepuka makosa ya kisarufi kwa channeli zilizotafitiwa na vyombo vyta habari vya Tanzania kwa ujumla. Ushahidi kutoka kwa hadhira unaonesha hivyo.

Wamiliki wa vyombo hivi kupewa semina mbalimbali kuhusu matumizi sahihi ya lugha kwa vyombo vya habari, hii itawezesha kusaidia kupunguza lugha za matusi kwenye vyombo vya habari (MS11).

Semina mbalimbali au warsha za Kiswahili zishirikishe watu wa vyombo vya habari ili waweze kupata nafasi ya kujifunza lugha kwa ufanisi kuweza kuepuka kufanya makosa (MS8).

Kuwepo kwa warsha au makongamano yanayohimiza matumizi sahihi ya lugha katika vyombo vya habari kutasaidia kwa kiwango fulani kuepuka makosa ya lugha (MS3).

Aidha, maoni ya mwanahabari (MS16) yalipendekeza jambo hilohilo kama lilivyopendekezwa na hadhira akisema kuwa “mabaraza ya Kiswahili yazidi kutoa elimu zaidi kuhusu matumizi sahihi ya lugha ya Kiswahili ili kuwasaidia wanahabari kuepuka makosa.” Kwa mujibu wa madondoo haya, data zilipendekeza kwamba utoaji wa semina na warsha kwa wanahabari ni suluhisho sahihi la kupunguza makosa ya kisarufi katika vyombo vya habari vya Tanzania. Hadhira wa vyombo vya habari na wanahabari walioitaftiwa, walipendekeza kwa wingi suala la utoaji wa semina kama mifano inavyoonesha. Semina ni mafunzo ya kutoa au kuimarisha maarifa. Mafunzo hayo hutolewa kwa watu ambao huhitaji kupata ujuzi wa jambo

fulani. Mtu anapofanya makosa ya kisarufi ya mara kwa mara anahitaji kusaidiwa kwa kupewa mafunzo juu ya matumizi sahihi ya lugha.

Semina itakuwa ni njia sahihi ya kupunguza makosa ya lugha. Semina hutolewa kwa nia ya kukazia maarifa, kujenga ujuzi na kukumbushia yale ambayo yamesahaulika. Kuwa na taaluma ya lugha peke yake hakutoshi kwani binadamu husahau asipojikumbushia jambo alilojifunza kwa muda mrefu. Kama waajiriwa wa vyombo vyta habari, wanahabari watanufaika na semina za lugha katika utangazaji kwa kuwafanya waimarike katika matumizi ya lugha, na hivyo kutumia Kiswahili sanifu na fasaha. Jukumu hili linapaswa kutimizwa na wanahabari wenyewe, waajiri wao kwa kushirikiana na mamlaka zinazoratibu matumizi ya Kiswahili. Taasisi zinazoratibu na kusimamia matumizi ya Kiswahili nchini zina wajibu wa kutoa mafunzo, kusositiza na kuwashimiza watumiaji wa Kiswahili wakiwamo wanahabari kutumia Kiswahili kinachofuata kanuni. Taasisi kama TATAKI na BAKITA zinawajibika kutoa semina na mafunzo ya matumizi sahihi ya Kiswahili kwa wanahabari ili watoe habari zisizo na makosa ya kisarufi. Serikali kupitia taasisi nyine inalo jukumu la kusimamia wanahabari kupata mafunzo muhimu ya kuimarisha matumizi sahihi ya Kiswahili kama alivyopendekeza MS13 kwamba *serikali kwa kushirikiana na Baraza la Kiswahili la Taifa (BAKITA) kuendelea kutoa mafunzo, warsha na semina mbalimbali kuhusu matumizi sahihi ya Kiswahili.* Mafunzo hayo yanapaswa kuwa ya mara kwa mara: ya ndani na nje. Ili kutimiza hilo, waajiri wanapaswa kuwapatia nafasi wanahabari kuimarisha ujuzi katika lugha ili kutoa habari kwa lugha sanifu na fasaha. Suluhisho hili kwa vyombo vyta habari, limetolewa pia na Omoera (2008b), anaposhauri juhudii kuwekwa na vyombo vyta habari.

Naijeria kuwapatia waandishi semina za kuwanoa ubongo, kuwashimiza wasome vitabu na vyanzo mbalimbali kuhusu uandishi na sarufi.

4.4.3 Kuajiri au Kutumia Wataalamu wa Lugha katika Vyombo vya Habari

Mtaalamu ni mtu mwenye ujuzi, taaluma au ustadi wa fani au jambo fulani maalumu; ni mtu aliyebobea katika taaluma fulani (BAKITA, 2015:716). Lugh nayo ina wataalamu wake kama wanaisimu na wasomi wengine wa masuala mbalimbali ya lugha na mawasiliano. Wataalamu hutafiti na kushauri juu ya mambo mbalimbali ya lugha ikiwa ni pamoja na kuchanganua matumizi ya lugha katika jamiilugha. Uchunguzi wao huenda sambamba na ushauri juu ya mambo mbalimbali ya lugha. Data zinaonesha kuwa kuajiriwa kwa wanahabari wenyewe taaluma ya lugha au wataalamu wa lugha ambao si wanahabari, ni njia mwafaka ya kuepuka makosa ya kisarufi katika vyombo vya habari vya Tanzania hususani channeli zilizochunguzwa.

Mimi naona kuwa usfaulu mzuri wa lugha ya Kiswahili kiwe kigezo cha kuajiriwa. Edapo kila mtangazaji au mwandishi wa habari anayeajiriwa atakuwa amesoma Kiswahili na kusfaulu kwa kiwango kizuri, ni wazi makosa ya ovyo ovyo hayatasikika kwenye vyombo vyaa haari (MS12).

Wahariri wanaoajiriwa wawe mahiri katika lugha ya Kiswahili. Umahiri huo wataupata kwa kufundishwa vyuoni na vyombo husika viajiri wahariri walio mahiri katika lugha (MS1).

Kutumia wataalamu wa lugha katika kueleza istilahi sanifu za Kiswahili kwa dhana za kisayansi na teknolojia ni suluhisho litakalopunguza baadhi ya makosa ya kuchanganya lugha za kigeni (MS10).

Mifano hii ni pendekezo la kuvitaka vyombo vya habari vya Tanzania kuajiri au kutumia watu ambao tayari ni wanataaluma ya lugha ya Kiswahili ili kuepuka makosa ya kisarufi. MS12 alipendekeza kuwa ufaulu wa Kiswahili uwe kipaumbele cha kupata wanahabari. Hii inamaanisha kuwa ili kuwapata wataalamu wa Kiswahili

ni lazima mwanahabari awe amefaulu vizuri somo la Kiswahili kama ushahidi wa kumudu vema matumizi sahihi ya lugha. Kwa upande wa MS1 anapendekeza kuwa wahariri wa vyombo nya habari wanapaswa kuwa ni wajuzi na mahiri wa lugha pia. Tafsiri yake ni kwamba, kuwa na ujuzi wa uhariri wa habari hakutoshi kumfanya mhariri aruhusu habari zisizo na makosa ya kisarufi kwa kuwa hana ufahamu wa kina juu ya kanuni za lugha. MS 10 anaamini kuwa wataalamu wa lugha wakitumiwa watasaidia kufanya tafsiri mbalimbali za maneno ya kigeni ambayo yanepotoshwa tafsiri zake au kutumia maneno ya lugha nyingine kama katika § 4.2.1.1. Pendekazo hili pia limetolewa na mmoja wa wanahabari waliosailiwa akisema kuwa “kuna haja ya idhaa zetu kuajiri wanahabari ambao wamebobe kwenye taaluma ya lugha kama ambavyo kuna wanahabari waliobobe kwenye maeneo mengine ambapo watu hao watasaidia sana kukosoa matangazo na habari zenye makosa (MS18)”.

Wataalamu wa lugha ya Kiswahili wakiwa katika vyombo nya habari watasaidia kukosoa na kuelekeza matumizi sahihi ya lugha; watatafuta istilahi na maneno sahihi yanayofaa kutaja dhana zinazolengwa kuwasilishwa; watapitia na kurekebisha makosa ya lugha yote na kisha kuruhusu habari zichapishwe na kutangazwa bila makosa ya kisarufi. Vyombo nya habari vinaweza kutuma maombi ya wataalamu wa lugha kutoka katika taasisi zinazoratibu na kusimamia masuala ya lugha kama TATAKI na BAKITA/BAKIZA ambapo taaluma ya lugha hufundishwa. Pia, vyuo nya habari vinapaswa kufundisha somo la lugha hasa kwa kumakinikia somo la sarufi na matumizi sahihi ya lugha. Jambo hilo litasaidia wanahabari wanaohitimu kuwa na ujuzi na taaluma ya lugha na hata wanapoajiriwa wakaelekeze matumizi sahihi ya lugha pamoja na kuhakikisha habari zinazotolewa hazina makosa ya lugha.

4.4.4 Kutungwa kwa Sheria Zinazolinda Matumizi Sahihi ya Lugha

Matokeo yameonesha kuwa kuna haja ya kutungwa kwa sheria za kuthibiti matumizi yasiyo sahihi ya lugha ya Kiswahili ili kuepusha makosa ya lugha ya makusudi kwa watumiaji wa Kiswahili wakiwamo wanahabari. Data zilizokusanywa kutoka kwa watifiwa zinaonesha kama ifuatavyo:

Kanuni na taratibu za kisheria ziwekwe ili kuweza kuondokana na tatiozo la matumizi yasiyo sahihi katika lugha pindi vyombo vya habari vinapotoa matangazo kipindi cha utoaji wa matangazo kwa lugha ya Kiswahili (MS6).

Kuwepo sheria zinazoongoza waandishi wa habari kutumia Kiswahili fasaha na sanifu (MS14).

Taasisi zinazosimamia mawasiliano na habari ziweke kanuni zinazowabana waandishi kutumia lugha inayofaa kulingana na muktadha wa mawasiliano (MS15).

Matokeo yanaonesha kuwa watafitiwa walipendekeza kutungwa kwa sheria madhubuti zinazolinda na kuongoza matumizi sahihi ya lugha ya Kiswahili. Tafsiri yake ni kwamba ipo tabia mionganoni mwa watumiaji wa lugha kuongea kwa kukiuka kanuni za matumizi sahihi kwa matakwa yao. Uigaji, majivuno, kutojali, ulimbukeni na mtindo binafsi wa mzungumzaji husababisha makosa ya lugha. Mazoea kama hayo huvuka mipaka na huathiri matumizi ya lugha katika maeneo ambayo lugha rasmi huhitajika kama kwenye vyombo vya habari. Kwa mfano, tamko *mambo* kama salamu halikuwa tamko lilitumika rasmi kwenye mawasiliano ya salamu bali lilianzia mtaani kama msimu. Hata hivyo, tamko hilo limeathiri kundi kubwa la watumiaji wa Kiswahili kiasi kwamba linatumika hata kwenye mawasiliano rasmi kama vikao na mikutano. Mara nyingi tumekuwa tukiwasikia viongozi wakihutubia umma hadharani na kupitia vyombo vya habari wakisalimia kwa tamko hilo. Hali kama hii inajitokeza vilevile kwenye matangazo ya vyombo vya habari vya Tanzania

hasa kwa watangazaji vijana. Kwa hiyo, kutungwa kwa sheria za kulinda matumizi sahihi ya Kiswahili kwa watumiaji wote kutapunguza makosa ya kisarufi kwenye vyombo vya habari kwa sababu watumiaji wa Kiswahili watakuwa makini kutofanya makosa ya lugha ya holelaholela ili wasichukuliwe hatua za uharibifu wa lugha kimakusudi.

4.4.5 Kufanya kwa Uhariri wa Kina

Baadhi ya makosa ya lugha kwenye vyombo vya habari vya Tanzania hufanya kutohana na uzembe katika kuhariri habari kwa makini (Massamba, 1995:8). Kukosa umakini katika kuandika na kuhariri habari ni chanzo cha makosa ya kisarufi katika vyombo vya habari vya Tanzania kama ambavyo data zimeonesha. Hivyo, ili kupunguza makosa yatokanayo na uzembe katika kuandika na kuhariri, umakini unahitajika. Hili ni mionganoni mwa masuluuhisho yaliyopendekezwa. Mathalani, MS 14 aliandika kwamba *wahariri watilie mkazo matumizi sahihi ya Kiswahili sanifu*. Endapo waandishi na watangazaji watakuwa makini kwenye kuandika na kuandaa habari zao, wahariri nao wakafanya uhariri wa kina bila shaka makosa kama utenganishaji na uunganishaji wa maneno hayatabainika kwenye habari ambazo zinachapishwa.

Hadi kufikia hapa, data zimeweza kujibu swalii mahususi la tatu kwa kuonesha njia zinazoweza kuchukuliwa na wanahabari wa vyombo vya habari vya Tanzania ili kuepuka kufanya makosa ya kisarufi katika utoaji wa habari. Kwa kufanya hivyo, malengo yote matatu ya utafiti huu yanakuwa yamefikiwa.

4.5 Muhtasari wa Sura

Lengo kuu la sura hii liliwa ni kuwasilisha na kuchambua data za utafiti zilizokusanywa kutoka uwandani. Katika kutimiza lengo hili, data zimewasilishwa, zikachanganuliwa na kutafsiriwa kwa ushahidi uliothibitika. Uchanganuzi na uwasilishaji wa data katika tasnifu hii, umezingaia mkabala wa kitaalumu pamoja na misingi ya nadharia za UHK na UM. Kwa hivyo, sura hii imejibu maswali yaliyoongoza utafiti ambayo yalilenga kutimiza malengo mahususi matatu kwa kubainisha na kuchanganua makosa ya kisarufi, sababu za kufanyika kwa makosa ya kisarufi katika vyombo vya habari na hatua za kuepuka makosa ya kisarufi kwenye vyombo vya habari vya Tanzania, hususani katika televisheni za TBC1, ITV na STAR TV.

SURA YA TANO

MUHTASARI, HITIMISHO NA MAPEDEKEZO

5.1 Utangulizi

Sura hii inawasilisha kwa muhtasari juu ya utafiti uliozaa tasnifu hii. Hivyo, sura inatoa muhtasari wa jumla wa utafiti, muhtasari wa matokeo ya utafiti, hitimisho na mapendeleko ya kitaaluma kuhusu mada ya utafiti.

5.2 Muhtasari wa Jumla

Utafiti huu ulilenga kuchunguza makosa ya kisarufi katika vyombo vyahabari vya Tanzania, umahususi uliwekwa kwa TBC1, ITV na STAR TV. Katika kutimiza azma hiyo, utafiti ulifanyika kwa hatua kadhaa. Hatua hizo zimewasilishwa kwenye tasnifu hii kwa sura.

Sura ya kwanza ya tasnifu imetoea taarifa za awali kuhusu utafiti ulifanyika. Sura inaeleza usuli wa mada kwa kufafanua namna ambavyo makosa ya kisarufi ni sehemu ya makosa ya lugha na kufafanua kwa ufupi historia ya vyombo vyahabari vilivyochunguzwa. Baada ya usuli, sura imefafanua kwa uwazi tatizo la utafiti. Ilibainishwa kwamba pamoja na watafiti kadha wa lugha ya Kiswahili kuandika juu ya makosa ya lugha kwenye vyombo vyahabari vya Tanzania, bado makosa hayo yanaendelea kufanyika ndani ya vyombo vyahabari vya Tanzania. Hali hii inaonesha kuwa kuendelea kufanyika kwa makosa ya lugha katika vyombo vyahabari vya Tanzania, ni tatizo ambalo halijapatiwa utatuzi na bado linahitaji kuendelea kuchunguzwa. Pia imeonekana kuwa watafiti walioshughulikia makosa ya lugha kwenye vyombo vyahabari vya Tanzania, walijikita kwenye redio na magazeti na kusahau televisheni. Aidha, malengo mahususi ya utafiti ambayo ni kubainisha

makosa ya kisarufi, kubainisha sababu za makosa ya kisarufi na kubainisha hatua za utatuza wa mkaosa hayo kwenye vyombo vya habari, yaliwekwa bayana. Maswali yaliyoongoza utafiti ili kutimiza malengo yaliwekwa wazi huku vipengele vya umuhimu na mawanda ya utafiti vimebainishwa pia.

Sura ya pili ilihu mapitio ya kazi tangulizi pamoja na nadharia zilizoongoza utafiti. Sura imefafanua kwa kina baadhi ya maandiko ya wataalamu kuhusu vipengele vya dhana ya makosa ya lugha na makosa ya kisarufi; makosa ya lugha na ya kisarufi kwa watumiaji wa lugha; makosa ya lugha na ya kisarufi kwenye vyombo vya habari vya Kiswahili na lugha nyinginezo. Katika kuhakiki mapitio hayo, mtatifi ameeleza kwa kina jinsi maandiko hayo yalivyomsaidia katika utafiti huku akibainisha utofauti na uhusiano kati ya maandiko hayo na utafiti huu. Aidha, pengo la kimaarifa ambalo watangulizi hawakuliona lilifafanuliwa kwa uwazi. Imeelezwa kuwa watafiti waliotafiti mada ya makosa ya lugha katika vyombo vya habari vya Tanzania hawakuchunguza na kuchanganua makosa ya kisarufi yanayotendeka katika televisheni zinazotumia Kiswahili bali maandiko mengi yalijikita kwenye makosa ya lugha kwenye magazeti na redio za Tanzania na kueleza kuwa vyombo vya habari hivyo huchangia kuharibu Kiswahili kwa kufanya makosa ya mara kwa mara katika utoaji wa matangazo yao (rejea §2.3). Vilevile, sura ilibainisha na kufafanua nadharia zilizoongoza utafiti. Viunzi vya UHK na UM vilielezwa kwa kina kama nadharia ambazo ziliongoza utafiti na kuonesha jinsi ambavyo zilimsaidia mtatifi kufikia malengo yake.

Katika sura ya tatu ya tasnifu hii, kumefafanuliwa na kuoneshwa kwa uwazi mbinu za utafiti ambazo zilitumika. Sura imefafanua kuwa utafiti ulifanyika Tanzania, wilaya

ya Kwimba. Vipengele vilivyofuata baada ya eneo la utafiti ni wango la utafiti pamoja na sampuli. Wango lililotafitiwa ni vyombo vya habari na hadhira yake huku sampuli iliyoteuliwa ilikuwa ni vyombo vya habari 3, matini 105 za habari pamoja na wasailiwa 20. Mbinu za usampulishaji zimefafanuliwa kwa uwazi ili kuonesha jinsi sampuli iliyopatikana ilikuwa faafu. Baada ya hapo, kipengele cha mbinu za ukusanyaji wa data kilifuata na kuelezwu kuwa usomaji wa matini, utazamaji na usikilizaji, na hojaji ni mbinu pekee zilizotumika kupata data za utafiti. Kipengele cha mwisho cha sura hii kilikuwa ni mkabala wa uwasilishaji na uchambuzi wa data. Sura imefafanua kwa kina kuwa mkabala wa kitaamuli ultumika kuchambua data na kuwasilisha matokeo.

Sura ya nne ndiyo ilikuwa kiini cha tasnifu hii. Imewasilisha data, kuzichambua pamoja na kutoa matokeo ya utafiti. Sura ililenga kufafanua majibu ya maswali ya utafiti yaliyosaidia kutimiza malengo (ufafanuzi zaidi utafanyika kwenye § 5.3 katika sura hii). Kwa ufupi, sura imeonesha aina za makosa ya kisarufi yanyofanyika kwenye vyombo vya habari vya Tanzania, sababu za makosa hayo na hatua za utatuzi wake pamoja na mjadala wa jumla wa sura hiyo.

Sura ya tano ni sura ambayo imefanya majumuisho ya tasnifu hii. Sura hii imewasilisha muhtasari wa jumla, matokeo ya utafiti na mapendekezo ya kitaaluma juu ya mada ya utafiti.

5.3 Muhtasari wa Matokeo

Matokeo ya utafiti yamewasilishwa kwa kuzingatia malengo mahususi yaliyowekwa ili kutimiza lengo kuu. Matokeo hayo yamechambuliwa kwa kina kwenye §4.2, §4.3

na §4.4 katika tasnifu hii. Kwa kuzingatia malengo hayo, muhtasari wa matokeo ni kama ifuatavyo:

Lengo la kwanza lilikuwa kubainisha makosa ya kisarufi katika habari za TBC1, ITV na STAR TV. Utafiti ulifanikiwa kutimiza lengo hilo kwa kukusanya data zilizothibitisha uwapo wa makosa ya kisarufi kwenye channeli zilizochunguzwa. Imebainika kuwa vyombo vya habari hivyo vinafanya makosa ya kisarufi yanayohusu vipengele vitano vya sarufi ya Kiswahili ambavyo ni msamiati, matamshi, muundo na semantiki. Data zimeonesha kwamba kila kipengele kimesheheni makosa kadhaa. Makosa ya kimsamiati yaliyobainishwa na kuchanganuliwa ni matumizi ya maneno ya Kiingereza; maneno yasiyostahili; kuandika maneno isivyo (kuunganisha na kutenganisha maneno); udondoshaji na uchopekaji wa maneno; na, matumizi ya maneno yasiyo sanifu. Kwa upande wa kipengele cha matamshi, data zimethibitisha kuwa watangazaji wa vyombo vya habari vilivyochunguzwa wanafanya makosa katika utamkaji wa maneno ya Kiswahili. Walitamka baadhi ya maneno isivytakiwa. Kwa mfano, maneno *wakati*, *aidha*, *kumalizika* na *katika* yalitamkwa isivyo kama ***waakti***, ***eidha***, ***kumalidhika*** na ***kalika***. Pia, kwa upande wa kipengele cha maumbo, wanahabari walifanya makosa ya maumbo ya umoja na wingi, uchopekaji na udondoshaji wa vipashio vya maumbo ya maneno. Kwa muundo, makosa yaliyobainishwa ni upatanisho wa kisarufi, mpangilio usio sahihi wa maneno kwenye tungo na urudiaji wa maneno. Makosa ya mwisho kubainishwa yalikuwa ni ya kipengele cha kisemantiki ambapo utafiti ulibainisha makosa ya utata, kukosa mantiki na kutokueleweka kwa vifungu vya maneno katika habari.

Lengo la pili lilikuwa ni kubainisha sababu za makosa ya kisarufi katika habari za TBC1, ITV na STAR TV. Data zimeonesha kuwa sababu mbalimbali ni chanzo cha wanahabari kufanya makosa ya kisarufi katika utoaji wa habari. Sababu hizo ni kukosa umahiri wa lugha ya Kiswahili; athari ya lugha ya kwanza; kasumba; kutomudu sarufi ya Kiswahili; ufahamu wa lugha mbili: Kiswahili na Kiingereza na ukosefu wa taaluma ya lugha (isimu ya Kiswahili). Hizi ni sababu kuu zilizobainishwa kutoka katika data zilizochanganuliwa kwa mujibu wa watafitiwa.

Lengo la tatu lilikuwa ni kubainisha hatua za kuchukuliwa ili kuepuka makosa ya kisarufi katika habari za TBC1, ITV na STAR TV. Matokeo yanaonesha kuwa zipo hatua ambazo zikichukuliwa zinaweza kusaidia wanahabari na watumiaji wa Kiswahili kwa ujumla, kuepuka kufanya makosa ya kisarufi. Sababu zilizobainishwa ni ufundishaji wa taaluma ya lugha kwa wanahabari; utoaji wa semina za mara kwa mara za matumizi ya lugha kwa wanahabari; vyombo vyta habari kuajiri na kutumia wataalamu wa lugha; kutungwa kwa sheria za matumizi ya lugha; na kufanya uhariri wa kina kabla ya kutoa habari.

5.4 Hitimisho

Utafiti huu ulisukumwa na madai ya wanataaluma wa lugha kuwa vyombo vyta habari vyta Tanzania hufanya makosa ya lugha ya mara kwa mara na yanayoharibu ukuaji wa Kiswahili. Kwa kuwa madai hayo yalitolewa kutohana na maandiko yaliyochunguza makosa ya lugha kwenye redio na magazeti na bado makosa ya lugha yanaendelea kufanyika, mtafiti aliamua kuchunguza makosa ya kisarufi kwa upande wa televisheni ili kuziba pengo kwa upande huo. Kwa kuongozwa na

nadharia ya UHK na UM, utafiti umefanikiwa kubainisha aina za makosa ya kisarufi, sababu za makosa hayo na hatua za kufuatwa ili kuyaepuka. Utafiti ulibainisha kuwa vyombo vya habari vya TBC1, ITV na STAR TV vina makosa ya kisarufi ya kimsamiati, kimamatamshi, kimaumbo, kimuundo na kisemantiki. Makosa hayo yalifanywa na wanahabari wa vyombo hivyo wakati wa kuwasilisha habari zao kupitia usomaji na uandishi wa habari za runingani na tovutini.

5.5 Mapendekezo

5.5.1 Mapendekezo ya Kuepuka Makosa

Pamoja na data za lengo la tatu kuonesha hatua mbalimbali zilizopendekezwa na watafitiwa, mapendekezo yafuatayo yanafaa kuzingatiwa ili kusaidia wanahabari wa Tanzania kuepuka makosa ya lugha:

Kuandaa Vipindi Mbalimbali vya Matumizi Sahihi ya Kiswahili: Taasisi zinazoratibu matumizi ya Kiswahili kama BAKITA na BAKIZA kwa kushirikiana na vyombo vya habari, zinapaswa kuandaa vipindi vingi vya matumizi ya lugha katika redio na televisheni. Vipindi hivyo vinapaswa kurushwa hewani kupitia vyombo mbalimbali vya habari ili visikike na kutazamwa na watumiaji wa lugha. Vipindi vieleze matumizi sahihi na yasiyo sahihi ya lugha ya Kiswahili. Vifafanue kwa kina aina ya mazungumzo kulingana na muktadha, hadhi, mada, uhusiano wa wazungumzaji, rika na shughuli mbalimbali ili kuwasaidia watumiaji wa Kiswahili kujua namna ya kuwasiliana kwa usahihi na kutumia Kiswahili fasaha. Hili litasaidia kueneza elimu ya matumizi sahihi ya Kiswahili pamoja na kanuni zinazoongoza lugha kwa wanahabari na hadhira ya vyombo vya habari.

Kutoa Machapisho ya Matumizi Sahihi ya Kiswahili: Wataalamu na watafiti wa masuala ya lugha wakishirikiana na mabaraza ya Kiswahili (BAKITA na BAKIZA), taasisi za uchunguzi wa lugha kama TATAKI na vyama vya Kiswahili kama CHAUKIDU, CHALUFAKITA na CHAKAMA, wafanye tafiti zinazohusu makosa ya lugha yanayofanywa mara kwa mara na watumiaji wa Kiswahili. Baada ya hapo, watoe machapisho mengi na kuyasambaza kwa wadau wa lugha ili kuwasaidia kupunguza makosa yasiyo ya lazima. Ushauri kama huu umetolewa na msailiwa mmojawapo aliyesema kuwa ‘*taasisi za ukuzaji wa lugha ya Kiswahili ziandae machapisho na mijadala itakayowahusisha waandishi ili kupunguza makosa katika tasinia ya habari na mawasiliano*’ (MS15). Maoni haya yanaafikiana na pendekezo linalofafanuliwa hapa. Hivyo, machapisho, miadhara pamoja na mijadala juu ya hali ya matumizi ya lugha kwenye vyombo vya habari vinavyotumia Kiswahili itasaidia kwa namna fulani kupunguza makosa ya kisarufi kwani watumiaji wa Kiswahili watapata ufahamu juu ya kanuni na matumizi sahihi ya lugha.

Matumizi ya Mara kwa Mara ya Kamusi na Machapisho Mbalimbali ya Lugha: Wakati mwingine kukosa umahiri wa lugha kwa kiwango cha juu husababishwa na kutokuwa na welewa wa kanuni mbalimbali za lugha. Ili kuepuka hali hiyo, wanahabari na watumiaji wa lugha kwa ujumla, hawana budi kujenga tabia ya kujisomea kamusi na maandiko mbalimbali yayonahusu lugha. Utumiaji wa kamusi wa mara kwa mara utawafanya wanahabari kumudu msamiati wa Kiswahili na hivyo kuepuka makosa ya matumizi ya maneno yasiyofaa, urudiaji wa maneno na matumizi ya maneno ya Kiingereza katika mawasiliano ya Kiswahili. Ushauri kama huu umetolewa pia na Omoera (2008b).

5.5.2 Mapendekezo ya Tafiti Zingine juu ya Mada hii

Hakuna utafiti wowote ambao hufanyika na kushughulikia kila kitu kwa sababu ya malengo yake. Hivyo, kulingana na mipaka na malengo ya utafiti huu, malengo yaliyowekwa yametimizwa. Hata hivyo, mtafiti wakati wa utafiti huu alibainisha mapengo ambayo anaamini yanahitaji kuzibwa kwa kufanya tafiti nyingine zaidi ya huu kuhusu mada ya makosa ya lugha katika vyombo vya habari na watumiaji wa Kiswahili kwa ujumla.

Kwanza, unahitajika utafiti wa kina wa matimizi ya lugha kwa watumiaji wa Kiswahili ili kujua ni kwa kiwango gani wanatumia vizuri au vibaya lugha hii. Na je, ni kwa kiwango gani matumizi hayo yanaimarisha lugha hiyo? Je, matumzi hayo yanakuza au yanadidimiza Kiswahili?

Pili, mtafiti anapendekeza kuwa tafiti nyingine zifanyike kujua namna ambavyo mitindo ya lugha na vipindi mbalimbali (tofauti na habari) kwenye vyombo vya habari vya Tanzania vinachangia makosa ya lugha.

Tatu, tafiti linganishi zifanyike kuhusu makosa ya lugha kwenye vyombo vya habari vya Tanzania kujua ni chombo kipi hufanya makosa mengi kuliko vingine na kwa sababu gani.

Nne, mtafiti alikutana na makosa ya uandishi wakati wa utafiti. Hivyo, unahitajika utafiti wa kutathmini makosa ya uandishi katika TBC1, ITV na STAR TV na vyombo vya habari vingine vya Kiswahili.

Tano, utafiti huu ulichunguza channeli za televisheni tu, hivyo unahitajika utafiti mwingine wa kuchunguza makosa ya lugha na hasa ya kisarufi katika redio za

mashirika yaliyochunguzwa. TBC ni shirika lenye channeli za redio kama TBC Taifa, TBC2 (televisheni), TBC FM; IPP ambalo ni shirika linalomiliki ITV lina channeli nyingine za Kiswahili za redio kama Redio One na Capital Redio, East Africa Redio na televisheni ya EATV; shirika la Shahara Media linalomiliki STAR TV lina channeli nyingine za redio kama Redio Free Africa (RFA) na Kiss FM. Hivyo, utafiti ukifanyika kwa channeli hizo tunaweza kupata picha halisi ya matumizi ya lugha na makosa ya lugha kwa vyombo vya habari hivyo.

Sita, mtafiti amebaini sababu za makosa ya lugha ambazo hazikubainishwa na watafitiwa wa utafit huu. Hivyo, anapendekeza zifanyiwe utafiti wa kina kujua namna zinavyochangia makosa ya lugha kwenye vyombo vya habari vya Tanzania. Sababu hizo ni: Uhaba wa msamiati kwa mtumiaji wa lugha husika; athari ya lugha ya Kiingereza; ukosefu wa umakini wakati wa kuandika na kuhariri; uteuzi mbaya wa msamiati; kuandika au kuzungumza harakaharaka.

Saba, mtafiti anashauri kwamba watafiti wengine wafanye utafiti unaochunguza athari za makosa ya kisarufi na makosa ya lugha kwa ujumla kwa watumiaji wa Kiswahili na ukuaji wa lugha yenye.

MAREJELEO

- Adaku, N.G. (2016). *Grammatical Error Analysis of Selected News Scripts of the Broadcasting Corporation of Abia State Radio, Umuahia.* (M.A Thesis) University of Nigeria, Nigeria.
- Aditya, P.D., & Amita, D. (2017). Linguistic Divergences in Newspaper's Headlines. *International Journal of Engineering Technology Science and Research 4* (7), 858-864.
- Akbari, E., & Kheirabadi, R. (2015). A Linguistic Analysis of Errors in News Agencies and Websites of Iran. *Theory and Practice in Language Studies* 5, (11) 2340 - 2347.
- Ayodele, O. (1988). African Print Media Misuse of the English Definite Article 'The': A Content Analysis of Seven Nigerian Newspapers1 Lead Items. *Africa Media Review 2* (3), 92-109.
- BAKITA. (2015). *Kamusi Kuu ya Kiswahili.* Toleo la 1. Dar esSalaam: Longhorn Publishers.
- Berger, C, R. (2003). Message Production Skills in Social Interaction. In J.O. Greene & B.R. Burleson (eds.), *Handbook of Communication and Social Interaction Skills* (pp.257-289). New Jersey: Lawrence Erlbaum Associates Publishers.
- Bhattacherjee, A. *Social Science Research: Principles, Methods, and Practices* (2nd ed). *Textbooks Collection.* Book 3.
- Biber, D., Johansson, S., Leech, C., Conrad, S., & Finegan, E. (1999). *Longman Grammar of Spoken and Written English.* England: Pearson Education Limited.
- Bukagile, G.R. (2007). *Kiswahili kwa Shule za Sekondari: Kidato cha Kwanza:* Dar es Salaam: Nyambari Nyangwine Publishers.

- Buliba, A., Gwachi, M., & Matinde, R. (2014). *Misingi ya Nadharia na Mbinu za Utafiti*. Mwanza: Serengeti Educational Publishers.
- Cassidy, W. P. (2007). Online News Credibility: An Examination of the Perceptions of Newspaper Journalists. *Journal of Computer-Mediated Communication* 12, 478–498.
- Chomsky, N. (1965). *Aspects of the Theory of Syntax*. USA: MIT Press.
- Conboy, M. (2003). Parochializing the Global: Language and the British tabloid Press. In J.Aitchison & D.M. Lewis (eds.), *New Media Language* (pp.46-54) London: Routledge.
- Corder, S.P. (1967). The Significance of Learner's Errors. *International Review of Applied Linguistics in Language Teaching* 5 (4), 161-170.
- Cunningsworth, A. (1987). *Evaluation and selecting EFL Teaching Materials*. London: Heinemann Education Book.
- DeCapua, A. (2008). *Grammar for Teachers: A Guide to American English for Native and Non-Native Speakers*. New York: Springer Science+Business Media, LLC.
- Feltsen, P. (2009). *Language Acquisition and the Errors We Make: A Comparison between Beginners and Intermediate Learners* (B.A Research Paper).Mid Sweden University, Sweden.
- Frost, J. (2016). 20 Writing Mistakes Even Native Speakers Make (Infographic). <https://www.grammarcheck.net/writing-mistakes-native-speakers/>. Ilisomwa 6/8/2020 saa 4.23 usiku.
- Fry, D. B. (1969).The Linguistic Evidence of Speech Errors. *BRNO Studies in English* 8, 69-74.
- Gass, S. M. & Selinker, L. (2008). *Second Language Acquisition: An Introductory Course*. (3rd ed). New York: Routledge, Taylor & Francis.

- Gbara, N. B. (2001). *Grammatical Errors in the Nigerian Print Media and their Effect on Audience Perception and Behaviour* (Master's Thesis). University of Nigeria, Nigeria.
- Getyngo, M. Peter. (1997). *Kenyan Newspaper Discourse: An Investigation in Typology and Ideology* (Master's Dissertation). University of Nairobi, Kenya.
- Gowon, R.P. (2009). Effects of Television and Radio on Speaking and Writing Skills of Senior Secondary School Students in Jos Metropolis. *African Research Review* 3 (2), 92-108.
- Greene, J. O. (2003). Models of Adult Communication Skill Acquisition: Practice and the Course of Performance Improvement. In J.O. Greene & B.R.Burleson (eds.), *Handbook of Communication and Social Interaction Skills* (pp.52-91). New Jersey: Lawrence Erlbaum Associates Publishers.
- Habwe, J. & Karanja, P. (2004). *Misingi ya Sarufi ya Kiswahili*. Nairobi: Phoenix Publishers.
- Hargie, O. (2006). Skill in Theory: Communication as Skilled Performance. In O. Hargie (ed.), *The Handbook of Communication Skills* (pp.7-36). London&NewYork: Routledge.
- Hassoon, F.K. (2016). A Stylistic Analysis of Selected Newspaper's Stories. *European Academic Research IV* (2), 1228-1247.
- Hohenberger, A., & Waleschkowski, E. (2005). Language Production Errors as Evidence for Language Production Processes – The Frankfurt Corpora. In S.Kepser & M.Reis (eds.), *Linguistic Evidences: Empirical, Theoretical and Computational Perspectives* (pp.285-305). Berlin: Mouton de Gruyter.
- Huang, C.-M., Wu, M.-C. & Chang, C.-C. (2007). Error Detection and Correction Based On Chinese Phonemic Alphabet in Chinese Text. *Modeling Decisions for Artificial Intelligence: Proceedings of 4th International Conference*, MDAI 2007, (pp.463-476). Kitakyushu, Japan.

- Idarous, A. (1995). Tafsiri katika Vyombo vyat Habari Tanzania. Katika S.A.K. Mlacha (mh.), *Kiswahili na Vyombo vyat Habari* (kur.52-60). Dar es Salaam: TUKI.
- Idarus, A. S. (2010). Makosa Yanayofanywa Mara kwa Mara katika Matumizi ya Kiswahili. Katika TUKI (wah.), *Makala za Semina ya Kimataifa ya Waandishi wa Kiswahili 1: Lugha ya Kiswahili* (Tol.3, kur. 173-187). Dar es Salaam: TUKI.
- Isani, S. (2011). Of Headlines & Headlinese: Towards Distinctive Linguistic and Pragmatic Genericity. *ASP La Revue Du GERA* 60. Ilipakuliwa kutoka <http://journals.openedition.org/asp/2523>; DOI:10.4000/asp.2523.
- Jagero, J. A., Mohochi, E.S., & Indede, F. (2013). The Usage of Kiswahili in Blog Discourse and the Effect on its Development. *International Journal of Humanities and Social Science 3 (14)*, 192-199.
- Jin, X. (2019). A Case Study of Communication Difficulties between a Chinese Advanced Learner and Native Speakers. *Journal of Language Teaching and Research 10* (1), 114-125.
- Jing, H., Xiaodong, H., & Yu, L. (2016). Error Correction in Oral Classroom English Teaching. *English Language Teaching 9* (12), 98-103.
- Kadeghe, M. (2012). *Kiswahili kwa Shule za Sekondari Tanzania: Kidato cha Kwanza* (Tol.3). Dar es Salaam: Jamana Printers Ltd.
- Karlsson, M., Clerwall, C., Nord, L. (2016). Do not Stand Corrected: Transparency and Users' Attitudes to Inaccurate News and Corrections in Online Journalism. *Journalism & Mass Communication Quarterly 94* (1), 148-167.
- Kawonga, G. A. (2017). Ubeberu wa Kiisimu na Mustakabali wa Lugha za Kiafrika: Mapitio

ya Sera ya Luga Tanzania. *MULIKA: Toleo Maalum la Makala ya Kongamano la CHAUKIDU*, 83-96.

Kihore, Y. M. (2004). Masuala ya Kisarufi katika Magazeti ya Mitaani ya Kiswahili –Tanzania. *Swahili Forum* (XI), 107-119.

Kihore, Y. M. (2003). *Sarufi Maumbo ya Kiswahili Sanifu (SAMIKISA) Sekondari na Vyuo*. Dar es Salaam: TUKI.

King'ei, K. (2000). Matatizo ya Matumizi ya Luga katika Vyombo vya Habari: Mifano kutoka Kenya. *AAP64: Swahili Forum* (VII), 45-56.

King'ei, K., & Kobia, J. (2007). Luga kama Kitambulisho: Changamoto ya Sheng Nchini Kenya. *Nordic Journal of African Studies* 16 (3), 320–332.

Kothari, C.R. (2004). *Research Methodology: Methods and Techniques* (2nd ed.). New Delhi: New Age International (P) Ltd., Publishers.

Kumar, R. (2011). *Research Methodology a step-by-step guide for beginners* (3rd ed.). London: SAGE Publications Ltd.

Ligembe, N. N (2017). *Kitangulizi cha Fonetiki na Fonolojia ya Kiswahili*. Dar es Salaam: Vision Strategic Impact Limited/Afro Plus Industries Ltd.

Lopez, V & Whitehead, D. (2013). Sampling Data and Data Collection in Qualitative research. *Nursing & Midwifery Research: Methods and Appraisal for Evidence Based Practice* 123, 123-137.

Maina, S. (2013, 13 Julai). Makosa katika Kiswahili, Usahihi Wake. *Mwananchi*. Ilipakuliwakutoka <https://www.mwananchi.co.tz/kolamu/lugha-yetu/Makosa-katika-Kiswahili--usahihi-wake/1614740-1914190-11lm5jk/index.html>

_____ (2014, 15 Juni). Vyombo vya Habari Gwiji wa Kuharibu Kiswahili. *Mwananchi*. Ilipakuliwa kutoka <https://www.mwananchi.co.tz/kolamu/Vyombo-vya-habari-gwiji-wa-kuharibu-Kiswahili/1607214-2349288-cp8y5vz/index.html>

- Makunja, G.S. (1995). Sarufi na Msamiati katika Vyombo vya Habari. Katika S.A.K. Mlacha (mh.), *Kiswahili na Vyombo vya Habari* (kur. 13-23). Dar es Salaam: TUKI.
- Masebo, J.A., & Nyangwine, N.C.M. (2016). *Nadharia ya Lughu Kiswahili 1: Kidato cha 5 & 6*. Dar es Salaam: Nyambari Nyangwine Publishers.
- Massamba, D. P. B. (1995). Kiswahili kama Lughu ya Mawasiliano. Katika S.A.K. Mlacha (mh.), *Kiswahili katika Kanda ya Afrika Mashariki: Historia, Matumizi na Sera* (kur. 1-11). Dar es Salaam: TUKI.
- _____. (2007). *Kamusi ya Isimu na Falsafa ya Lughu* (Tol.2). Dar es Salaam: TATAKI.
- Massamba, D.P.B., Kihore, Y.M., na Hokororo, J.I. (1999). *Sarufi Miundo ya Kiswahili Sanifu*. Dar es Salaam: TUKI.
- Massamba, D.P.B., Kihore, Y.M., na Msanjila, Y.P. (2004). *Fonolojia ya Kiswahili Sanifu (FOKISA) Sekondari na Vyuvo*. Dar es Salaam: TUKI.
- Matinde, R. S. (2012). *Dafina ya Lughu, Isimu na Nadharia*. Mwanza: Serengeti Educational Publishers.
- Media Ownership Monitor Tanzania. (2018). *Mambo ya Umiliki wa Vyombo vya Habari*. Ilipakuliwa kutoka <http://tanzania.mom-rsf.org>.
- Mochiwa, Z.S.M. (2000). Sintaksia ya Vivumishi vya Kiswahili. *Kiswahili: Jarida la Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili 63*, 23-36.
